# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Agosti 7, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579990

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



ST.JOSEPH UNIVERSITY In Tanzania

"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"

Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA

SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on 24th August, 2019, "Entrance is free". For details www.alumni.sjuit.ac.tz

For more information contact: +255 676 504 147 +255 745 281 505




## Aliyepata ajali gari la RC afariki dunia

UKURASA 2

# Manara aburuzwa kortini Simba Day



UKURASA 2



# NDEGE NYINGINE YAANGUKA, YAUNGUA

Mabaki ya ndege ya Shirika la Tropical Air yenye namba za usajili 5H-NOW, iliyopata ajali baada ya kuanguka wakati ikitaka kupaa katika kisiwa cha Mafia, mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### SERIKALI KUAJIRI 500 UHAMIAJI

SERIKALI imesema imebaini upungufu wa askari katika Idara ya Uhamiaji hasa maeneo ya viwanja...

UKURASA WA 7

### FAMILIA ILIVYONUSURIKA KUUAWA NA WANAKIJIJI

KUNDI la wananchi ambao idadi yao haijafahamika, wamevamia nyumbani...

UKURASA WA 26

### WAZIRI ASITISHA OPERESHENI KUCHOMA NYUMBA, MAZIZI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesitisha operesheni ya kuwaondoa...

## Waziri Mkuu aanika fursa SADC

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA YATETEMESHA NCHI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Haji Manara aburuzwa mahakamani Simba Day

**Na Mwandishi Wetu**

MSEMAJI wa Klabu ya Simba ya jijini Dar es Salaam Haji Manara na wenzake watatu wameburuzwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akidaiwa deni na fidia ya Sh. milioni 83.3 baada ya kupokea bidhaa zenye nembo ya Dela Boss Perfume bila kuzilipia.

Mbali na fedha hizo, mlalamikaji Abu Masoud Al Jahdhamy LLC, ameiomba mahakama kuwaamuru walalamikiwa, Manara, Beatrice Ndungu na Palm General Supply, kumlipa fidia nyingine itayoona zinafaa na gharama za mawakili.

Kesi hiyo ya madai namba 128/2019 ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Wanjah Hamza na imepigwa kalenda mpaka Agosti 29, mwaka huu itakapotajwa tena.

Katika madai ya msingi, mlalamikaji amefungua kesi hiyo akiwadai walalamikiwa fedha hizo baada ya kuwasambazia bidhaa yenye nembo ya Dela Boss Perfume 'Tanzania' zilizotengezwa Dubai.

Ilidaiwa kuwa mlalamikaji aliingia mkataba na Manara Desemba 19, 2018 kwa kuchapa bidhaa zenye maneno hayo.

Katika mkataba huo, mlalamikaji alitakiwa kupata asilimia 70 na Manara asilimia 30 na kwamba faida itakayopatikana angemrudishia mlalamikaji gharama za uwekezaji wa kufikisha bidhaa jijini Dar es Salaam.

Januari 21, 2019 mlalamikaji kupitia kampuni ya AMA Trading LLC, ilituma bidhaa hizo jijini Dar es Salaam ambazo zina thamani ya Sh. milioni 46 na zilipokelewa na mlalamikiwa wa pili, Ndungu na wa tatu kama mawakala.

Januari 21, 2019 mlalamikaji alituma fomu ya madai ya Sh. 83,300,000 kwa mlalamikiwa wa pili na wa tatu akitaka kulipwa faida ya uwekezaji na kiasi kilichotumika kununulia bidhaa hizo pamoja na faida.

Walalamikiwa walipokea bidhaa hizo na mpaka sasa hawajalipa chochote pamoja na kudaiwa kwa maneno na maandishi kutoka kwa mlalamikaji.

Mlalamikaji anadai kuwa kutokana na kitendo hicho kimemsababishia usumbufu mkubwa na hasara katika biashara zake.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Kiwanda cha Ital Shoe, Novatus Kaijange (wa pili kulia), katika Maonyesho ya Nne ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), yanayoendelea, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaliwa: Maonyesho SADC fursa pekee kwa Watanzania

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Wiki ya Maonyesho ya nne ya Viwanda ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ni fursa pekee ya kutangaza bidhaa zinazozalishwa nchini.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua mabanda kwenye maonyesho hayo yanayoendelea kwenye Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Maonyesho hayo ambayo yalifunguliwa juzi na Rais John Magufuli, yanafanyika katika maeneo matatu ambayo ni JNICC, viwanja wa Gymkhana na viwanja vya Karimjee. "Nimekuja kufanya ufuatiliaji wa maandalizi ya Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi za SADC, nimekuta yanaendelea vizuri. Nimekuja kuangalia mwitikio wa wajasiriamali wa pande zote mbili za Muungano pamoja na wajasiriamali kutoka nchi wanachama wa SADC, na pia mwitikio wa wananchi wetu ukoje," alisema.

Waziri Mkuu alisema fursa hiyo ni muhimu kwa Watanzania kuonyesha bidhaa za ndani ili wageni wanaokuja wajue kuna bidhaa zipi zinazozalishwa nchini. "Tumetoa fursa kwa nchi za SADC zote nao pia waonyeshe bidhaa zao. Maonyesho haya ni ya wazi, Watanzania wanayo nafasi ya kuja kuona na kujifunza," alisema.

Alisema mbali ya fursa ya masoko, Tanzania inayo pia fursa ya kupata teknolojia mpya na za kisasa ikiwa ni pamoja na wawekezaji wa viwanda vya usindikaji bidhaa mbalimbali. "Tumeona utaalamu unaotumika kutengeneza bidhaa mbalimbali, hii maana yake ni kwamba tunajifunza na teknolojia zinazotumika," alisema na kuongeza: "Tunayo fursa ya kukaribisha viwanda kutoka nje ya nchi, wote hapa wameleta bidhaa zao. Pia tunawakaribisha waje waanzishe viwanda kwa ubia na Watanzania. Sisi tunayo ardhi, tunazalisha mazao mengi tu, kwa hiyo mbia wa nje anaweza kuunganisha mtaji na Mtanzania na wakajenga kiwanda hapa nchini."

Mbali ya fursa za kiuchumi kwao binafsi, Majaliwa aliwataka washiriki watangaze vivutio vya utalii vilivyopo nchini ambavyo vitasaidia kuwafanya wageni wanaoshiriki mkutano huo watamani kubaki nchini na kuvitembelea.

"Watanzania tutumie nafasi hii kutangaza vivutio vingine tulivyonavyo. Mbuga za wanyama tunazo nyingi, tunao Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote barani Afrika na huwezi kuupanda kutokea popote. Ili uupande, ni lazima uje Tanzania," amesema.

"Pia tuna eneo maarufu la Olduvai Gorge ambalo ni chimbuko la binadamu wa kwanza duniani, na hili liko eneo liko Ngorongoro. Tuna fukwe nzuri, zenye mchanga mzuri ambazo ukikaa wala huwezi kuchafuka, zina urefu wa zaidi ya km. 1,400 kutokea Tanga hadi Mtwara," aliongeza.

Mapema, Waziri Mkuu alifanya kikao na Mawaziri wa Mambo ya Nje, Utumishi na Utawala Bora, Viwanda na Biashara wa SMT, Viwanda, Biashara, Wazee na wa Zanzibar (SMZ), Naibu Mawaziri wa Tamisemi, Mambo ya Nje na Mifugo na Uvuvi na kuwapa maelekezo ya kuboresha maandalizi hayo. Kikao hicho pia kilihudhuriwa na makatibu wakuu wa wizara hizo.

## Aliyepata ajali gari la RC afariki dunia

**Na Romana Mallya**

KASOBI Shida (26), mtoto wa dereva wa Mkuu wa Mkoa wa Mara aliyepata ajali akiendesha gari linalotumiwa na baba yake, Shida Masaba (55) kumwendesha mkuu wa mkoa huo, amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu kutokana na ajali hiyo.

Ajali hiyo ilitokea Jumapili baada ya baba wa kijana huyo kurejea nyumbani akitumia gari hilo aina ya Land Cruiser lenye namba za usajili STL 5961 na Kasobi kulichukua na kuondoka nalo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Juma Ndaki, aliliambia Nipashe jana kuwa kijana huyo, alifariki dunia usiku wa kuamkia jana.

Alisema baada ya ajali hiyo, Kasobi alilazwa katika Hospitali ya Rufani ya Musoma akiendelea na matibabu ya majeraha aliyopata.

Alisema taratibu za mazishi zinafanywa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Kamanda Ndaki aliongeza kuwa baada ya ajali hiyo, baba wa kijana huyo, Masaba alipata mshtuko na kulazwa hospitalini na hadi kifo cha mwanawe kinatokea, alikuwa hajaruhusiwa kwenda nyumbani.

HABARI KITAIFA

# Ulinzi waimarishwa kisa kudhibiti viboko

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

ASKARI wa wanyamapori wa Pori la Akiba la Rukwati mkoani Katavi, wamewasili katika kijiji cha Shanwe Manispaa ya Mpanda kwa ajili ya kuweka ulinzi katika bwawa la Milala lililovamiwa na viboko zaidi ya 60.

Askari hao wamepelekwa ili kuimarisha usalama wa wananchi wa kijiji hicho kutokana na hatari zinazotokana na viboko hao.

Meneja wa pori hilo, Pachwi Mlwina, alisema uamuzi huo umetokana na athari ambazo wananchi hao wamekuwa wakizipata kutokana na kuwapo kwa viboko hao kwani hali inazidi kuwa mbaya kutokana na kuwajeruhi na kuwaua.

Alisema kwa muda mrefu wananchi hao wamekuwa wakiomba serikali kuwavuna viboko hao kwa kuwa wamekuwa kero kwao kutokana na kula mazao yao, kuwanyima uhuru kutokana na kuingia mpaka kijijini na kuwadhuru.

Meneja huyo alisema kutokana na hali hiyo, uongozi wa pori hilo la akiba umeamua kuweka kambi maalumu ya askari wake ambao wataimarisha ulinzi ili kuwalinda wananchi hao kwa kuwa hawawezi kuvumilia kuona watu wakiendelea kupoteza maisha wakati uwezo wa kuwalinda wanao.

Alisema askari hao watakuwa wakiishi katika kijiji hicho mpaka hapo itakapokuwa vinginevyo, lengo ni kuhakikisha wananchi wanaendelea na maisha bila kuathirika.

Katibu Tawala wa mkoa huo, Abdala Malela, aliwaeleza wananchi hao kuwa serikali imesikia kilio chao cha muda mrefu, hivyo wasiwe na wasiwasi kwa kuwa watapewa ulinzi na wataendelea na shughuli zao.

Hata hivyo, aliwataka kuacha tabia ya kuwachokoza wanyamapori kwani kijiji chao kipo karibu na pori la akiba la Rukwati.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Saloma Kaliki, aliishukuru serikali kwa kusikia kilio chao, na kuwaomba askari wa wanyamapori wawahakikishie ulinzi wame wanapokwenda kuvua samaki katika bwawa hilo kwa sababu wanalitegemea kwa ajili ya kupata kitoweo.

Ulinzi huo umewekwa zikiwa ni siku chache baada ya watu wawili kuuawa na wanyama hao walipokuwa wamekwenda katika bwawa hilo kuvua samaki kwaajili ya kitoweo.




Rais John Magufuli akisalimiana na Meneja Masoko wa Kampuni ya Vodacom Tanzania, Noel Mazoya, alipotembelea banda lao katika Maonyesho ya Nne ya Viwanda ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), yaliyofunguliwa rasmi jijini Dar es Salaam juzi. Vodacom ni miongoni mwa wadhamini wa maonyesho hayo. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Vodacom Tanzania, Jacqueline Materu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndege nyingine yaanguka

**Na Salome Kitomari**

SIKU nne baada ya ajali ya ndege kutokea wilayani Sikonge mkoani Tabora, ajali nyingine ya usafiri huo wa anga ilitokea jana wilayani Mafia mkoani Pwani.

Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) ilieleza kuwa chanzo cha ajali hiyo ya Mafia ni ndege kukosa nguvu ya kupaa kwenye Uwanja wa Ndege wa Mafia.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mtendaji wa TCAA, Hamza Johari, alisema ndege hiyo ya Shirika la Tropical Air yenye namba za usajili %H-NOW ilikuwa ikitokea Mafia kuelekea Dar es Salaam.

"Ilivyojaribu kupaa, ilishindwa kuinuka lakini baadaye iliinuka na ilivyokaribia mwisho wa eneo la kurukia (run way), iliinuka kidogo kama inapaa lakini haikwenda mbali ilirudi chini.

"Ilirudi chini na kuserereka kwenda kugonga uzio wa uwanja wa ndege, rubani alifungua mlango kwa haraka na abiria wote walitoka na baadaye ililipuka. Abiria wanne walipata majeraha madogo madogo na wanaendelea na matibabu Hospitali ya Mafia," alisema.

Joari aliongeza kuwa TCAA itaendelea kutoa taarifa kwa umma baada ya wataalamu wake kufanya uchunguzi wao kwa ndege zote mbili. "Tunafanya uchunguzi wa mara kwa mara, ndege zote zinazoruka angani ila bado ni vyombo vya moto na injini ni injini au mashine, huwezi kuwa na uhakika asilimia 100 kwa kuwa inaweza kuwa mpya na bado ikapata shida.

"Cha msingi ni kujua ilikuwa ni nini na nini kifanyike, lengo ni kuhakikisha kwamba ajali hazitokei na ndiyo maana tunaona inaweza kupita mwaka hazijatokea," alisema.

Jumapili iliyopita, majira ya asubuhi, katika Kijiji cha Mahompa, Kata ya Igigwa wilayani Sikonge, ilitokea ajali ya ndege yenye namba za usajili ZU-TAF aina ya Sling Aircraft na kusababisha vifo vya abiria, rubani na msaidizi wake.

# Serikali kuajiri 500 Uhamiaji

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema imebaini upungufu wa askari katika Idara ya Uhamiaji hasa maeneo ya viwanja vya ndege na tayari imetangaza nafasi za ajira ili kutatua changamoto hiyo.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo jana muda mfupi baada ya kumaliza ziara yake kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume visiwani Zanzibar.

Alisema katika bajeti ya mwaka huu wa fedha, serikali imepanga kuajiri jumla ya askari 500 ambao watakwenda kufanya kazi kwenye viwanja vya ndege mbalimbali nchini.

Alisema Idara ya Uhamiaji hivi karibuni ilitangaza nafasi za kazi 200 ambazo ni kati hizo 500 zinazotakiwa kutolewa kwa mwaka huu wa fedha.

"Tuna changamoto ya watendaji katika viwanja vyetu vya ndege, hii inatokana na uhakiki ambao serikali iliufanya na kubaini wapo watu walioajiriwa pasipo kufuata taratibu na wengine wakilipwa mishahara hewa, baada ya kuondolewa kumekuwa na upungufu.

"Hivi karibuni, Idara ya Uhamiaji ilitangaza nafasi za ajira na tu

INAENDELEA UK.8


SHUKRANI



IRMA

**Familia ya Dk.C.U.S. Makupa** inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Jumuiya nzima ya hapa Moshi na viunga vyake, bila kusahau na wale wote waliotoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi yetu, ndugu na marafiki , waliotufariji na kutuwezesha kufanikisha mazishi ya mke wangu mpendwa Irma , mama wa William, Andrew, Philip na bibi wa Malaika na Ursulla!

*Kwa vile haitakuwa rahisi kumshukuru kila mmoja, tunawaomba mkubali shukrani zetu, na Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki*

215363602

TAARIFA KWA WAZAZI NA MTU YEYOTE ANAYEHUSIKA.



Uongozi wa **St. Christina Girls Secondary School** iliyopo Tanga Mjini Inawataarifu wazazi/ walezi wote kuwa **ERNEST MKAMI** aliyekuwa Mwalimu wetu hayupo tena hapa St. Christina Girls Secondary School Tanga tangu **tarehe 15 July 2019.**

Shule haitahusika na haitatambua Huduma, yoyote Itakayofanywa na huyu Mwalimu.
Asante sana.

Tangazo hili limetolewa na
Mwenyekiti wa Bodi ya shule

115364802

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

**KUMB: PPR/19 - 08/1**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 7 AGOSTI 2019

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, Tarehe 7 Agosti 2019. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya D**ar es Salaam,** zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Julai 2019. Kwa mwezi Agosti 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 160/lita (sawa na asilimia 6.90), Shilingi 102/lita (sawa na asilimia 4.63) na Shilingi 81/lita (sawa na asilimia 3.75), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 159.09/lita (sawa na asilimia 7.27) na Shilingi 102.10/lita (sawa na asilimia 4.90) na Shilingi 81.01/lita (sawa na asilimia 3.96), mtawalia.

(b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga nazo zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Julai 2019. Kwa mwezi Agosti 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimepungua kwa Shilingi 134/lita (sawa na asilimia 5.76), Shilingi 103/lita (sawa na asilimia 4.61) na Shilingi 163/lita (sawa na asilimia 7.30), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 133.49/lita (sawa na asilimia 6.07), Shilingi 102.78/lita (sawa na asilimia 4.87) na Shilingi 162.36/lita (sawa na asilimia 7.71), mtawalia.

(c) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Mtwara zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Julai 2019. Kwa mwezi Agosti 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini** (Lindi, Mtwara na Ruvuma) zimepungua kwa Shilingi 105/lita (sawa na asilimia 4.50) na Shilingi 124/lita (sawa na asilimia 5.43), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 104.24/lita (sawa na asilimia 4.74) na Shilingi 123.57/lita (sawa na asilimia 5.72), mtawalia. Aidha, kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

(d) Kwa kiasi kikubwa, punguzo la bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara linatokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums) kama inavyoonekana katika Jedwali C.

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (formula) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.**

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

**JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA**

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | **Petroli (Shs/Lita)** | **Dizeli (Shs/Lita)** | **Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)** |
| **Dar es Salaam** | **2,153** | **2,107** | **2,086** |
| **Arusha** | **2,248** | **2,188** | **2,123** |
| Arumeru (Usa West) | 2,248 | 2,188 | 2,123 |
| Karatu | 2,266 | 2,206 | 2,141 |
| Longido | 2,259 | 2,199 | 2,134 |
| Monduli | 2,253 | 2,193 | 2,129 |
| Monduli-Makuyuni | 2,258 | 2,198 | 2,133 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,332 | 2,272 | 2,208 |
| **Pwani (Kibaha)** | **2,157** | **2,112** | **2,091** |
| Bagamoyo | 2,164 | 2,118 | 2,097 |
| Chalinze Junction | 2,167 | 2,121 | 2,100 |
| Chalinze (Msata) | 2,171 | 2,125 | 2,104 |
| Kibiti | 2,173 | 2,128 | 2,107 |
| Kisarawe | 2,160 | 2,114 | 2,093 |
| Mkuranga | 2,162 | 2,117 | 2,096 |
| Rufiji | 2,180 | 2,135 | 2,114 |
| **Dodoma** | **2,211** | **2,166** | **2,145** |
| Bahi | 2,219 | 2,173 | 2,152 |
| Chamwino | 2,207 | 2,161 | 2,140 |
| Chemba | 2,238 | 2,192 | 2,171 |
| Kondoa | 2,244 | 2,199 | 2,178 |
| Kongwa | 2,209 | 2,163 | 2,142 |
| Mpwapwa | 2,213 | 2,167 | 2,146 |
| Mtera (Makatopora) | 2,230 | 2,185 | 2,164 |
| **Geita** | **2,318** | **2,273** | **2,252** |
| Bukombe | 2,307 | 2,262 | 2,240 |
| Chato | 2,339 | 2,294 | 2,273 |
| Mbogwe | 2,356 | 2,311 | 2,290 |
| Nyang'hwale | 2,333 | 2,288 | 2,267 |
| **Iringa** | **2,217** | **2,171** | **2,150** |
| Ismani | 2,222 | 2,176 | 2,155 |
| Kilolo | 2,221 | 2,176 | 2,155 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,227 | 2,181 | 2,160 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,368** | **2,323** | **2,302** |
| Biharamulo | 2,343 | 2,297 | 2,276 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,385 | 2,339 | 2,318 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,390 | 2,345 | 2,324 |
| Muleba | 2,368 | 2,323 | 2,302 |
| Ngara | 2,356 | 2,311 | 2,289 |
| Misenyi | 2,377 | 2,331 | 2,310 |
| **Katavi (Mpanda)** | 2,361 | 2,315 | 2,294 |
| Mlele (Inyonga) | 2,343 | 2,297 | 2,276 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,353 | 2,307 | 2,286 |
| **Kigoma** | **2,384** | **2,339** | **2,318** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,396 | 2,351 | 2,330 |
| Buhigwe | 2,373 | 2,328 | 2,307 |
| Kakonko | 2,341 | 2,296 | 2,275 |
| Kasulu | 2,370 | 2,325 | 2,304 |
| Kibondo | 2,348 | 2,303 | 2,282 |

215364601

# TANGAZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **2,237** | **2,177** | **2,113** |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,241 | 2,181 | 2,116 |
| Mwanga | 2,231 | 2,170 | 2,106 |
| Rombo (Mkuu) | 2,254 | 2,194 | 2,129 |
| Same | 2,224 | 2,164 | 2,099 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,244 | 2,184 | 2,119 |
| **Lindi** | **2,232** | **2,174** | **2,145** |
| Lindi-Mtama | 2,236 | 2,179 | 2,163 |
| Kilwa Masoko | 2,255 | 2,198 | 2,120 |
| Liwale | 2,267 | 2,210 | 2,166 |
| Nachingwea | 2,251 | 2,194 | 2,174 |
| Ruangwa | 2,258 | 2,201 | 2,176 |
| **Manyara (Babati)** | **2,282** | **2,222** | **2,157** |
| Hanang (Katesh) | 2,292 | 2,232 | 2,168 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,297 | 2,237 | 2,172 |
| Mbulu | 2,295 | 2,234 | 2,170 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,314 | 2,254 | 2,189 |
| **Mara (Musoma)** | **2,331** | **2,286** | **2,265** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,372 | 2,327 | 2,305 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,340 | 2,295 | 2,274 |
| Rorya (Shirati) | 2,375 | 2,329 | 2,308 |
| Bunda | 2,322 | 2,277 | 2,256 |
| Bunda (Kisorya) | 2,332 | 2,287 | 2,265 |
| Butiama | 2,328 | 2,283 | 2,262 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,377 | 2,331 | 2,310 |
| Tarime | 2,342 | 2,297 | 2,276 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,347 | 2,301 | 2,280 |
| **Mbeya** | **2,260** | **2,214** | **2,193** |
| Chunya | 2,269 | 2,224 | 2,203 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,284 | 2,238 | 2,217 |
| Kyela | 2,276 | 2,230 | 2,209 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,244 | 2,198 | 2,177 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,269 | 2,223 | 2,202 |
| **Morogoro** | **2,178** | **2,132** | **2,111** |
| Mikumi | 2,193 | 2,148 | 2,127 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,216 | 2,170 | 2,149 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,238 | 2,192 | 2,171 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,227 | 2,182 | 2,161 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,226 | 2,181 | 2,160 |
| Malinyi | 2,236 | 2,191 | 2,170 |
| Kilosa | 2,196 | 2,151 | 2,130 |
| Gairo | 2,196 | 2,151 | 2,130 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,188 | 2,143 | 2,122 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 2,178 | 2,132 | 2,111 |
| Turiani | 2,203 | 2,157 | 2,136 |
| **Mtwara** | **2,218** | **2,161** | **2,159** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,254 | 2,197 | 2,207 |
| Masasi | 2,234 | 2,177 | 2,184 |
| Newala | 2,239 | 2,182 | 2,191 |
| Tandahimba | 2,232 | 2,175 | 2,184 |
| Nanyamba | 2,232 | 2,175 | 2,184 |
| **Mwanza** | **2,303** | **2,257** | **2,236** |
| Kwimba | 2,321 | 2,275 | 2,254 |
| Magu | 2,311 | 2,265 | 2,244 |
| Misungwi | 2,297 | 2,252 | 2,231 |
| Sengerema | 2,335 | 2,290 | 2,269 |
| Ukerewe | 2,362 | 2,317 | 2,296 |
| **Njombe** | **2,245** | **2,200** | **2,179** |
| Njombe (Kidegembye) | 2,266 | 2,220 | 2,199 |
| Ludewa | 2,283 | 2,238 | 2,216 |
| Makambako | 2,237 | 2,192 | 2,171 |
| Makete | 2,276 | 2,230 | 2,209 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,243 | 2,197 | 2,176 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,326** | **2,280** | **2,259** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,326 | 2,280 | 2,259 |
| Kalambo (Matai) | 2,333 | 2,287 | 2,266 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,339 | 2,294 | 2,273 |
| **Ruvuma (Songea)** | **2,304** | **2,246** | **2,210** |
| Mbinga | 2,316 | 2,259 | 2,243 |
| Namtumbo | 2,295 | 2,237 | 2,239 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,342 | 2,284 | 2,253 |
| Tunduru | 2,269 | 2,211 | 2,269 |
| **Shinyanga** | **2,282** | **2,236** | **2,215** |
| Kahama | 2,295 | 2,250 | 2,229 |
| Kishapu | 2,310 | 2,265 | 2,244 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,313 | 2,267 | 2,246 |
| Simiyu (Bariadi) | 2,323 | 2,278 | 2,257 |
| Busega (Nyashimo) | 2,316 | 2,271 | 2,250 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,326 | 2,281 | 2,260 |
| Maswa | 2,315 | 2,269 | 2,248 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,322 | 2,276 | 2,255 |
| **Singida** | **2,243** | **2,198** | **2,177** |
| Iramba | 2,256 | 2,210 | 2,189 |
| Manyoni | 2,228 | 2,182 | 2,161 |
| Ikungi | 2,239 | 2,193 | 2,172 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,268 | 2,222 | 2,201 |
| **Songwe (Vwawa)** | **2,269** | **2,224** | **2,202** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,276 | 2,230 | 2,209 |
| Ileje | 2,273 | 2,227 | 2,206 |
| Momba (Chitete) | 2,278 | 2,233 | 2,212 |
| Tunduma | 2,273 | 2,228 | 2,207 |
| **Tabora** | **2,307** | **2,261** | **2,240** |
| Igunga | 2,261 | 2,215 | 2,194 |
| Kaliua | 2,326 | 2,280 | 2,259 |
| Ulyankulu | 2,320 | 2,275 | 2,253 |
| Nzega | 2,271 | 2,226 | 2,205 |
| Sikonge | 2,319 | 2,273 | 2,252 |
| Urambo | 2,320 | 2,275 | 2,253 |
| Uyui | 2,308 | 2,262 | 2,241 |
| **Tanga** | **2,191** | **2,131** | **2,066** |
| Handeni | 2,212 | 2,152 | 2,087 |
| Kilindi | 2,227 | 2,167 | 2,102 |
| Korogwe | 2,203 | 2,143 | 2,079 |
| Lushoto | 2,213 | 2,152 | 2,088 |
| Mkinga (Maramba) | 2,198 | 2,138 | 2,073 |
| Muheza | 2,196 | 2,136 | 2,071 |
| Pangani | 2,198 | 2,138 | 2,073 |

**JEDWALI B: BEI ZA JUMLA**

| Bei za Jumla - DSM | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| Bei Kikomo | 2,028.93 | 1,983.13 | 1,962.75 |

| Bei za Jumla - TANGA | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| Bei Kikomo | 2,067.32 | 2,006.92 | 1,943.21 |

| Bei za Jumla - MTWARA | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| Bei Kikomo | 2,094.05 | 2,036.50 | ----- |

**JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

**BANDARI YA DAR ES SALAAM**

| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| **Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia** | Punguzo la Dola 61.647/Tani | Punguzo la Dola 63.805/Tani | Punguzo la Dola 63.439/Tani |
| **Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)** | Punguzo la Dola 24.122/Tani | Ongezeko la Dola 0.215/Tani | Ongezeko la Dola 5.550/Tani |

**BANDARI YA TANGA**

| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| **Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia** | Punguzo la Dola 61.647/Tani | Punguzo la Dola 45.155/Tani | Punguzo la Dola 76.635/Tani |
| **Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)** | Ongezeko la Dola 5.740/Tani | Punguzo la Dola 8.450/Tani | Punguzo la Dola 10.500/Tani |

**BANDARI YA MTWARA**

| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| **Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia** | Punguzo la Dola 61.647/Tani | Punguzo la Dola 50.200/Tani | n/a |
| **Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)** | Ongezeko la Dola 5.740/Tani | Punguzo la Dola 18.140/Tani | n/a |

**JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

| | Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|
| **Mafuta yalipokelewa mwezi wa:** | **DSM** | Julai 2019 | Julai 2019 | Julai 2019 |
| | **Tanga** | Julai 2019 | Julai 2019 | Julai 2019 |
| | **Mtwara** | Julai 2019 | Julai 2019 | n/a |
| **Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:** | **DSM** | Juni 2019 | Juni 2019 | Juni 2019 |
| | **Tanga** | Juni 2019 | Juni 2019 | Juni 2019 |
| | **Mtwara** | Juni 2019 | Juni 2019 | ---- |
| **Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:** | **DSM** | Mei 2019 | Mei 2019 | Mei 2019 |
| | **Tanga** | Mei 2019 | Mei 2019 | Novemba 2018 |
| | **Mtwara** | Mei 2019 | Aprili 2019 | ---- |

**Nzinyangwa E. Mchany**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA!**

215364601

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ndugai amesema kweli uzazi kuzingatia uchumi

**SUALA** la uzazi wa mpango ni ajenda ya dunia, sababu mojawapo ikiwa ni kupunguza mzigo wa umaskini na makali ya maisha kwa familia nyingi.

Ni kweli kwamba vitabu vitakatifu vinapingana na mpango huo, kwamba kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha maagizo ya Mungu.

Uzazi wa mpango umekuwa ukisisitizwa na mataifa yaliyoendelea, ingawa hatukubaliani na approach (njia) zote wanazozitumia kwa sababu baadhi zinakiuka maadili, mila, desturi, miiko na utamaduni wetu kama taifa.

Hata hivyo, kwa kuzingatia ukweli na hali halisi ya uchumi na ugumu wa maisha, tunapaswa kukubali kuzingatia uzazi wa mpango ili familia zipunguziwe nzigo wa changamoto hizo. Ikumbukwe kuwa ongezeko la idadi ya watu, inasababisha kupungua kwa rasilimali kunakosababishwa na mahitaji kuongezeka.

Kwa mfano, zamani huduma za msingi za jamii kama elimu, afya, maji, chakula zilikuwa zinapatikana kwa urahisi kutokana na serikali kutoa ruzuku, hivyo kuzifanya zitolewe bila malipo.

Kutokana na mazingira ya wakati ule kabla ya serikali kupungukiwa na uwezo huo kutokana na sababu mbalimbali, kubwa yakiwa masharti ya wakubwa wa dunia, lilikuwa jambo la kawaida kwa familia kuzaa idadi yoyote ya watoto bila kuwapo athari.

Hata hivyo, kwa sasa mambo hayo hayawezekani tena kutokana na kila mtu kuubeba msalaba wake mwenyewe, kama mmoja wa wanasiasa wastaafu nchini, mwenye taaluma ya uchumi alivyowahi kueleza miaka kadhaa iliyopita likiwa ni angalizo lake. Alichokisema mwanasiasa wakati ule hakikuwafurahisha wengi, lakini alikuwa anaona mbele, na ukweli huo unathibitika sasa.

Juzi, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitoa kauli ambayo ni changamoto kwa Watanzania na inapaswa kuchukuliwa kwa uzito wake kuhusiana na suala hilo, akiwataka Watanzania kuzaa idadi ya watoto kulingana na uchumi wa familia.

Alitoa rai hiyo jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa siku mbili wa wabunge wa nchi za Afrika na Asia, waliokutana kujadili ukuaji wa maendeleo na idadi ya watu.

Alisema taifa linapaswa kuwa na idadi ya watu endelevu ambao wataishi maisha marefu na wenye uchumi mzuri.

Alieleza kuwa Jambo la muhimu ni kuwa idadi ya watoto ilingane na uchumi wa familia au kaya na taifa, na kuwa kuhusu idadi ya watoto mtu azae wangapi, inategemea na uchumi wa familia husika.

Alifafanua zaidi kuwa suala la uchumi haliwezi kuangaliwa kitaifa, bali linatakiwa kuangalia katika ngazi ya familia ndipo matokeo ya kitaifa yataonekana.

Alisema Bunge litaendelea na jukumu lake la kuishauri serikali kuhusu sera mbalimbali zitakazowezesha watu kuishi miaka mingi na kuwa nchi yenye uchumi imara.

Alichokisema Ndugai ni kwamba familia zijenge utamaduni wa kuzaa watoto kwa kuzingatia uwezo wao kiuchumi ili kumudu mahitaji kama ya kuwasomesha, chakula, huduma za afya na mengineyo bila kutarajia msaada wa mtu mwingine au serikali.

Tunaamini kabisa kwamba kama jamii yetu itabadilika na itaupokea ushauri huu na kuufuata, bila shaka familia zitapunguza kama si kumaliza kabisa utegemezi, ambao ni kichocheo kikubwa cha umaskini.

Itakuwa vizuri ikiwa wanasiasa wengine wataendelea kutoa elimu hii kwa kuwa wana ushawishi mkubwa katika jamii yetu, na wanasilikilizwa na kuaminiwa na wananchi wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Raphael Kibiriti

## Muungwana Lazima Nilonge

# Operesheni safisha mitaro ifanyike nchi nzima kudhibiti magonjwa

**KUNA** mengi ambayo serikali ya awamu ya tano inazidi kujijengea uhalali kwenye suala zima la utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazokabili wananchi katika suala zima la kujenga ustawi na maendeleo ya jamii ya Kitanzania.

Ninaweza kuzungumzia maeneo mengi kuanzia kwenye suala zima la kupambana dhidi ya rushwa na ufisadi, watumishi hewa, uhalifu hususani unyang'anyi, ujambazi na ujangili.

Lakini hata katika kuboresha hali ya miundombinu ya barabara, vituo vya afya, ukarabati na ujenzi wa madarasa, maabara, maktaba, utoaji wa elimu bure kwa kutaja baadhi ya mambo.

Muungwana anaona haya yote ni katika ile dhima ya kutekeleza majukumu na wajibu wa serikali hii kwa wananchi wake.

Na hiyo ni kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo rais na timu yake, waliinadi wakati wa kampeni za kutafuta ridhaa ya kuongoza taifa hili.

Kama nilivyosema hapo juu kuna mengi ambayo yametekelezwa na serikali hii, lakini kwa makusudi maalumu Muungwana amevutiwa zaidi kuzungumzia operesheni mbili ambazo kwa mtazamo wake zimeiongezea alama serikali ya awamu ya tano.

Zimeiongezea alama mbele ya macho ya wananchi na hasa wenye mapenzi mema kwa ustawi wa taifa na raia wake, lakini pia hata katika suala la usafi wa mazingira na uhai wa viumbe vinavyoyategemea mazingira hayo.

Operesheni ya kwanza anayoirejea Muungwana ni ile iliyochukuliwa na serikali mwaka 2017 inayofahamika hadi leo kama operesheni 'piga marufuku viroba' vilivyokuwa maarufu katika maeneo mbalimbali nchini.

Kupitia kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, serikali ilipiga marufuku uzalishaji, uuzaji, uingizaji na matumizi ya pombe inayofungwa kwenye pakiti za plastiki kwa jina la viroba kuanzia Machi Mosi, mwaka 2017.

Aidha, ikaweka wazi kwamba ambaye angebainika kutumia angewajibishwa kwa kulipa faini, kufungwa jela au vyote kwa pamoja.

Ilichukua hatua hiyo kwa nia nzuri ya kulinda afya ya Watanzania, hususani vijana ambao ndio nguvukazi ya taifa hili wanaotengeneza sehemu kubwa ya idadi ya Watanzania takribani milioni 55 kwa hivi sasa.

Kwa wanaokumbuka hali ilipokuwa imefikia wakati huo kiasi kwamba viroba vilienea kila kona hata kwa watoto wa shule za msingi ambao nao walianza kuvitumia kwa sababu ya urahisi wake wa kuvibeba, kwani iliwezekana hata kuviweka mfukoni na kutembea navyo.

Madhara ya viroba yalikuwa mabaya sana kwa afya na maendeleo ya Watanzania kwani mbali na ajali za barabarani zilizotokana na uendeshaji wa kizembe hasa kwa madereva wa bodaboda, pia yaliharibu mazingira kutokana na kuzagaa kwa vifungashio hivyo.

Operesheni ya pili ambayo imeendelea kuipa alama serikali hii ni ile iliyopiga marufuku uzalishaji, uingizaji, usafirishaji nje ya nchi, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko aina ya plastiki maarufu kama 'Rambo' iliyokuwa ikitumika kubebea bidhaa kuanzia Juni Mosi.

Katika operesheni zote mbili, serikali ilitoa maelekezo na hatua madhubuti za kuwachukulia wote ambao wangekaidi maelekezo yake.

Kama nilivyosema hapo juu, kufanikiwa kwa operesheni hizo kunaonyesha kwamba serikali hii inapoelekeza marufuku dhidi ya dosari fulani iliyo na madhara kwa watu wake, wananchi wanaelewa na kutekeleza.

Wanafanya hivyo kwa sababu wanajua haina simile katika kuchukua hatua.

Wakati Muungwana akipongeza umadhubuti wa serikali katika kusimamia masuala yenye tija kwa wananchi, anatoa wito operesheni kama hiyo sasa ielekezwe katika usafi wa mitaro kwenye majiji na miji, hasa jiji la Dar es Salaam, lenye hali mbaya katika eneo hilo.

Muungwana ana imani kwamba serikali ikielekeza nguvu kwenye eneo hili la mitaro katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, suala la mlipuko wa magonjwa kama kipundupindu na homa ya dengue yatakwisha.

HABARI KITAIFA



Ofisa Mwandamizi wa Mifumo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Godfrey Malunda (kulia), akiwaelekeza wanachama wa mfuko huo, kuhusu michango yao walipotembelea katika maonyesho ya Nanenane kitaifa, Viwanja vya Nyakabindi, mkoani Simiyu jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Polisi yaua watu watatu wakidaiwa majambazi

**Na Timothy Itembe,**
TARIME

JESHI la Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, limeua watu watatu wanaodaiwa kuwa majambazi kwa kujihusisha na vitendo vya uhalifu, yakiwamo mauaji na unyang'anyi wa kutumia silaha za moto.

Hayo yalibainishwa na Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Henry Mwaibambe, na kueleza kuwa juzi saa nane usiku katika Kitongoji cha Makerero kijiji cha Nyamwaga Kata ya Nyamwaga askari wa kikosi cha kupambana na uhalifu waliwaua watu hao watatu.

Kamanda Mwaibambe alisema watu hao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya uhalifu wa unyang'anyi wa kutumia silaha pamoja na mauaji.

Kamanda huyo aliongeza kuwa mmoja wao alitambuliwa kwa jina la Emanuel Marwa Kenara (35) mkazi wa kijiji cha Nyamwigura, huku wengine majina yao hayajatambuliwa ambao wanakadiriwa kuwa na umri wa miaka kati ya 30 hadi 45, na wote ni wanaume. Mwaibambe aliongeza kuwa baada ya askari kumkamata Kenara, Agosti 3, mwaka huu alikuwa tayari kuwaonyesha askari polisi mahali alipoficha silaha anayoitumia kufanyia uhalifu.

Alisema askari na mtu huyo wakiwa wanaelekea katika eneo la tukio ambapo silaha hiyo ilikuwa imefichwa ndipo ghafla majambazi wenzake wawili walianza kuwashambulia askari polisi kwa risasi, ambapo polisi walijibu mapigo na kuwapiga risasi majambazi hao. Mwaibambe aliongeza kuwa Kenara naye alipata mwanya na kutaka kukimbia ndipo walipigwa risasi na polisi na kujeruhiwa sehemu mbalimbali za miili yao.

Mwaibambe alisema waliwachukua kuwapeleka hospitali kwa matibabu, lakini kwa bahati mbaya wakafia njiani kabla hawajafika hospitali.

Mwaibambe aliongeza kuwa kwenye eneo la tukio yamepatikana maganda manne ya risasi ya AK-47 silaha iliyofutwa namba ikiwa na risasi tano kwenye magazine na simu mbili za mkononi, na kwamba miili imehifadhiwa katika hospitali ya wilaya inayomilikiwa na Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa uchunguzi wa madaktari.

# Familia ilivyonusurika kuuawa na wanakijiji

**Na Lilian Lugakingira,**
KYERWA

KUNDI la wananchi ambao idadi yao haijafahamika, wamevamia nyumbani kwa Tryphone Jeremiah (48), wakabomoa nyumba, kufyeka mashamba yake ya migomba, miti na mibuni na kuua mifugo ikiwamo mbuzi kutokana na mgogoro wa ardhi kati ya Tryphone na baadhi ya wanakijiji wa Kishanda "B" Kata ya Kibale Wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera, unaodaiwa kudumu kwa muda mrefu.

Wakizungumza na waandishi wa habari baadhi ya mashuhuda wakiwamo waliokuwa wakichunga mbuzi, walisema walipoona kundi la wananchi wakielekea katika mashamba hayo walilazimika kukimbia kujificha ili kunusuru maisha yao, huku taarifa kutoka katika eneo hilo zikidai kuharibiwa kwa mali za baba huyo kumetokana na mwenyekiti wa kijiji hicho kukamatwa na kuwekwa ndani, akituhumiwa kuhusika na mgogoro huo wa ardhi.

Jeremiah alisema walikuwa na mbuzi zaidi ya 100, lakini hadi sasa wamesalia 39 tu na kuwa baadhi wameuawa na wengine hawafahamiki walipo, huku akionyesha hofu ya usalama wake na familia, hivyo kuiomba serikali kuingilia kati mgogoro huo na kuupatia ufumbuzi, ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kutokea.

Alisema kuwa wakati wananchi hao wakiharibu mali hizo Jumapili iliyopita mchana, yeye alikuwa kanisani, na kuwa mgogoro wa ardhi kati yake na baadhi ya wananchi uliosababisha unyama huo ulianza tangu mwaka 2007.

Mtoto wa Tryphone, Ezra Tryphone, alisema wakati wanakijiji hao wanatekeleza unyama huo kwa wachungaji wa mifugo pamoja na mdogo wake, Erneus Tryphone, walikimbia na kujificha nao wakihofia kushambuliwa, na kuwa mashamba yaliyofekwa yalikuwa na ukubwa wa hekta 10.5.

Alisema mashamba hayo yalikuwa ni mali ya watu watatu, baba yao alikuwa na migomba na kahawa hekta tatu, yeye (Ezra) alikuwa na hekta 1.5 na mdogo wake (Erneus) hekta moja, na kuwa shamba la miti iliyopandwa miaka sita iliyopita lilikuwa na ukubwa wa hekta 6.

Naye mchungaji wa mbuzi hao, Fatius Mwesiga, alisema baada ya wanakijiji hao kuvamia walijificha kwa kuhofia usalama wao, huku akidai kuwatambua baadhi yao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kishanda, Medius Atanas, alisema mgogoro huo ulitokana na mlalamikaji kujimilikisha ardhi kubwa, na pia mifugo yake ilikuwa kero kwa wanakijiji.

"Baada ya mlalamikaji kujimilikisha eneo kubwa la ardhi, uliibuka mgogoro baina yake na baadhi ya wanakijiji," alisema mwenyekiti huyo.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Ahmed Msengi, alithibisha kutokea kwa tukio hilo na kusema mashamba yaliyoharibiwa ni ya migomba, mibuni na miti, na kuwa pia wananchi hao wamebomoa nyumba ya mlalamikaji pamoja na kuwaua baadhi ya mbuzi wake na wengine kujeruhiwa.

Alisema kwa mujibu wa mlalamikaji, alikuwa na mbuzi zaidi ya 100, hivyo kati ya hao waliobaki hai wanaonekana ni 39 na mbuzi 57 hawajulikani walipo.

Msengi alisema chanzo cha mgogoro huo ni mlalamikaji kumiliki ardhi kubwa, mgogoro ambao ulishafikia mahakamani, na kuwa mpaka sasa hakuna mtu aliyekamatwa kuhusiana na tukio hilo, baada ya watuhumiwa kukimbia.

# Taboa yalalamika kutoridhishwa ukusanyaji maoni

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi (Taboa), kimesema hakijaridhishwa na utaratibu wa kuharakisha ukusanyaji wa maoni ya wadau wa usafirishaji nchini bila kuwashirikisha na maoni yao kutozingatiwa.

Kauli hiyo imekuja siku chache baada ya kikao cha wamiliki wa vyombo vya usafiri na madereva kususia mkutano wa kupokea maoni ya wadau katika rasimu ya kanuni za sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), wakipinga lugha iliyotumika na muda waliopewa kabla ya mkutano huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Taboa, Ene Mrutu, alisema nyaraka waliyopewa Ijumaa iliyopita ina kurasa 115 na imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, huku wakiambiwa kuwa sheria mama imeshapita na hakuna kitakachobadilika.

Alisema imekuwa kawaida kwa wadau kutoa maoni yao tangu ilivyokuwa Sumatra na kupuuzwa na kwamba hivi karibuni walitoa maoni kwenye sheria ya usafirishaji jijini Dodoma, lakini ilipitishwa bila kuzingatia hata jambo moja la kwao.

"Tumewaambia tunahitaji tupewe muda hakuna sababu ya haraka, tumeomba siku 14 na iwe kwa lugha ya Kiswahili na ndiyo tutatoa maoni yetu," alisema na kuongeza:

"Tumegundua kuna sheria za ovyo na kilichotukera kuna watu wa serikali walitumia kauli za kejeli kuwa sheria mama imeshapita ambayo walitoa maoni Dodoma na hayakuzingatiwa."

Kwa mujibu wa Mrutu, maoni yao ilikuwa ni kupunguza faini ambayo ni kati ya Sh. 500,000 hadi Sh. milioni mbili kwa gari inayosababisha ajali na kwamba waliomba ziondolewe au kupunguzwa kwa kuwa wamejitahidi kupunguza ajali kwa kiasi kikubwa.

"Hakuna sababu ya kutuwekea kanuni ngumu kiasi hiki wakati tumeshirikiana na mamlaka husika tumepunguza ajali za barabarani kwa kiasi kikubwa," alisema.

Vile vile, alisema jambo jingine wasilolitaka kwenye kanuni hizo ni ushuru wa 'service leave' wa asilimia 0.3 ya mapato ghafi kabla ya kodi.

"Tulisema yasiwapo bali iachiwe Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na siyo Latra, na sheria inaingiliana na mambo ya ndani sheria ya mwendo

INAENDELEA UK. 8

# Waonywa matumizi ya zebaki kienyeji

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

SERIKALI imeandaa mpango wa taifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu ulioainisha fursa zitakazowezesha wachimbaji hao kuendelea na shughuli za uzalishaji wa dhahabu bila kuathiri mazingira nchini.

Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, aliyasema hayo, jana baada ya kufanya ziara ya kikazi kukagua shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Wilaya ya Tarime mkoani Mara hususan maeneo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu.

Alisema ofisi yake inaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu kuhusu madhara ya zebaki kwa afya ya binadamu na mazingira na kuwataka kuchenjua dhahabu kupitia vituo mahiri saba vya mafunzo na uchenjuaji wa dhahabu vinavyojengwa katika mikoa ya Simiyu, Mara, Kagera, Katavi, Mbeya, Ruvuma, Tanga na Geita.

Alisema serikali imeona umuhimu wa kuungana na jumuiya ya kimataifa ili kukabiliana na madhara yatokanayo na matumizi ya zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu kwa wachimbaji wadogo na kuwaelimisha kutumia njia salama na rafiki wa mazingira.

Akiwa katika Kata ya Kenyamanyori, Mtaa wa Kebaga, Sima alipata fursa ya kujionea shughuli za uchenjuaji wa dhahabu kwa kutumia zebaki na kueleza kuwa uchenjuaji huo una athari kwa afya za binadamu na mazingira kwa ujumla.

Alisema zebaki inasababisha magonjwa ya ngozi, moyo, figo na kuharibu mfumo wa neva za fahamu ikiwa watumiaji hawatazingatia miongozo iliopo.

"Sisi kama serikali lengo letu kubwa ni kuhakikisha tunawaelimisha wananchi wetu kwa kuwaambia madhara ya matumizi ya zebaki na kuwashawishi kutotumia zebaki kwa shughuli za uchenjuaji dhahabu," Sima alisema.

Alizitaja fursa zilizopo katika mpango wa kitaifa kuwa ni amoja na upatikanaji wa masoko ya dhahabu kupitia masoko ya madini ya mikoa yanayojengwa katika mikoa yote nchini.

Alisema fursa nyingine ni upatikanaji wa mikopo midogo na ya kati kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu na kuwezesha vikundi vya kinamama wanaojishughulisha na uchimbaji wa dhahabu kwa kutoa mafunzo kuhusu uchenjuaji salama na rafiki kwa mazingira.

# Tanzania yauza nje samaki wa mabilioni

**Na Said Hamdani, LINDI**

TANZANIA imeuza nje tani milioni 38 za samaki wa chakula na mazao ya baharini, hivyo kuiingizia jumla ya Sh. bilioni 491.0 katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Naibu Waziri wa Mifugo na Mifugo, Abdallah Ulega, ndiye aliyebainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari, viwanja vya Maonesho ya Wakulima Nanenane, eneo la Ngongo Manispaa ya Lindi.

Amesema mauzo hayo yamefanyika kipindi cha mwaka wa 2018/2019, huku samaki aina ya chakula wakiongoza kwa kuwa na idadi kubwa.

Ulega alisema kufuatia mauzo hayo, serikali imeweza kujikusanyia mrabaha kiasi cha Sh. bilioni 15.8.

Alisema kufuatia hali hiyo, hakuna sababu wananchi kuendelea kuwa maskini, wakati rasilimali za kujiongezea kiuchumi zipo, hivyo kinachotakiwa ni kujituma ikiwamo kutumia mazao yanayotokana na bahari ili waondokane na umaskini.

"Kinachotakiwa ni watu wenyewe kuhakikisha wanajituma katika kufanya kazi, fursa za kuondokana na umaskini zipo," alisema Ulega.




# Bil. 25/- kujenga daraja Mto Kagera

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh. bilioni 25 za kugharamia ujenzi wa daraja la Mto Kagera linalounganisha Wilaya za Misenyi na Karagwe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), Geoffrey Mwambe, aliyasema hayo wakati akikagua maendeleo ya uwekezaji mkoani Kagera.

Mwambe alisema kiasi hicho cha fedha kilichotolewa na Serikali kitasaidia kuongeza ufanisi wa uwekezaji kwenye kiwanda hicho, na kukiunganisha na Wilaya ya Karagwe.

Alisema lengo la ujenzi huo ni kuimarisha uwekezaji kwenye kiwanda hicho kwenye eneo la Kitengule na upanuzi wa mashamba mapya ya miwa.

"Daraja hili litagharimu zaidi ya Sh. bilioni tisa. Serikali imetoa Sh. bilioni tano ikiwa ni mpango mkakati wake wa kuimarisha mazingira ya iwekezaji na kurahisisha miundombinu," alisema.

Alisema wenye kiwanda hicho walitoa ombi kwa Rais John Magufuli Agosti mwaka jana wakiomba daraja hilo ili liunganishe mashamba hayo na wananchi.

"Kwa sasa wananchi wanazunguka umbali wa zaidi ya kilomita 140 kwenda na kurudi katika kufuata huduma muhimu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema kiwanda hicho kimekuwa na tija ya kiuchumi mkoani kwake kutokana na kutoa ajira zaidi ya 6,000 kwa vijana.

Mwenyekiti wa Bodi ya kampuni ya kiwanda hicho cha sukari, Seif Ally, alisema kuwa mwezi Novemba mwaka 2017, Rais Magufuli alitembelea mradi wao mkubwa wa uwekezaji kwenye kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari na kutoa maelekezo ya kuongeza uzalishaji.

# Taboa yalalamika

INATOKA UK. 7

wa dereva anakwenda shule anakaguliwa na bado Latra naye wanataka wamkague sasa mwingiliano umetukera," alisema Mrutu.

Alisema pia kuna tozo nyingi kwenye kanuni ikiwamo ya kuthibitisha dereva ya Sh. 50,000, Sh. 20,000 na Sh. 5,000, jambo linalotufanya tujiulize maswali mengi.

"Kwanini mtu kama amesoma shule ya udereva akaenda kukaguliwa akafaulu, wao tena wanataka kumgakua kwasababu gani?" Alihoji.

"Kumpa Latra madaraka yote tunaogopa kwa kuwa siyo 'mtu' wa weledi wa kufanyakazi na weledi yuko kwenye amri zaidi, hana kumuita na kumweleza kosa au kuonya, wanatumia ubabe kwa kutumia vijana wao. Kuwapa madaraka makubwa ni kuua sekta ya usafirishaji nchini," alibainisha.

Alipoulizwa hatua za siku za usoni alisema: "Safari hii tumesema tutatoa maoni kama hatutasikilizwa kazi ya usafirishaji itakuwa ngumu sana tutashindwa."

Mrutu alisema mara nyingi wanatoa maoni, lakini yakienda Latra au Sumatra yakachukuliwa hata mawili au matatu ni bahati sana, na kwamba wanaonekana kama wanakwenda kupoteza muda wao na hakuna anayejali.

"Tunayemtolea maoni ni yeye (Latra) ambaye ametengeneza kanuni, tuna wasiwasi sana kama maoni yetu hayafiki sehemu husika, siku zote vikao vya maoni wanakuja wao wenyewe juzi alikuwa aje Katibu Mkuu wa Uchukuzi hakuja, akaja Mkurugenzi wa Uchukuzi na bado hawakuwa na kauli rafiki kwetu," alifafanua.

Katibu huyo alisema iwapo wataendelea kupuuzwa hivyo itafikia wakati watashindwa kuendelea na shughuli ya usafirishaji.

Pia, kikao hicho juzi kiliendelea kwa baadhi ya wajumbe kutoa maoni yao, huku Mkurugenzi wa Usafirishaji kutoka wizarani, Aron Kisaka, akisema wameyapokea maoni ya wadau ya suala la muda na lugha ya kanuni na yatafanyiwa kazi.

# Serikali kuajiri 500 Uhamiaji

INATOKA UK. 3

tahakikisha viwanja vyote vya ndege nchini vinapata watendaji wapya," Masauni alisema.

Aliwataka wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama katika uwanja huo kufanya kazi kwa ushirikiano ili yale yaliyotokea viwanja wa ndege vya Mwanza na Kilimanjaro, yasitokee tena.

"Kama mtakumbuka yaliyotokea Uwanja wa Ndege wa Mwanza na kule Kilimanjaro, ni aibu kwa taifa na vyombo vilivyopo vya ulinzi na usalama, madini na dhahabu kukamatwa Kenya wakati vyombo hivi vilikuwapo," alisema.

Masauni aliongeza kuwa Rais John Magufuli aliwanyooshea kidole polisi kutokana na tukio hilo la aibu.

## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (katikati), akikata utepe kuashiria kuzindua mradi wa usambazaji wa umeme katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa miji, katika Kijiji cha Mwanabwito, wilayani Kibaha Vijijini, mkoa wa Pwani jana. Uzinduzi huo ulishuhudiwa na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya REA, viongozi wa Wizara ya Nishati na taasisi zilizo chini yake ikiwamo REA na Tanesco. **PICHA: WN**

# Mikakati yawekwa kudhibiti mlipuko wa ebola Kigoma

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

MKOA wa Kigoma umetajwa kuwa ni moja ya mikoa iliyoko hatarini wakazi wake kupata mambukizi ya virusi vya ugonjwa wa ebola.

Hali hiyo inatokana na kupakana na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) inayokabiliwa na ongezeko la watu 2,673 walioathiriwa na ugonjwa huo kuanzia Agasti, 2018, huku watu 1,823 wakipoteza maisha tangu Julai 31, mwaka huu, sawa na asilimia 67% ya watu walioathiriwa na ugonjwa huo.

Kutokana na mwingiliano wa shughuli za kibiashara na undugu kwa baadhi ya wakazi wa mkoa wa Kigoma, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, serikali imeratibu zoezi la aina ya mazoezi, mafunzo, ufuatiliaji na tathmini ya uwezo wa utoaji majawabu endapo ugonjwa utaingia mkoani hapa.

Lengo ni kukabiliana na uwezekano wa mlipuko wa ugonjwa huo.

Mkurugenzi Msaidizi Utafiti na Mipango Utawala na Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Bashiru Taratibu, alieleza kuwa ofisi hiyo inasimamia kitengo cha maafa, ambapo zoezi la utayari linafanywa kwa mfumo wa afya awamu ya kwanza ambao unatekelezwa katika mikoa ambayo kuna uwezekano wa kupata mambukizi ikiwamo Kagera, Kigoma na Mwanza.

"Wadau mbalimbali wa afya kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Wizara ya Mifugo na wadau mtambuka tudhibiti kabla ya kuingia kwetu," alisema na kuongeza kuwa lengo la serikali ni kudhibiti maeneo ya mipakani. "Sasa wataalamu wamepewa mafunzo, tunataka tuone matokeo ya mafunzo, ili kubaini mapungufu ya waliopata mafunzo kwa kuyaboresha, Kigoma, Mwanza na Kagera, ambayo ni mikoa iliyoko hatarini kupata maambukizi ya virusi vya ebola," alisisitiza Taratibu.

Mtaalamu wa Masuala ya Afya ya Jamii na Dharura Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Faraja Mwaseja, alisema zoezi hilo litaanza kilitarajiwa kuanza juzi hadi Ijumaa.

Ofisa Afya mwandamizi wa Wizara ya Afya, Remidius Kakulu, alisema changamoto kubwa Kigoma ni kutokana na mwingiliano wa watu kutoka DRC na Burundi.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Paul Chaote, alikiri kuwa mkoa huo una changamoto ya baadhi ya mipaka kuwa wazi hususan njia zisizo rasmi kuna uwezekano wa ugonjwa huo kulipuka.

# PBZ yadai wakulima wa korosho Mtwara bil. 1.4/-

**Said Hamdani,** LINDI

BENKI ya Wananchi Zanzibar (PBZ) tawi la Mkoa wa Mtwara, inadai Jumla ya Sh. bilioni 1.4 ikiwa mikopo iliyobaki mikononi mwa wakulima, waliyokopeshwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Hayo yameelezwa na Ofisa Masoko wa Benki hiyo, Nassir Mohamed Zaid, alipokuwa akizungumza na Nipashe kwenye Maonyesho ya Wiki ya Wakulima Nanenane katika viwanja vya Ngongo, Manispaa ya Lindi.

Zaid alisema kiasi hicho kinachodai ni miongoni mwa mikopo ya Sh. bilioni 2.8 iliyotolewa kwa wanachama wakulima zaidi ya 2,000, vikiwamo vyama vya msingi na ushirika (AMCOS) 50 katika mikoa ya Mtwara na Lindi mwaka 2018/2019.

Alitaja maeneo ya wakulima walionufaika na mikopo hiyo ni wa Tandahimba, Newala, Namnyamba, Masasi mkoani Mtwara pamoja na kata mbili za Mkoa wa Lindi, ikiwamo ya Mnolela.

Zaid alisema katika mikopo iliyotolewa mwaka huo, kiasi kilichorejeshwa kwenye benki hiyo ni Sh. bilioni 1.4 sawa na asilimia 50 ya fedha zilizotolewa kwa mikopo msimu uliopita.

Alitaja sababu zilizochangia hali hiyo kuwa ni mfumo wa kuhakiki wakulima halisi uliokuwa umewekwa na serikali. Pia alisema kutokana na jitihada zinazoonyeshwa na wakulima, uongozi wa benki hiyo, unaendelea kujipanga upya kutoa mikopo mingine kuendeleza shughuli za kilimo. "Licha ya changamoto zilizopo kwa upande wetu, viongozi tunaendelea kujipanga, ikiwamo kufanya utafiti ili tuwapatie mikopo mingine," alisema Zaid. Zaid alikuwa akizungumza baada ya Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Evod Mmanda, kukamilisha kutembelea mabanda yaliyopo viwanja vya Maonyesho ya Nanenane Kanda ya Kusini.

Alisema licha ya changamoto zilizojitokeza, uongozi wa PBZ unaendelea kujiweka sawa kuendelea kuchangia michango yao katika kilimo, ambacho uzalisha ajira kwa zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania. Kwa upande wake, DC Mmanda akizungumza na waandishi wa habari wakati wa majumuisho, aliwahimiza wananchi wa mikoa ya Mtwara na Lindi kuyatumia mabonde yaliyopo kuzalisha vyakula ukiwamo mpunga ili kupunguza adha ya kuagiza mchele kutoka maeneo mengine.

# Sababu halmashauri kutofikia makusanyo

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

HALMASHAURI wilayani Mpanda mkoani Katavi, imefanikiwa kukusanya mapato ya ndani Sh. bilioni mbili kwa kipindi cha kuanzia Julai 2018, hadi Juni 2019, huku ikieleza sababu za kutofikiwa lengo la makusanyo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Hamad Mapengo, alisema hayo kwenye kikao cha kumaliza mwaka cha Baraza la Madiwani mwishoni mwa wiki.

Alisema halmashauri hiyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/2019 imekusanya kiasi cha Sh. 2,387,580,044.49 ikiwa ni mapato yao ya ndani kati ya Sh. 3,175,309,820.00 ikiwa ni sawa na asilimia 75.19 wakati kwa msimu uliopita walikusanya asilimia 90.

Mbali na kukusanya mapato hayo ya ndani, halmashauri hiyo kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha ilipanga kukusanya kiasi cha Sh. 25,804,825,692.98 kutokana na vyanzo vya mapato ya ndani, mishahara, matumizi mengineyo na maendeleo. Hata hivyo, walikusanya Sh.17,576,019,480.58 sawa na asilimia 68.11. Mapengo alisema halmashauri hiyo haikufikia lengo la kukusanya mapato yake ya ndani kwa asilimia 100 kutokana na sababu mbalimbali ambapo baadhi ya sababu ni kufutwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato ya ndani.

Alisema baadhi ya mapato yaliyokuwa yanakusanywa na halmashauri kuhamishiwa kwenye Serikali Kuu na kushuka kwa uzalishaji wa zao la tumbaku kutokana na kampuni za ununuzi wa tumbaku kushusha kilo wanazonunua zao hilo.

Mwenyekiti huyo aliwataka watendaji wa halmashauri hiyo kuendelea kukusanya mapato kwa bidii ili kuifanya halmashauri hiyo iweze kujiendesha. Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Romuli Rojasi, alisema hadi kufikia Machi mwaka huu halmashauri hiyo ilikuwa imekusanya mapato yake ya ndani yasiyo dhidi ya asilimia 30, na kuwa hata hivyo mapato yaliongezeka kuanzia Aprili.

Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Tanganyika, Reginald Mhango, aliihimiza halmashauri hiyo kuongeza kasi ya kukusanya mapato ya ndani ili kwa mwaka huu waweze kukusanya zaidi ya asilimia 80 ya mapato yao ya ndani.

## Wakulima waitwa Nanenane kupata elimu ya vipimo

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

WAKALA wa Vipimo (WMA) umewakaribisha wananchi wa Simiyu na mikoa ya karibu kuhudhuria katika maonyesho ya Nanenane ambayo yanafanyika katika Viwanja vya Nyakabindi Bariadi mkoani Simiyu.

Stella Kahwa, Mkurugenzi wa Ufundi wa WMA, alisema wananchi watakapotembelea banda lao watapata fursa ya kujifunza namna ya kufungasha bidhaa za wajasiriamali kwa kutumia vipimo sahihi na kuandika alama kwa usahihi katika kifungashio kwa lengo la kuongeza thamani za bidhaa wanazozalisha.

Alisema kwa kuwa mikoa ya kanda ya ziwa wakulima bado wanaendelea kuuza pamba, katika banda la wakala huo, wanatoa elimu ya utambuzi wa mizani sahihi iliyohakikiwa na iliyoidhinishwa kutumika katika zoezi la ununuzi wa pamba katika vyama vya msingi.

Kahwa aliongeza kuwa kwa sasa WMA inahakiki dira za maji hivyo wananchi watapata nafasi ya kujifunza namna ya uhakiki unavyofanyika katika dira za maji na namna ya kutambua dira ambazo zimehakikiwa na kufungwa lakiri ya Wakala kuhakikisha kunakuwa na biashara ya haki ambapo mamlaka za maji zinatoza fedha kwa usahihi kulingana na matumizi ya wateja wao.

Kwa mujibu wa Kahwa, serikali inafanya jitihada za kuanzisha masoko ya madini katika kila mkoa ili kuhakikisha kuwa madini hayatoroshwi na yanauzika kwa urahisi, na kuwa wananchi watakapo tembelea banda hilo watapata kufahamu mchango katika sekta ya madini.

Kahwa aliwataka wafanyabiashara kufanya kazi zao kwa uadilifu na kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa kwani adhabu zitolewazo kwa wakiukaji wa sheria ya vipimo ni kali. Kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo sura na. 340 na mapitio yake ya mwaka 2002, endapo mfanyabiashara atabainika kutenda kosa kinyume na sheria hiyo na akakiri kutenda kosa husika, atapaswa kulipa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 20,000,000 kwa kosa la kwanza kulingana na idadi ya makosa aliyotenda.

Endapo mtuhumiwa atakamatwa na kosa kwa mara ya pili na kuendelea na akipelekwa mahakamani akakutwa na hatia adhabu ni faini isiyopungua Sh. 500,000 na isiyozidi Sh. milioni 100 au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

# Wawili kizimbani tuhuma za kudhalilisha watoto miaka 12

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa Wete, imempandisha kizimbani mtuhumiwa , Omar Ali Hamad (28), mkaazi wa Mkanjuni Mtambwe Kusini kwa tuhuma za kumbaka mtoto wa miaka 12.

Akisomewa shtaka lake na mwendesha mashtaka wa Mahakama hiyo, Ali Amour Makame, mtuhumiwa huyo alikana kutenda kosa hilo na kuiomba mahakama impe dhamana.

"Mheshimiwa hakimu, mimi sijafanya jambo hilo wananisingizia tu, naiomba mahakama yako inipatie dhamana," alidai mtuhumiwa huyo.

Hakimu Abdalla Yahya Shamhuna, alikubali ombi la dhamana aliloomba mshtakiwa na kusema kesi hiyo itarudi tena mahakamani Agosti 19, mwaka huu.

Ilidaiwa mahakama hapo mtuhumiwa alitenda kosa hilo siku na tarehe isiyofahamika Jauari mwaka 2018 saa 7:00 mchana Mkanjuni Mtambwe Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa kuwa, bila ya halali alimbaka mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 12.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume cha kifungu cha 125 (1) (2) (e) na kifungu cha 126 (1) cha Sheria namba 6 ya mwaka 2004, Sheria ya Zanzibar.

Wakati huo huo, mahakama hiyo imempandisha kizimbani Juma Hamad Hassan (75) mkaazi wa Mkanjuni Mtambwe Kusini kwa tuhuma za kumfanyia unyanyasaji mkubwa mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 12.

Akisomewa shtaka lake na mwendesha mashtaka wa mahakama hiyo, Ali Amour Makame, mtuhumiwa alikana kutenda kosa hilo na kuiomba mahakama impe dhamana.

Hakimu wa mahakama hiyo, Abdalla Yahya Shamhuna, alikubali ombi la dhamana aliloomba mshtakiwa na kusema atakapokamilisha masharti yaliyotakiwa mahakama itampatia dhamana.

"Mtuhumiwa dhamana zako ziko wazi na utapewa dhamana utakapokamilisha masharti yalitakiwa," alisema hakimu.

Mtuhumiwa aliyakamilisha masharti ya dhamana na kesi hiyo itarudi tena mahakamani Agosti 19, mwaka huu.

Ilidaiwa mahakama hapo kuwa, mtuhumiwa alitenda kosa hilo Julai 11, mwaka jana, mchana, Mkanjuni Mtambwe Kusini Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa bila ya halali na kwa ajili ya kukidhi matamanio yake ya kimwili, alimvua nguo mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 12 na kumfanyia udhalilishaji.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume cha kifungu cha 139 (1) (a) na (2) (a) cha sheria namba 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.



Mchuuzi wa mifagio akisaka wateja kando ya Barabara ya Mwai Kibaki, katika eneo la Mikocheni A, jijini Dar es Salaam jana. Fagio moja linauzwa kwa bei ya 2,500/-. **PICHA: JOHN BADI**

# Kesi migogoro ardhi, mirathi zatikisa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KESI za migogoro ya ardhi na madai ya mirathi zimetajwa kukithiri kwa wananchi wa Shinyanga Mjini, kutokana na baadhi yao kupata elimu ya msaada wa kisheria, na kuanza kudai haki zao ambazo walidhulumiwa awali kutokana na kutozijua sheria.

Imeelezwa idadi kubwa ya wananchi hasa wa hali ya chini wamekuwa wakidhulumiwa mali zao kutokana na kutozijua sheria, pamoja na wengine kukosa fedha za kulipa mawakili kwa ajili ya kusimamia kesi zao, hivyo kujikuta wakikosa haki zao kwa mujibu wa sheria na kubaki kuwa wanyonge.

Hayo yalizungumza na meneja mradi wa huduma wa msaada wa kisheria, John Shija, kutoka Shirika la PACESH Shinyanga Mjini, ambao hutoa msaada huo wa kisheria bure kwa wananchi.

Alisema kesi nyingi ambazo wanazipokea kwenye shirika lao ni za migogoro ya ardhi pamoja na mirathi, zikifuatiwa na zingine za ukatili, ndoa, matunzo ya mtoto, madai pamoja na migogoro ya kazi.

"Shirika letu la PACESH mara baada ya kuanza kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara, mabonanza ya michezo, magulio, vyombo vya habari, pamoja na matukio ya kitaifa, ndipo watu wakaamuka na kuanza kudai haki zao ambazo walizulumiwa kutokana na kutozijua sheria," alisema Shija.

"Kesi ambazo zinaongoza ni za migogoro ya ardhi pamoja na mirathi, ambapo mwaka jana kesi za ardhi tulipokea 144, na mwaka huu hadi Juni tumeshapokea 23, za mirathi zilikuwa 85, na (2019) zimeshafika nane, ambapo baadhi bado zipo mahakamani na zingine zimeshakwisha na kila mtu alipata haki yake kisheria," aliongeza.

Naye mmoja wa wanufaika wa msaada huo wa kisheria kutoka Shirika la PACESH, Spora Sultani Masibuka mkazi wa Shinyanga Mjini, ambaye alikuwa ana kabiliwa na tatizo la mgogoro wa ardhi, ambapo kwa sasa ana miliki yake, alilipongeza shirika hilo na kutoa wito kwa wananchi walitumia ili kupata haki zao.

# Wanawake wahamasishwa kusoma Sayansi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAWAKE nchini wameshauriwa kusoma masomo ya Sayansi ili waweze kuingia katika masuala ya usafiri wa anga na kupata wataalamu wengi zaidi wa jinsia hiyo waliobobea katika fani hiyo.

Kaimu mkufunzi mkuu kitengo cha huduma katika viwanja vya ndege, Thamarat Abeid, alisema hayo wakati akizungumza katika maonyesho ya Nanenane kuwa changamoto kubwa iliyopo ni wanawake wengi kuogopa kusomea masomo ya Sayansi.

Alisema kumekuwapo na changamoto kubwa ya wanawake kuogopa kusomea masomo hayo, kutokana na mfumo uliopo kuwa yanafaa wanaume pekee jambo ambalo sio sahihi na kuwataka kujitokeza kwa wingi kusomea masomo hayo, ili waweze kufanya kazi kubwa ambazo zinadhaniwa ni za wanaume pekee.

Abeid aliwataka pia kujiunga kwa wingi katika Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC), kilichopo chini ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), ili waweze kuchukua kozi mbalimbali ambazo zitawasaidia kupata ajira kwa haraka.

Alisema, chuo hicho kilianzishwa mwaka 1985 na kimekuwa kikitoa kozi mbalimbali ikiwamo kuongoza ndege, kutoa taarifa za ndege angani, kozi ya wahandisi wa mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ya usalama katika viwanja vya ndege.

"Mpaka sasa hivi wamehitimu wanafunzi zaidi ya 3,476 kwa kipindi cha miaka minne na idadi kubwa ya wanafunzi wanatokea nchini Uganda, kati ya hao waliohitimu wanafunzi zaidi ya 500 wanatokea nchini Uganda na hiyo ni kutokana na huduma nzuri tunazotoa ikilinganishwa na vyuo vingine vilivyopo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

Aliongeza kuwa, mapato yatokanayo na chuo hicho yameongezeka na kwa mwaka wa fedha uliopita walikusanya Sh. bilioni mbili na kwa mwaka huu wanatarajia kukusanya Sh. bilioni tatu na wanategemea kuvuka malengo waliyopangiwa.

Vile vile, alifafanua zaidi kuwa, chuo hicho kipo katika mchakato wa kuwa kituo bora cha umahiri kimataifa, ili kiweze kukidhi vigezo vya kuwa kituo bora ni lazima watengeneze kozi zinazokidhi vigezo hivyo na wapo katika mchakato huo.

Naye Ofisa Habari wa Mamlaka hiyo, Bestina Magutu, aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi katika chuo hicho ili waweze kusoma kozi mbalimbali ikiwamo masuala ya usafiri wa anga kwa kuwa wanawake wakiamua wanaweza.

Alifafanua kuwa chuo hicho kimekuwa kikitoa huduma nzuri na zilizo bora kitaifa na kimataifa, ambazo huwawezesha kupata ajira ndani na nje ya nchi.




Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro (kulia), akisikiliza maelezo kuhusu bidhaa anazotengeneza mjasiriamali, Rosemary Masawe maarufu Katarina wa Karatu, wakati alipotembelea banda lake, lililopo katika maonyesho ya Nanenane kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini, katika viwanja vya Themi Njiro, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# AfCHPR yaenda Comoro kuhamasisha mkataba

**Na Allan Isack,** ARUSHA

UJUMBE wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), umeanza ziara katika nchi za Comoro na Zimbabwe, kuzihamasisha kuridhia mkataba ulioanzisha na mahakama hiyo.

Pia imezitaka nchi hizo kuweka azimio la kuruhusu watu binafsi asasi zisizo za kiserikali kuitumia mahakama hiyo moja kwa moja yenye makao yake jijini hapa.

Kwa mujibu wa Msajili wa Mahakama hiyo, Dk. Robert Eno, Rais wa Mahakama ya Afrika, Sylvain Oré, ataongoza ujumbe huo akiwa ameambatana na Jaji Ben Achour na maofisa wengine waandamizi kutoka idara ya usajili.

Dk. Eno alisema wajumbe hao watakutana na kufanya mazungumzo na marais, mawaziri wa mambo ya nje, mawaziri wa katiba na maspika wa bunge.

Alisema ujumbe huo utakuwa nchini Comoro, kuanzia Agosti 7 hadi 8, na nchini Zimbabwe utakuwa Agosti 14 hadi 15.

Alisema ziara hiyo, imelenga kuimarisha na kuitangaza mahakama hiyo ya Afrika yenye majukumu ya kutoa haki kwa binadamu na watu.

"Ziara hizi zitasaidia kukuza uelewa wa uwepo wa mahakama hii na kuzihimiza nchi za Afrika kusaini mkataba ulioanzisha Mahakama ya Afrika pamoja na kuazimia au kuruhusu watu binafsi kutumia mahakama hiyo.

"Ili mahakama iweze kufanya kazi yake sawa sawa na kisha kuimarisha mfumo wa haki za binadamu Afrika, nchi nyingi zinapaswa kuridhia mkataba huo na kuazimia kwa mujibu wa ibara ya 34 (6)," alisema Jaji Oré katika taarifa iliyotolewa na Msajili wa Mahakama hiyo, Dk. Eno mwishoni mwa wiki.

# Viongozi wa dini waaswa kukumbuka wasiojiweza

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

VIONGOZI wa dini nchini wametakiwa kurejesha fadhila kwa waumini wao kwa kuwasaidia wananchi na watu wasiojiweza.

Hayo yamesemwa jana na Nabii Mkuu Dk. Geor Davie wa huduma ya Ngurumo ya Upako, wakati akigawa fedha za kuwaongezea mitaji baadhi ya wafanyabiashara wadogo wa eneo la Kisongo lililopo ndani ya Halmashauri ya Arusha DC Wilaya ya Arumeru, mkoani hapa.

Alisema viongozi wengi wa dini wamekuwa hawarudishi fadhila kwa waumini wao, huku wengine wakisahau jamii inayowazunguka kwa kuwa hata katika vitabu vya dini imeandikwa watu wasio jiweza, yatima na maskini wasaidiwe.

Alimpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa jinsi anavyofanya kazi na kuwajali wanyonge na watu wasiojiweza.

"Mimi binafsi nitaendelea kumwombea pamoja na kumuunga mkono katika juhudi za kuleta maendeleo kwa wananchi na taifa kwa ujumla, maana anafanya kazi kubwa ya kumtukuza Mungu," alisema na kuongeza:

"Kutoa msaada huu ni njia moja wapo ya kumuunga mkono Rais wetu kwa kazi nzuri anazofanya na tutaendelea kumuunga mkono rais wetu ameonyesha njia ya kusaidia wanyonge na wasiojiweza na mimi kama kiongozi wa serikali ya ufalme wa Mungu nimeamua kumuunga mkono na leo sio mwanzo wala mwisho nitaendelea kutoa msaada kila siku kadiri Mungu anavyo niongoza," alisema.

Alisema katika serikali za duniani wananchi wa hali ya chini ndio wapiga kura na ndio walipa kodi, vilevile katika serikali ya ufalme wa Mungu wao ndio watoaji wakubwa wa sadaka na matoleo mbalimbali, hivyo kundi hilo likiwezeshwa watafanya zaidi ya jinsi wanavyofanya sasa katika serikali zote mbili.

Alisema fedha alizotoa jana kwa ajili ya kuwaongezea mitaji wajasiriamali wadogo wa eneo la Kisongo ni zaidi ya Sh. milioni 10.

Alisema huo ni mwendelezo wa kuwawezesha wafanyabiashara ndogo ndogo ambao kwa mwaka huu tangu Januari ameshatoa zaidi ya Sh. milioni 200, ikiwa ni pamoja na kuwajengea nyumba watu wasio na uwezo, kuwapa vijana pikipiki za biashara (bodaboda) pamoja na kutoa magari kwa watu mbalimbali, huku akiahidi kutoa pesa na mali kwa watu wengine kadiri Mungu atakavyo mwongoza.

Wakiongea baada ya kupokea msaada huo wa mitaji baadhi ya wajasiriamali wamemshukuru Nabii Mkuu, kwa kuwawezesha kibiashara huku wakisema utawasaidia kukuza biashara zao.

"Kwakweli namshukuru Mungu kwa kutuletea huyu baba, mimi nilikuwa na mtaji wa machungwa wa Sh.10,000, lakini akanipa Sh. 100,000 nashukuru kwa kuwa nitabadilisha biashara ya kuuza machungwa na nitaanza kuuza dagaa nashukuru sana," alisema Mary Kristofa.

Kwa upande wake, Marieta Daudi, alimshukuru kwa msaada huo na kuwataka viongozi wengine wa dini kuwa na moyo huo wa kutoa ili kuweza kuwainua wananchi wa chini na wasiojiweza.

# Mbunge atoa habari njema shule iliyofungwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Esther Mmasi, amesema timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), wameridhia Shule ya Sekondari Kolila, iliyokuwa imefungwa kutokana na kushindwa kujiendesha ifunguliwe.

Kwenye ukurasa wake wa moja ya mtandao wa kijamii, Mmasi ameeleza kuwa katika ziara yake ya kikazi Kata ya Old Moshi Mashariki, Jimbo la Moshi Vijijini, serikali kupitia Ofisi ya Ofisa Elimu Mkoa wa Kilimanjaro, imetoa kauli ya kuwarejeshea wananchi umiliki wa shule hiyo.

"Pamoja na kukusanya, kutatua na kuzipokea kero za wananchi wa Kata ya Old Moshi Mashariki, pia tumefanikiwa kutatua mgogoro wa Shule ya Sekondari Kolila. Katika ziara yangu niliambatana na timu ya Ofisa Elimu Mkoa na mwanasheria kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Kwa muda sasa, Mbunge huyo amekuwa akipigania kufunguliwa kwa shule hiyo hasa baada ya kudai mara kadhaa kufanya mawasiliano na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selamani Jafo.

"Utatuzi wa Shule ya Sekondari Kolila, serikali kupitia kwa Ofisa Elimu Mkoa imetoa kauli ya kuwarejeshea wananchi umiliki wa shule, hivyo shule hiyo itakuwa mikononi mwa serikali na si umiliki wa kanisa kama ilivyokuwa awali. Majibu hayo yametokana na uchunguzi wa kina uliofanywa na timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Elimu na Tamisemi."

Kwa mujibu wa mbunge huyo, serikali imeagiza watumishi waliokuwa wakifanya kazi katika shule hiyo kufanyiwa tathmini ya madai yao na stahiki zao ili walipwe.

Alipotafutwa jana kwa njia ya simu kutoa ufafanuzi kuhusu taarifa hiyo, Ofisa Elimu Mkoa wa Kilimanjaro, Paulina Nkwama, alisema "taratibu za mawasiliano na ninyi wanahabari, si unazifahamu eeh, haya tufuate taratibu."

Mwezi Septemba mwaka jana, Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Kilimanjaro ikiongozwa na Mwenyekiti wake Patrick Boisafi, iliielekeza serikali ihakikishe shule hiyo inafunguliwa.

# Kenya, Tanzania waanzisha jukwaa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MPANGO wa ushirikiano wa vijana baina ya nchi za Afrika na Ujerumani (AGYI), unaotekelezwa nchini na Shirika la Tanzania Youth Coaliation, umeanzisha jukwaa la pamoja kati ya nchi za Tanzania na Kenya ili kujadili changamoto za kitaaluma na matokeo chanya yanayopatikana kutokana na mpango huo.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Miradi wa Shirika la Tanzania Youth Coaliation (TYC), Erick Nyoni, jukwaa hilo linashirikisha wadau mbalimbali pamoja na shule zote za sekondari nchini ambazo zinafanya programu ya mabadilishano ya wanafunzi.

Akizungumza jana katika mkutano unaoendelea mkoani Kilimanjaro ambao umepewa jina la 'school camping conference', Nyoni alisema TYC mwaka jana ilifanya zoezi la kuzitambua na kuainisha shule zote nchini zinazofanya programu ya mabadilishano ya wanafunzi na kugundua hakuna jukwaa hilo.

"Tumeona kuna umuhimu wa kuwapo jukwaa la kukutanisha shule zinazofanya exchange program (mpango wa kubadilishana uzoefu) na shule za nchi nyingine tofauti ili kujifunza hizo exchange program zina changamoto gani na mambo mazuri yaliyopo katika mpango huo."

Akieleza zaidi kuhusu utekelezaji wa mpango huo, Meneja Mradi wa AGYI, Lyidia Maika, ameeleza kuwa Shirika la Tanzania Youth Coaliation (TYC), limepata nafasi ya kuwa watekelezaji wakuu wa mpango huo nchini Tanzania.

"Kuna miradi ya muda mrefu inayohusisha kujifunza kama ASA, ambao ni wa kujifunza elimu ya maendeleo inayofanyika Ujerumani. Miradi hiyo inalenga vijana wanaotaka kuelewa zaidi juu ya ulingano na utegemeano wa ulimwenguni, wakijiuliza maswali ya kina ya namna wanavyotaka kuimarisha ulimwengu kuwa endelevu na wenye usawa," alieleza.

Miradi mingine ni Weltwart, ambao ni mradi wa maendeleo wa kujitolea ulioanzishwa mwaka 2008 na Wizara ya Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa ya nchini Ujerumani (BMZ), wenye lengo la kuwapa vijana fursa za kujifunza kupitia mabadilishano ya kitamaduni.

Vile vile, Meneja huyo ameutaja mradi mwingine kuwa ni ENSA, ambao unalenga kuanzisha na kukuza uhusiano wa kishule baina ya Ujerumani, Afrika, Asia, Latini Amerika na nchi za Kusini Mashariki mwa Bara la Ulaya.

ENSA inakusudia zaidi katika kuwasaidia vijana ambao wako pembezoni kijamii na kimfumo.

Juzi, akizindua mpango huo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Avemaria Semakafu, alizitaka shule 24 za sekondari nchini zinazoshiriki programu za mabadilishano ya wanafunzi, kukubaliana kwanza na wabia wanaotekeleza mpango huo kwa kuzitambua changamoto zinazojitokeza na kuzitatua.

Alizitaka shule hizo kabla ya kushiriki katika programu hiyo, kila shule kufanya makubaliano na mbia ambaye atashiriki naye kwenye mpango huo na kuweka malengo ambayo yanalenga kujifunza, lakini pia kuongeza ujuzi kwa wanafunzi.



Katibu wa CCM wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Ally Kidunda, akizungumzia zoezi la usajili wa wanachama wa CCM, kwa njia ya kielektroniki wilayani humo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC atoa somo kwa CCM waendesha bodaboda

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amekipa somo Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani humo, akikieleza kuwa njia pekee ya kulikamata kwa sasa kundi kubwa la waendesha Bajaj na bodaboda, sio kuwa na maneno mengi, bali wafanye kazi ili watu hao wawaamini kama wanavyomwamini Rais John Magufuli.

Ole Sabaya alitoa darasa hilo jana, wakati alipokutana na waendesha Bajaj wa Mji Mdogo wa Bomang'ombe katika kikao cha pamoja cha kujadili changamoto zinazowakabili na kutafuta namna bora ya kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu.

"Hawa waendesha Bajaj ni hazina ya uchaguzi mkuu ujao na ninyi chama changu (CCM), hawa watu kwenu ni wa muhimu wakati wa uchaguzi tu, namna peke yake ya kukamata kundi kubwa sio kuwa na blah blah nyingi, fanya kazi watu watakuamini tu," alisema na kuongeze:

"Yaani waulize leo kama tunarudi kwenye sanduku la kura tunamtafutia kura Rais John Magufuli, kwa kuwa mnafikiri atatumia nguvu nyingi sana kujieleza, watakwambia hapana kwa sababu amejipambanua kwa kazi zenye tija kwa taifa."

Ole Sabaya amesisitiza kuwa kundi la waendesha bajaji na pikipiki maarufu kama bodaboda ni muhimu sana, lakini baadhi ya viongozi wa serikali na vyama vya siasa wamekuwa wakiwaacha ya mwisho, wakati wa uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani.

Alisema mara nyingi CCM imekuwa ikijisahau na kuwaacha na kujikuta wakiunga mkono vyama vya upinzani, lakini ukiwaangalia sio kwamba wanakaa huko walipo kwa sababu wanapapenda, ila wanakaa huko kwa sasabu wako viongozi wanakwepa kuwasaidia, wana wadharau na kundi hilo linajikuta likisema bora wakose wote.

Katika mkutano huo, Mkuu huyo wa Wilaya aliwaeleza waendesha bajaji hao kuwa, kwa kiwango fulani ofisi yake imeanza kupunguza matatizo yao, huku akiwaahidi kushughulikia mpango wa kukopeshana wa madereva hao.

"Nina kiwango cha mikopo yenu ya bajaji, kwa sababu wanachotaka benki ni ku deposit (kuweka) asilimia 20 ya fedha yote inayohitajika. Sasa ile asilimia 20 kwa bajaji 15 ninazo tayari. Ila jambo ambalo nimewaitia la muhimu nimeona fedha hizi baadaye tunaweza kuanza kuwakopesha halafu zikaanza kuwagombanisha, nasitaki ninyi muanze kugombana."

Ukurasa 18



Majenerali Sudan wawazidi raia kete mzunguko wa kidiplomasia

## Wanawake Dar waungana kuwania nafasi za uongozi



Ukurasa 19

## Kimataifa



## Obama akosoa viongozi wanaotoa kauli za chuki

Ukurasa 17


# siasa

JUMATANO AGOSTI 7, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




## SADC inapofungua fursa za maendeleo Tanzania

Ukurasa 15

### BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-8

PIUS Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa Serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia, Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa na leo hii tunaendelea kutokea tulipoishia wiki iliyopita. Endelea na sehemu hii ya nane ya kitabu hicho inayoanzia na Madai ya Tume ya Nyalali, 1992...

**(ii) Madai ya Tume ya Nyalali, 1992**

Hata mapendekezo ya Tume ya Nyalali kwamba, muundo wa Muungano uwe wa serikali tatu haukutokana na matakwa ya wananchi walio wengi. Taarifa ya Tume hiyo yenyewe inasema hivi (Kitabu cha Kwanza, uk 121):

- "Kuhusu ile hoja inayosema kwamba, muundo wa serikali tatu unadaiwa na watu wach-

Endelea 16



Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

## Sera za Trump sasa zavuruga uhusiano ya Korea, Japan

Ukurasa 20

# Hamasa kubwa wanawake kuwania nafasi za kuchaguliwa mwaka 2020

**Na Theodatus Muchunguzi**

UNAWEZA kusema hamasa ni kubwa kuwawezesha wanawake kugombea uongozi wa kuchaguliwa katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Safari hii imewekwa mikakati mbalimbali kufanikisha lengo hili, ikiwamo kushirikishwa makundi mbalimbali, wakiwamo wanaume kufanya hamasa.

Hili linafanyika kwa lengo la kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya kufanya maamuzi kama mabaraza ya madiwani, Bunge na Baraza la Wawakilishi.

Kadhalika, lengo ni kuwawezesha wanawake kuacha kusubiri hisani ya Rais katika nafasi za kuteuliwa pamoja na viti maalum, ambavyo vimekuwa vinadaiwa kuwadhalilisha wanawake katika vyama vya siasa.

Harakati za kuhamasisha wanawake kugombea nafasi za kuchaguliwa zimeshika kasi zaidi Zanzibar na Pemba kwa upande wa Tanzania Visiwani.

Wadau wa mtandao wa jinsia kikiwamo Chama Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) ofisi za Zanzibar, ndio wanaoongoza harakati za uhamasishaji huo kwa kushirikisha wadau wakiwamo viongozi wa dini, vyama vya siasa na makundi mengine.

Wiki iliyopita nilishuhudia moja ya mikutano mikubwa ya kuhamasisha wanawake kugombea uongozi katika shehia mbili za Majenzi na Shumba Mjini Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambapo wahamasishaji wakiwamo viongozi wa dini, wanasiasa na wengine walizungumza masuala kadhaa kwa wanawake pamoja na vijana waliojitokeza.

Salehe Jema, Katibu wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Kaskazini Pemba, anasema sasa ni wakati mwafaka kwa kinamama kujitokeza kugombea nafasi za uongozi wa kuchaguliwa kwa kuwa wana uwezo mkubwa.

Lakini anaeleza kusikitishwa na hali ya sasa kutokana na Baraza la Mji Micheweni halina madiwani wanawake wa kuchaguliwa.

"Sijui kwa nafasi za uwakilishi kama wawakilishi wanawake wa kuchaguliwa mnafika saba. Mnategemea hisani ya Rais au viti maalum... huku ni kujidhalilisha, la kufanya ni kuchukua fomu za kugombea katika mabaraza, uwakilishi na ubunge," alisema.

Jema anawahamasisha wanawake kuwa jasiri kwa kuwaiga wanawake kadhaa ambao waliwahi kushika nafasi za juu nchini na kuzitumikia kwa mafanikio.

Miongoni mwa wanawake anawataja kuwa ni Julie Maning ambaye aliwahi kuwa waziri wa sheria katika serikali ya awamu ya kwanza na Thabita Siwale ambaye alikuwa waziri wa elimu.

Wengine ni Dk. Asha-Rose Migiro, Amina Salum Ali ambaye aliwahi kuwa waziri wa fedha Zanzibar (sasa Waziri wa Viwanda na Bishara Zanzibar), na kwamba pia aliwahi kushika nafasi za uongozi kimataifa pamoja na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

"Hawa wote wamefanya vizuri, kwa nini na ninyi msifanye?" anahoji na kuongeza: "Hamuwezi kuwa mawaziri au makamu wa rais bila kuwa wabunge au



Wanawake wa shehia za Majenzi na Shumba Mjini Wilaya ya Micheweni, wakiwa katika mkutano wa kuhamasishwa kugombea uongozi katika Shule ya Sekondari Micheweni wiki iliyopita. **PICHA: THEODATUS MUCHUNGUZI**

wawakilishi."

Jema anawashauri vijana wa Zanzibar wakishaoa kuacha kuwaonea wivu wake zao, badala yake wawaruhusu wajitokeze kugombea udiwani, ubunge na uwakilishi.

Mwanasiasa huyo anawataka wanawake kujiunga na vyama vya siasa ili wapate nafasi za kugombea kwa kuwa sheria ya sasa ya Tanzania hairuhusu mgombea binafsi bali inawataka wagombea wote kupitia vyama vya siasa. Isaack Maganza, mchungaji kutoka Kanisa la RGC Chake Chake, anawataka wanaume kuondoa mifumo dume kwa kuwanyanyapaa wanawake, na kuwa sio kweli kuwa wanawake hawaruhusiwi kuingia katika siasa.

"Mwanamke kuingia katika uongozi pia ni uchumi, uongozi si elimu bali kipaji ambacho Mungu amemjalia mtu...kama ni kipaji tumwachie fursa hiyo, ukiwa mwanasiasa ndipo unakuwa kiongozi," mchungaji Maganza anawaeleza wanawake.

Sheikh Abdallah Nassoro Adallah, kutoka Jumuiya ya Maimamu (Jumaza), anasema katika maeneo mengi duniani wanaume ndio wanaoshika nafasi za uongozi, lakini wapo wanawake kadha walioweza kuchomoza na kuwa viongozi wazuri, huku akimtaja Bibi Titi Mohamed, mmoja wa waasisi wa Tanu kuwa miongoni mwao.

Anawataka wanawake kuingia katika uongozi wa kuchaguliwa ili kuleta mabadiliko na maendeleo katika jamii, ikiwamo kuondoa kero zinazowakabili hususan udhalilishaji.

Hata hivyo, Sheikh Abdallah maarufu kama 'Maulid' pamoja na kuhamasisha wanawake kuingia katika siasa, anawapa angalizo kuwa wakishapata uongozi wasiwadharau wala kuwakwaza waume zao, vinginevyo watakuwa wamepoteza malengo yaliyokusudiwa.

Riziki Ali Hamad, mmoja wa vijana wa kike wa shehia hizo, anasema kuwa wanawake wana uwezo, na kuwahamasisha wenzako kujitokeza kugombea uongozi.

"Wanawake tunaweza, najiandaa kugombea nafasi ya uwakilishi katika uchaguzi mkuu wa 2020," anasema Riziki kwa kujiamini katika mkutano huo wa hadhara uliofanyika katika Shule ya Sekondari Micheweni.

Mtumwa Hamis Jongo, Mratibu Msaidizi wa Jinsia Shehia ya Mjenzi, anasema kuwa wanawake wana uwezo wa kuwa viongozi bora, lakini anawataka wanaume wajitafakari kwa nini wanaendelea kuwanyanyasa wanawake.

Kuluthum Ali Kombo, Mratibu wa Wanawake na Watoto Sheria ya Majenzi, anaeleza kuwa mwaka 2017 aligombea nafasi ya uenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), lakini alishindwa.

Kuluthum anasema kuwa licha ya kushindwa hajakata tamaa, na kwamba mwakani atagombea ingawa haelezi nafasi anayokusudia kugombea.

Meneja wa Sera na Utetezi wa Tamwa Zanzibar, Hawra Shamte, anasema chama chao kinahamasisha wanawake kushiriki siasa kupitia kampeni ya kuleta mabadiliko kwa wanaume (male change agent) katika maeneo yote ya Zanzibar na Pemba.

Kwa mujibu wa Shamte, lengo ni kuwafikia wanawake 4,000 kupitia wahamasishaji ambao ni viongozi wa vyama vya siasa, dini na jamii ili kubadilisha mitazamo ya jamii kwamba mwanamke hastahili kugombea uongozi.

Alisema walianza tangu mwaka 2015 kwa kuwafikia wanawake takribani 300 na kuwawezesha, ingawa hawakupata matokeo chanya ya kuwaingiza katika nafasi za kuchaguliwa.

Anasema miongoni mwa vikwazo ni vyama vya siasa kutowasaidia wanawake pamoja na baadhi ya viongozi wa dini kutokana na aya za dini kutowaruhusu wanawake.

"Hivyo wengi walianguka, tulitafuta ushauri katika baadhi ya taasisi kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kubaini changamoto, na zikaainishwa kuwa ni vyama vya siasa, wao kwa wao na viongozi wa dini," anasema Shamte.

Anaongeza kuwa njia waliyoshauri itumike ni kubadili mitazamo ya jamii kwamba wanachokifanya sasa ni kuzifikia wilaya zote za Unguja na Pemba, na kuwa zilishaundwa timu 20, ambapo 10 ni za Unguja na 10 Pemba.

Shamte pia anabainisha kwamba kuna timu ya wajuvi (think tank) 10 inayojumuisha Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), viongozi wa dini, wanasiasa na Baraza la Wawakilishi pamoja na ushirikishaji wa vyombo vya habari.

Shamte anasema katika jitihada za kuongeza idadi ya wanawake katika siasa, Tamwa kupitia mradi wake wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Uongozi wa Siasa (Women Empowerment Political Leadership), mwaka 2020 wameamua kuwahamasisha wagombee katika majimbo badala ya viti maalum.

"Ndio maana tunahamasisha vyama viwakubali. Tunahamasisha wengi tofauti na mwaka 2015 ambapo waliopo barazani hawazidi asilimia 37. Wanawake wana msimamo kuwa watagombea mwakani," anasema.

Na Mashaka Mgeta

# SADC inapofungua fursa za maendeleo Tanzania



Rais John Magufuli (mbele ya jukwaa), akifungua Maonyesho ya SADC juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

TANZANIA ipo katika wiki ya mwanzo ya 'hekaheka' za mkutano wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), zilizoanza kwenye ukumbi wa Julius Nyerere International Conference (JNIC) jijini Dar es Salaam.

Juzi, Rais John Magufuli atakayekabidhiwa Uenyekiti wa SADC unaotokana na utaratibu wa mzunguko, alifungua wiki na maonyesho ya nne ya viwanda katika ukanda wa Kusini mwa Afrika, vikiwa ni sehemu katika ratiba ya kufanyika kwa mkutano huo.

Baada ya wiki na maonyesho hayo kukamilika Agosti 8, mwaka huu, siku inayofuata kutaanza vikao vya makatibu wakuu na wataalamu wa nyanja mbalimbali kutoka nchi wanachama wa SADC, kikao cha mawaziri wa nchi na hatimaye Agosti 17 na 18, mwaka huu utafanyika mkutano rasmi wa wakuu wa nchi.

Inaweza kuaminika kwamba kufanyika kwa mkutano huo hapa nchini ni muendelezo wa utamaduni wa SADC kufanya hivyo kwa nchi ambayo Rais ama Mkuu mwenye mamlaka ya dola, anakabidhiwa uenyekiti.

Ndio maana mkutano wa 38 wa SADC uliofanyika Agosti 17 na 18, mwaka jana kwenye Kituo cha Mikutano cha Safari Court jijini Windhoek, Jamhuri ya Namibia ukiwa na kauli ya "Kukuza maendeleo ya miundombinu na uwezeshaji wa vijana kwa ajili ya maendeleo endelevu', ulimchagua Rais wa nchi hiyo, Dk. Hage Geingob kuwa Mwenyekiti.

Dk. Geingob aliyekabidhiwa wadhifa huo kutoka kwa Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini, atamkabidhi wadhifa huo Rais Magufuli kwenye mkutano wa SADC wa mwaka huu. Wote watatu watakutana kwenye kikao kitakachofanyika Agosti 16, mwaka huu, kwa mujibu wa utaratibu wa SADC.

Mbali na Rais Magufuli, viongozi wengine watakaokabidhiwa nyadhifa katika muundo wa SADC ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Dk. Faraj Mnyepe, atakayekuwa mwenyekiti wa mikutano ya wataalamu wa SADC na Waziri wa wizara hiyo, Profesa Palamagamba Kabudi, atakayekabidhiwa uenyekiti wa baraza la mawaziri wa jumuiya hiyo.

Nafasi nyingine zinazopaswa kuchukuliwa na Watanzania katika muundo huo, zitajulikana na kutangazwa baada ya Rais Magufuli kukabidhiwa rasmi Uenyekiti wa SADC.

Kufanyika kwa mkutano hapa nchini kumekuja na kauli mbiu ya maonyesho yanayoendelea kwenye viwanja vya Gymkhana, Karimjee na JNIC inayosema 'Mazingira bora kwa maendeleo endelevu na jumuishi ya viwanda, kukuza biashara, viwanda na ajira,'inayoendana na azma ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda.

Geofrey Mbinga, mtaaluma wa masuala ya uchumi anasema uwiano uliopo kati ya kauli mbiu hiyo na azma ya Tanzania katika kuelekea uchumi wa viwanda, ni fursa pana inayopaswa kutumiwa na Watanzania hasa wafanyabiashara wadogo na wa kati, kubaini namna bora ya kukuza mitaji na biashara zao kulifikia soko la SADC.

"Wapo wafanyabiashara wenye viwanda katika ngazi mbalimbali watafika nchini kushiriki maonyesho, wapo watakaokuja kutafuta ushirikiano nakadhalika... sasa ni wakati muafaka kwa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo ambayo kama ingekuwa ni kuifuata kwenye nchi nyingine, wangetumia gharama kubwa," anasema Mbinga.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, jumla ya washiriki 2,026 kutoka ndani na nje ya nchi, walikuwa wamethibitisha kushiriki, ingawa idadi hiyo ilitarajiwa kuongezeka kutokana na kuwapo maombi mapya.

Manyanya akasema washiriki hao wanatoka katika sekta za viwanda, ujasiriamali, taasisi za umma na zile za binafsi kutoka mataifa mbalimbali hususani yaliyo wanachama wa SADC.

Maonyesho hayo yatakayofikia kilele chake Agosti 8, mwaka huu, yatafuatiwa na kikao cha makatibu wakuu walio wataalamu katika sekta mbalimbali. Kisha kutakuwa na kikao cha mawaziri wa nchi wanachama wa SADC na hatimaye mkutano wa wakuu wa nchi hizo.

**TANZANIA YA VIWANDA**

Licha ya kauli mbiu ya maonyesho ya nne ya viwanda kujielekeza katika sekta ambayo Tanzania imeipa kipaumbele katika mageuzi ya uchumi wake, Mkuu wa Idara ya Viwanda na Ushindani wa SADC, Johansein Rutaihwa, anasema jumuiya ina mkakati wa kuendeleza viwanda kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015 - 2063.

Kwa mujibu wa Rutaihwa, mkakati huo uliozinduliwa mwaka 2015 na wakuu wa SADC, utafikia kilele cha awamu yake ya kwanza mwaka kesho.

Kwa maana nyingine, kufanyika maonyesho ya viwanda hapa nchini ni fursa nyingine ambayo Watanzania wanaweza kupima safari ya kuelekea katika uchumi wa viwanda katika mukhtadha wa mkakati huo wa SADC.

Mbinga anaizungumzia hali hiyo kwa kusema, ufuatiliaji na tathmini zitakazofanyika kupitia maonyesho hayo na maudhui mengine katika mijadala na hotuba wakati wa mkutano wa SADC, vitaiwezesha Tanzania 'kujipanga vizuri zaidi' katika muendelezo wa kuwekeza kwenye viwanda.

Anasema hatua hiyo ni muhimu kwa vile SADC kupitia mkakati wake wa kuendeleza viwanda, itakuwa inaingia katika awamu ya utekelezaji wa kati ya mwaka 2021 mpaka mwaka 2050. Kwa upande wake, Rutaihwa anasema katika utekelezaji wa mkakati huo, SADC inaziangalia rasilimali ambazo nchi wanachama zinazo, zikiwamo zinazotokana na kilimo, madini, utalii na hivyo kuzijengea uwezo zaidi katika kufikia malengo yao ya kiuchumi.

**KWA NINI KUCHANGAMKIA FURSA**

Nchi za SADC ni moja ya masoko makubwa ya kikanda ambayo kama Watanzania watazibaini fursa na kujikita kufanya biashara katika maeneo tofauti, ni wazi kwamba watakuwa miongoni mwa wanufaika wakubwa wa ushirikiano huo wa kikanda.

Hali hiyo inatokana na ukweli wa kitakwimu kwamba biashara zinazofanyika ndani ya ukanda huo zipo kwa kiwango kidogo kinachofikia asilimia 21 tu, kwa mujibu wa Rutaihwa.

Ni kutokana na hali hiyo, Watanzania wanapaswa kuutumia mkutano wa SADC kama 'nyenzo' muhimu ya kubaini fursa kama masoko, taratibu na uhitaji kama ilivyo kwa azma ya jumuiya kutaka biashara kati ya raia na nchi za jumuiya hiyo kuwa na bidhaa zilizosindikwa na si malighafi kama ilivyozoeleka.

Mshauri wa masuala ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa, Oscar Mbise anasema pamoja na kuwapo fursa hizo na nyinginezo, Watanzania hawapaswi kufikiri kwamba ni rahisi kuzifikia, kwa vile upo ushindani mkubwa kati ya nchi wanachama, kila moja ikiwahimiza watu wake `kuzikimbilia'.

"Tunaposema ushirikiano wa kikanda ni dhana inayotuleta pamoja, lakini kukiwa na ushindani mkubwa kati ya nchi na nchi, hivyo isije ikaonekana kama ni rahisi kulifikia na kulimudu soko la SADC, tunatakiwa kujipanga vizuri ili kumudu ushindani uliopo," anasema.

***Mwandishi wa makala haya anapatikana katika simu namba +255 754 691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.***

UCHAMBUZI

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-8

Inatoka Uk. 13

ache tu, hoja hiyo ni ya kweli. Lakini, tumezingatia kwamba, katika kuamua mambo mazito ya kisiasa, siyo busara kuweka uzito mkubwa kwenye takwimu peke yake…Kwa maoni yetu, mtazamo unaofaa zaidi katika suala la kisiasa kama hili, ni kupima uzito wa hoja yenyewe inayotolewa, kuliko kuangalia wingi wa watu wanaoitoa. Tunafikiri kuwa, hoja ya muundo wa serikali tatu katika muungano wetu ina uzito wa kutosha, na haitakuwa ni busara kuikataa hoja hiyo kwa kufuata mtazamo wa takwimu tu."

(iii) Madai ya Tume ya Kisanga, 1999

Hali kadhalika, pendekezo la Tume ya Jaji Kisanga la kuwa na muundo wa serikali tatu halikutokana na maoni ya wananchi wengi.

Taarifa ya Tume ya Jaji Kisanga (Kitabu cha kwanza, uk 43) inasomeka kama ifuatavyo:

- "Jedwali na. 1.1 linaonesha kwamba, kwa Zanzibar muundo unaopendelewa zaidi ni muundo wa serikali mbili, ambapo 96.25% ya maoni yaliyotolewa yanapendelea muundo huo. Unaofuata ni muundo wa serikali tatu ambao umependekezwa na 3.48% ya maoni yote. Aidha, muundo ambao unaonesha kutokupendwa ni ule wa serikali moja ambao ni 0.8% ya maoni yaliyotolewa ndiyo yalipendelea muundo huo. Jedwali na. 1.2 linaonesha kwamba, kwa upande wa Tanzania Bara muundo unaopendwa zaidi vilevile ni ule wa serikali mbili, ambapo 84.97% ya maoni yaliyotolewa yanapendelea muundo huo. Unaofuata ni muundo wa serikali moja ambao unapendekezwa na 9.91% ya maoni yote. Aidha muundo usiopendekezwa ni wa serikali tatu ambapo maoni yaliyopendekeza muundo huo ni 4.32% tu kati ya yale yalitolewa. Jedwali na. 1.3 linaonesha kwamba, kitaifa, muundo wa serikali mbili ndio unaopendwa zaidi ( 88.27%), ukifuatiwa na muundo wa serikali moja (6.54%), na mwisho ni serikali tatu (4.32%)."

Lakini, pamoja na takwimu hizo, pendekezo la Tume ya Jaji Kisanga lilikuwa kwamba:

- "Baada ya kutafakari na kutathmini miundo yote ya Muungano iliyopendekezwa, na kuchambua manufaa na matatizo ya kila muundo, Tume inashauri Serikali kwamba, Muundo unaofaa katika mazingira ya sasa ya nchi yetu ni ule wenye serikali tatu."

(iv) Madai ya Tume ya Jaji Warioba, 2013

Machapisho yote ya Tume ya Jaji Warioba, ambayo ni Kitabu cha Randama (uk 48), Kitabu cha Takwimu (uk 67), Bango Kitita la Randama (uk 153), pamoja na Hotuba ya Mwenyekiti Warioba aliyoitoa kwenye Bunge Maalum la Katiba wakati wa kuwakilisha mapendekezo ya Tume yake (uk 31); yote hayo yanadai kuwa "takwimu zinaonesha kwamba wananchi wengi wamependekeza mfumo wa Muungano wa Serikali tatu."



Baba wa Taifa la Zanzibar, Abeid Karume (kulia waliokaa), akiwa na viongozi wenzake wa Serikali ya Kwanza ya Mapinduzi. **PICHA: MTANDAO**

> "Baada ya kutafakari na kutathmini miundo yote ya Muungano iliyopendekezwa, na kuchambua manufaa na matatizo ya kila muundo, Tume inashauri Serikali kwamba, Muundo unaofaa katika mazingira ya sasa ya nchi yetu ni ule wenye serikali tatu."

Lakini, kumbe madai hayo, kwamba, "Wananchi wengi" walipendekeza mfumo wa Muungano wa serikali tatu, siyo ya kweli hata kidogo, kama uchambuzi ufuatao unavyothibitisha:

Kitabu cha Tume ya Jaji Warioba cha Takwimu za ukusanyaji wa maoni ya wananchi kuhusu Mabadaliko ya Katiba kina takwimu za aina mbili. Aina ya kwanza ni idadi ya sampuli za maoni, na aina ya pili ni idadi ya watu waliotoa maoni.

Uhalisia wa Takwimu hizo

Kwa upande wa Tanzania Bara, takwimu zinaonesha sura ifuatayo:

(i)Jumla ya maoni yote yaliyokusanywa na Tume ya Jaji Warioba, yalikuwa 684,303.

(ii)Jumla ya maoni yaliyotolewa katika eneo la Muungano, yalikuwa ni 39,223, sawa na asilimia 5.7%.

(iii)Jumla ya maoni yaliyotolewa kuhusu muundo wa Muungano, yalikuwa 26,625, sawa na 3.9%.

(iv)Jumla ya maoni yaliyopendekeza muundo wa Serikali moja, yalikuwa ni 3,564, sawa na asilimia 0.5%.

(v)Jumla ya maoni yaliyopendekeza muundo wa Serikali mbili, yalikuwa ni 6,459, sawa na asilimia 0.9%.

(vi)Jumla ya maoni yaliyopendekeza muundo wa Serikali tatu, yalikuwa ni 16, 321, sawa na asilimia 2.4.

Kwa upande wa Zanzibar, takwimu zinaonesha sura ifuatayo:

(i)Jumla ya maoni yote yaliyokusanywa na Tume ya Jaji Warioba yalikuwa 49,671.

(ii)Jumla ya maoni yaliyotolewa katika eneo la Muungano yalikuwa ni 37,881, sawa na asilimia 76.3%.

(iii)Jumla ya maoni yaliyotolewa kuhusu muundo wa Muungano yalikuwa ni 19,351, sawa na asilimia 0.05%.

(iv)Jumla ya maoni yaliyopendekeza muundo wa Serikali moja yalikuwa ni 25, sawa na asilimia 0.05%.

(v)Jumla ya maoni yaliyopendekeza muundo wa Serikali mbili yalikuwa ni 6,693, sawa na asilimia 13.5%

(vi)Jumla ya maoni yaliyopendekeza muundo wa Serikali tatu yalikuwa ni 960, sawa na asilimia 1.9%.

(vii)Jumla ya maoni yaliyopendekeza muundo wa Muungano wa Mkataba yalikuwa ni 11,659, sawa na asilimia 23.5%.

**Uchambuzi**

Kwa upande wa Tanzania Bara, kati ya maoni 39,223 yaliyozungumzia eneo la Muungano, ni maoni 26, 625 ndiyo yaliyozungumzia suala la muundo wa Muungano. Kati ya idadi hiyo ya maoni 26,625, maoni yaliyopendekeza muundo wa serikali tatu yalikuwa ni 16, 321 tu, sawa na asilimia 61%.

Ni muhimu ifahamike kwamba, hii 61% ni asilimia ya wale wananchi 26,625 tu waliotoa maoni juu ya Muungano, na siyo asilimia ya Watanzania wote! Lakini, pamoja na ukweli huo, hii ndiyo asilimia iliyotumiwa na Tume ya Warioba kudai kwamba, Wananchi wengi wa Tanzania eti walipendekeza muundo wa Serikali tatu!

Kwa hiyo, ukweli unabaki kuwa ni wananchi wachache sana (yaani, 16,321 kati ya Watanzania zaidi ya milioni 40) ndio walipendekeza muundo wa Muungano wa Serikali tatu.

Kwa upande wa Zanzibar, kati ya jumla ya maoni 49,671 yaliyozungumzia eneo la Muungano, ni maoni 960, sawa na asilimia 1.9% tu, ndiyo yaliyopendekeza muundo wa Serikali tatu.

**6.3.3 Msimamo imara wa Mwalimu Nyerere**

Msingi wa msimamo imara wa Mwalimu Nyerere ulikuwa kutetea Mkataba wa Makubaliano ya Muungano, ambao ndio ulikuwa umeweka muundo wa Serikali mbili. Msimamo huo ulishika sehemu kubwa sana katika kukwamisha madai ya Muundo wa Serikali tatu, kama ninavyoeleza hapa chini.

Kumbuka maneno aliyoyaandika Mwalimu Nyerere katika makala zake "Asili ya Muungano wa Serikali mbili,"kwamba, "Hofu yetu ilikuwa kwamba, tukiwa na serikali moja, Tanganyika itaonekana kuwa imeimeza Zanzibar. Hatukutaka tudhaniwe, hata kwa kimakosa, kwamba tumenzisha ubeberu mpya! Basi, tukatafuta mfumo ambao utaiondolea Zanzibar hofu hii ya kumezwa. Hiyo ndiyo asili ya muundo wa Serikali mbili. Badala ya kutunga muundo wa Muungano kama wapumbavu, tulitazama hali halisi yetu ilivyokuwa, na tukabuni mfumo uliotufaa zaidi."

Msimamo imara wa Mwalimu Nyerere wa kutetea muundo wa Serikali mbili unadhihirika katika matukio yote yaliyojaribu kuingiza muundo wa Serikali tatu wakati wa uhai wake, kama ifuatavyo:

(i)Kuhusu Rasimu ya Katiba iliyoandaliwa na Rais Aboud Jumbe

Rasimu ya Katiba ya Rais wa Zanzibar Aboud Jumbe, ilikuwa imelenga kuleta mabadiliko ya Katiba ambayo yangeweka muundo wa Serikali tatu, maelekezo yanathibitisha msimamo imara wa Mwalimu Nyerere wa kukataa muundo wa Serikali tatu unaonekana katika nukuu ifuatayo ya kumbukumbu za Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM cha Februari 1984, wakati wa kuhitimisha mjadala juu ya jambo hilo:

Mwenyekiti Nyerere (akielekeza maneno yake kwa Rais Aboud Jumbe, Makamu wa Rais na Makamu Mwenyekiti wa CCM):

Makamu: Hali ya hewa imechafuka Zanzibar.Katika hali hiyo, wewe huwezi tena kuendele kuiongoza Zanzibar. Lazima ujiuzulu.

Aboud Jumbe: Mwenyekiti, nakubali, najiuzulu.

Mjumbe Job Lusinde: Mwenyekiti, Ndugu Aboud Jumbe ana vyeo vingi katika serikali zote mbili na pia katika Chama Cha Mapinduzi. Naomba atamke wazi anajizulu nafa si ipi?

Aboud Jumbe: Mwenyekiti, najiuzulu nafasi zote za uongozi nilizokuwa nazo.

Mwenyekiti Nyerere: Basi, itabidi uniandikie mara moja barua ya kujiuzulu kwako.

Aboud Jumbe: Mwenyekiti, nitafanya hivyo mara baada ya kutoka hapa.

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**

## Obama akosoa viongozi wanaotoa kauli za chuki

RAIS wa zamani wa Marekani, Barack Obama, amewataka Wamarekani kukataa lugha za chuki na kibaguzi kutoka kwa viongozi wao.

Obama ambaye amekuwa akiongea kwa nadra tangu alipoondoka madarakani, japo hakumtaja kiongozi yeyote kwa jina, lakini kauli yake hiyo imekuja huku Rais Donald Trump, akiwa katika harakati za kujinasua kuwa kauli zake dhidi ya wahamiaji ndizo chanzo cha kuchochea mauaji nchini humo.

Jumla ya watu 31 wameuawa katika mashambulio ya bunduki kwenye majimbo ya Texas na Ohio, mwishoni mwa wiki iliyopita.

Akiwa madarakani, Obama alipigana bila ya mafanikio kudhibiti umiliki wa silaha za moto nchini Marekani.

Aliiambia BBC mwaka 2015 kwamba, kushindwa kupitisha kwa sheria za kudhibiti silaha, ndilo jambo kubwa alilofeli akiwa kama kiongozi wa nchi hiyo.



Rais wa zamani wa Marekani, Barrack Obama. **PICHA: MTANDAO**

Obama amekuwa akikwepa kuzungumzia sera za Trump, hususani ya uhamiaji ambayo imekuwa ikipingwa na makundi tofauti. Hata hivyo, safari hii ametoa tamko.

"Inabidi kwa pamoja tukatae lugha zinazotoka kwenye kinywa cha kiongozi wetu yoyote ambaye analisha mazingira ya uoga na chuki ama anayefanya ubaguzi kuwa jambo la kawaida," anasema na kuongeza:

"Viongozi wanaowafanya watu ambao hawafanani nasi kuonekana kama mashetani, ama wanaodai kwamba watu wengine wakiwemo wahamiaji wanahatarisha mfumo wetu wa maisha, ama wanaodai kuwa Marekani ni ya jamii moja tu ya watu, ni wa kuwapinga."

TRUMP AHUTUBIA

Rais Trump amekemea chuki na imani kuwa mtu mweupe ana nguvu zaidi alipohutubia umma baada ya tukio la mashambulizi yaliyogharimu maisha ya watu 31 katika miji ya Texas na Ohio.

Ametaka mabadiliko katika udhibiti wa silaha, pia hukumu ya kifo iwakabili watu wanaotekeleza mauaji ya watu wengi, lakini kutazama tena sheria zinazohusu silaha.

"Ugonjwa wa akili na chuki hufyatua risasi, na si silaha," alisema katika Ikulu ya Marekani juzi.

Hakuonyesha kuunga mkono hatua za kudhibiti bunduki, zilizopendekezwa na Congress.

"Kwa sauti moja, taifa letu lazima likemee ubaguzi wa rangi, uhasama na mtazamo kuwa watu weupe ndio wenye nguvu… mawazo haya mabaya lazima yashindwe… chuki haina nafasi Amerika," alisema.

Maoni yake yalikuja muda mfupi kabla ya mtuhumiwa huko El Paso, Texas, kushtakiwa kwa mauaji.

Polisi wa El Paso pia walithibitisha kwamba waathirika wengine wawili walikufa hospitalini, hivyo idadi ya vifo vya Texas kuongezeka hadi kufikia 22.

Trump alisema sera kadhaa, ikiwemo ya ushirikiano zaidi kati ya wakala wa serikali na kampuni za vyombo vya habari vya kijamii, mabadiliko ya sheria za afya ya akili na kumaliza "utukufu" wa ghasia katika utamaduni wa Amerika lazima ziangaliwe.

Alitaka sheria kali zitakazoruhusu watekelezaji wa sheria kuchukua silaha kutoka kwa watu wanaoaminika kuwa tishio kwao wenyewe au kwa wengine.

Alisema mashirika ya serikali lazima yafanye kazi kwa pamoja ili kubaini watu wanaoweza kufanya vitendo vya ukatili, kuzuia upatikanaji wao wa silaha za moto na akapendekeza kuwaweka kizuizini kama njia ya kuwazuia washambuliaji.

Akaelekeza wizara ya sheria kupendekeza sheria kuhakikisha wale wanaotenda uhalifu wa chuki na mauaji ya watu wengi wanakabiliwa na adhabu ya kifo.

Rais alikosoa video za mitandaoni kwa kuchochea vurugu katika jamii.

"Ni rahisi sana leo kwa vijana wenye shida kujiingiza kwenye utamaduni unaosherehekea vurugu…lazima tuzuie au kupunguza hili na inapaswa kuanza mara moja," alisema.

Hata hivyo, hakuzungumzia ukosoaji juu ya msimamo wake mkali dhidi ya uhamiaji haramu, ambao wapinzani wanasema umechangia kuongezeka kwa mashambulio yanayochochewa na ubaguzi.

Awali Trump alikuwa akiandika kwamba watunga sheria katika Congress wanapaswa kupitisha sheria za ukaguzi kwenye vifurushi na "mageuzi ya uhamiaji yanayohitajika sana."

Alisema kuwa "yuko wazi na yuko tayari kujadili maoni yote ambayo yatafanya kazi" na kwamba wanasiasa wa Republican na Democrats wanapaswa kuungana pamoja kushughulikia hili.

KILICHOTOKEA EL PASO

Wachunguzi wanatazama kama shambulio lilichochewa na chuki, huku ikielezwa kuwa adhabu inaweza kuwa kifo.

Takriban watu 20 waliuawa na wengine 26 wakijeruhiwa katika ufyatuliaji wa risasi kwenye duka la jumla mjini El Paso jimbo la Texas.

Gavana wa Jimbo hilo, Greg Abbot, alitaja shambulio hilo kuwa mojawapo ya siku mbaya zaidi katika historia ya jimbo la Texas.

Maofisa wa polisi wanachunguza iwapo shambulio hilo lililofanyika maili chache kutoka kwa mpaka wa Marekani na Mexico lilikuwa la uhalifu wa chuki.

Mtu mwenye umri wa miaka 21 kwa sasa anazuiwa na polisi.

KILICHOTOKEA DAYTON

Kanda za video katika mitandao ya kijamii zilionyesha watu wakikimbia huku milio mingi ya risasi ikisikika barabarani.

Inadaiwa kwamba shambulio hilo lilifanyika nje ya klabu ya burudani ya Red Peppers katika barabara ya tano ya E.

Klabu hiyo baadaye ilichapisha katika mtandao wa twitter ikisema wafanyakazi wake wako salama.

Polisi wanasema wote walioathirika walikuwa barabarani.

Polisi wanasema mshukiwa huyo alikuwa akiishi katika eneo la Allen, Dalla yapata kilomita 1,046 Mashariki mwa El Paso. Ametajwa na vyombo vya habari vya Marekani kuwa ni Patrick Crusius.

Kanda za video za CCTV zilizodaiwa kuwa za mshambuliaji huyo ambazo zilionyeshwa katika vyombo vya habari vya Marekani, zinaonyesha mtu aliyekuwa amevalia Tisheti nyeusi pamoja na vilinda masikio.

**BBC**

UCHAMBUZI

# Majenerali Sudan wawazidi raia kete mzunguko wa kidiplomasia

**Na Ani Jozeni**

MAJENERALI ambao hivi sasa wako katika mazungumzo yasiyoisha ya kugawana madaraka na raia nchini Sudan, wanaelekea kukamata usukani wa mwenendo wa mazungumzo baada ya naibu mwenyekiti wa Baraza la Mpito la Kijeshi, Jenerali Mohamed Hassan Dagalo (aitwaye Hemeti) kuzuru Misri.

Alifanya mazungumzo yaliyofuatiliwa kote duniani na Rais Abdel Fattah al-Sisi, ambako majadiliano hayo yalitoa picha ya mazungumzo kati ya wakuu wa nchi mbili jirani, na siyo nafasi ya Misri katika kusuluhisha mgogoro wa utawala nchini humo. Usuluhishi unafuatiliwa na Ethiopia, Umoja wa Afrika.

Katika majadiliano kati ya Jenerali al-Sisi na Jenerali Dagalo, suala la msingi lililokuwa mezani ni Misri kuunga mkono juhudi za uimarishaji wa uthabiti wa kisiasa na usalama nchini Sudan.

Huo ni mpangilio wa hisia unaoonyesha wazi kuunga mkono upande wa majenerali katika mzozo wa kikatiba unaoendelea nchini humo.

Jenerali Dagalo anajulikana nchini Sudan kuwa ndiye anayeshikilia makali kwa upande wa utawala wa mpito wa kijeshi, anayeungwa mkono na vikosi maalum vya jeshi la nchi hiyo ambavyo kimsingi vinaidhibiti nchi.

Licha ya kuwa siyo mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi, anaonekana ana nguvu.

Mazungumzo ya Al Sisi na Hemeti yalilenga ushirikiano wa jumla kati ya Misri na Sudan, ikiwa ni pamoja na miradi ya uunganishaji wa umeme, kwa mujibu wa Ofisi ya Rais jijini Cairo, suala ambalo wachunguzi wa habari wanaona ni mwendelezo wa mageuzi kutoka demokrasia pana kwenda utawala wa kijeshi wenye mwelekeo wa wastani.

Ni mara ya kwanza utawala wa kijeshi wa Sudan umeingia katika mahusiano na majadiliano ya ushirikiano na nchi nyingine, na kufanikisha ziara ya Misri ni ushindi.

Na mwelekeo wa majadiliano ni kielelezo kuwa hisia za nchi muhimu kikanda zinafanana na majenerali hao.

Kwa mfano wakati wa ziara ya Hemeti nchini Misri, kulikuwa na ujio wa Mfalme Abdullah II wa Jordan kwa lengo la kuendeleza majadiliano ya amani Mashariki ya Kati, mkakati ambao unaendana na kile alichokifuata Hemeti.

Ni kuacha kuendeleza mazungumzo na'wanademokrasia' na 'wanaharakati' wa Mamlaka ya Palestina kwa upande mmoja na kundi la Hamas eneo la Gaza kwa upande mwingine, na kulenga mahusiano kati ya nchi.

Ni juhudi za kuona jinsi ya kutumia dola za Marekani bilioni 50 au zaidi ambazo utawala wa Rais Donald Trump umeahidi kuingiza kufikia 'amani ya kiuchumi' ya ukanda huo.

Wachunguzi wa habari wanaaminisha kuwa Sudan na Misri zina uhusiano wa jadi wa kihistoria ambao kimsingi bado unaendelea, kwani mto Nile ni muhimu kwa uchumi wa Misri tangu zama za kale, na matawi yake yanaunganika Sudan.

Isitoshe kuna mwingiliano wa kijamii na kiitikadi kati ya nchi hizo mbili, ambako utawala wa kijeshi wa Sudan unaendana na makundi ya kiharakati nchini Misri yanayopingana na utawala wa kijeshi.

Sasa umekuwa utawala wa kiraia baada ya Jenerali Al Sisi kupigiwa kura, kumaliza muhula na kupigiwa kura tena, kidemokrasia.

Kutokana na hali ya Sudan kushindwa kukamilisha mabadiliko halisi kutoka utawala wa Jenerali al Bashir ambaye pia alikuwa anatawala kiraia, utawala wa kijeshi unaanza kuonekana ni tunu.

Nchi za jirani hazitaki mazingira ya ugomvi usioisha nchini humo, na ni wazi kuwa endapo kuna ukinzani wa kina kati ya jeshi na viongozi wa kiraia jeshi lazima lisikilizwe. Uamuzi uko kwake.

Ila bado kuna kizuizi cha kina katika mwelekeo wa jeshi la Sudan, kuwa hali ikivuka mpaka uwezo wa kusikilizana na viongozi wa kiraia ukaharibika kabisa, nchi inaweza kuingia katika hatua nyingine ya mapinduzi, badala ya kutulia na kutengemaa.

Ni hapo kunatokea tofauti za kihisia na mwelekeo katika ngazi za juu za utawala wa mpito wa kijeshi uliopo, kati ya wale wanaoona kuna haja ya kudhibiti tu hali ilivyo, au kwa lugha ya mtaani 'kanyaga twende,' na wale wenye hisia ya kidemokrasia.

Wanahofia hali isiharibike, umwagaji damu uanze, vikwazo.

Kwa upande mwingine kuna nchi kama Marekani ambayo hisia zake hazitofautiani sana na zile za washirika wake katika Mashariki ya Kati, ambao wanaunga mkono utawala wa kijeshi unaodhibiti demokrasia hatarishi ya kimapinduzi.

Hata hivyo, kwa upande wa Sudan haielekei kuwa Marekani inaona hali ya Libya au Misri, ambako itikadi ya kiharakati na siasa kali ni wazi ilikuwa inakaribia kuteka nchi, na kule Misri walishinda uchaguzi mkuu na kuwa na viti zaidi bungeni, wakapitisha sheria za kiharakati.

Makundi ya kijinsia na wanafunzi yakarudi mitaani.

Nchini Sudan harakati ya kidemokrasia imeongozwa na vikundi vya kitaaluma na vyama vya wanafunzi, ambavyo kwa jadi yao ni mrengo wa kiliberali na siyo wa siasa kali kama kina hayati Dk. Mohamed Morsi nchini Misri.

Alikuwa mgombea wa kundi la Muslim Brotherhood wakati wa uchaguzi mkuu baada ya mapinduzi kumng'oa mtawala wa muda mrefu Hosni Mubarak na kumpeleka jela, na kundi hilo liliposhinda likaona limepata ridhaa ya kutekeleza sheria ndoto za kidini, zisizoendana na wakati, yaani uhuru wa mtu binafsi na usawa wa kijinsia.

Ndiyo hali ya Misri ikazorota tena, jeshi likaingilia kati kurudisha



Rais Abdel Fattah al-sisi wa Misri (kushoto), akiwa na Kiongozi wa Baraza la Mpito la Kijeshi la Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan (kulia), walipokutana jijini Cairo nchini Misri. **PICHA: MTANDAO**

> Kwa mfano wakati wa ziara ya Hemeti nchini Misri, kulikuwa na ujio wa Mfalme Abdullah II wa Jordan kwa lengo la kuendeleza majadiliano ya amani Mashariki ya Kati, mkakati ambao unaendana na kile alichokifuata Hemeti.

utawala wa kiliberali, wa wastani, wa uhuru.

Ziara ya Jenerali Dagalo nchini Misri ni hatua ya kutaka kufifisha uwepo wa Ethiopia katika juhudi za kufikia uelewano kuhusu kuundwa kwa serikali ya mpito inayoshirikisha raia, ila dai la kutaka raia ndiyo waongoze kipindi hicho cha mpito linaelekea kukwama.

Hata hivyo, licha ya kutiwa saini makubaliano yanayolipatia jeshi nafasi ya kuongoza kipindi cha mwelekeo kwa miezi 18 halafu raia wachukue kipindi kinachofuata, kuna hatihati ya makubaliano kusainiwa na kuanza kutumika.

Uelewano unaosikika kutoka kwa viongozi wa waandamanaji hauendani na moto wa harakati unaoendelea barabarani, kwa walio wengi wanataka raia wachukue usukani.

Juhudi za Ethiopia kusuluhisha mvutano wa utawala nchini Sudan umefanya dunia kusikilizia juhudi hizo zimefikia wapi, huku Umoja wa Afrika (AU), kimsingi ukijiunga na Ethiopia katika kutafuta suluhu inayolenga kuheshimiwa kwa madai ya demokrasia ya waandamanaji.

Ziara ya Hemeti nchini Misri haiingizi nguvu nyingine ya usuluhishi bali inafuta umuhimu wa juhudi hizo kwa hatua ya kuitambua Sudan kama iliyo na utawala halisi unaokubalika, na ulio na uwezo wa kuchukua nafasi yake katika mashauri ya kimataifa. Ni kuona maandamano kama suala la ziada.

Ukiangalia kwa uwezo wa kiuchumi na mahusiano ya nje, kujipanga Ethiopia na AU nyuma ya waandamanaji kulifanya utawala wa kijeshi wa mpito uonekane ndiyo hasa kikwazo, ndiyo wasioelewa wananchi wanataka nini.

Ziara ya Hemeti nchini Misri imegeuza kibao katika hali hiyo, kuipatia serikali ya kijeshi ya mpito sura ya ukawaida katika mahusiano kikanda na kimataifa, hivyo kuanza kujenga taswira kuwa ni viongozi wa maandamano ambao wanataka 'matokeo makubwa sasa' hali inayoweza kuparaganyisha nchi.

Badala ya majenerali kutuhumiwa kuwa hawaelewi juhudi za Ethiopia na AU, kwa kufunga na kufungua kofia ya Abracadabra aliyoleta Hemeti kutoka Misri, viongozi wa waandamanaji watageuziwa kibao.

Misri imekuwa ndiyo mshenga wa utawala wa kijeshi wa mpito Sudan kuwa unakubalika.

UCHAMBUZI

# Wanawake Dar waungana kuwania nafasi za uongozi

## •Ni baada ya kupata mafunzo

Na Sabato Kasika

MOJA ya malalamiko ya muda mrefu ya wanawake ni kukosa haki za msingi ndani ya jamii, ikiwamo kupata nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali za maamuzi, hasa kwenye ulingo wa siasa kama vile udiwani na ubunge.

Si katika nafasi hizo tu bali pia kwenye ukuu wa wilaya na mikoa, nafasi ambazo wanaamini bado zinachukuliwa na wanaume huku wao wakiachwa pembeni kana kwamba hawana uwezo wa kuongoza.

Wamekuwa wakitoa kilio hicho, wakizingatia kuwa mikataba na makubalino mbalimbali katika uga wa kitaifa na kimataifa imetoa kipaumbele kwenye usawa wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na kuondolewa kwa aina zote za ubaguzi dhidi yao.

Mkataba wa kuondolewa kwa aina zote za ubaguzi kwa mfano unatokana na maazimio ya Mkutano wa nne wa Kimataifa wa Wanawake uliofanyika Beijing nchini China mwaka 1995, na kuwa chachu ya wanawake kudai haki zao.

Katika kuhakikisha wanawake wanashika nafasi nyingi za uongozi, ni muhimu kuwaelimisha na kuwajengea uwezo wa kujiamini na kuvunja vikwazo vinavyowazuia kuwania nafasi hizo.

Ndivyo ambavyo Taasisi ya Kuwezesha Wanawake na Kulinda Watoto ya Ekama Developement Foundation Tanzania, imefanya kwa baadhi ya wanawake kutoka vyama mbalimbali vya siasa mkoani Dar es Salaam.

Wanawake 20 kutoka vyama vyenye wabunge vya CCM, Chadema, NCCR-Mageuzi na ACT-Wazalendo, wamepata mafunzo ya siasa na uongozi kwa muda wa mwaka mmoja.



Mwanafatina Said (kulia) akipokea cheti kutoka kwa mgeni rasmi Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kijitonyama, Philip Kumanya (wa pili kushoto), baada ya mafunzo. Kushoto ni mkurugenzi wa Ekama Kokuteta Mtembei. **PICHA: SABATO KASIKA**

### LENGO LA MAFUNZO

Ofisa wa Jinsia wa Ekama, Wahilina Kejo anasema yalikuwa ni kwa ajili ya kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

"Mafunzo yaligawanyika kwenye masomo saba na kulikuwa na walimu mbalimbali, waliofundisha masomo hayo hapa hapa jijini Dar es Salaam," anasema.

Kejo anataja masomo hayo kuwa ni kutatua migogoro katika jamii, Haki ya kushiriki katika siasa, haki za binadamu, majukumu ya viongozi wa siasa, kuzungumza mbele ya hadhara na sheria ya vyombo vya habari.

"Somo jingine lilikuwa ni majukumu na sifa za viongozi wa Serikali Kuu na masomo yote yalifundishwa na walimu mbalimbali wakiwamo, Profesa Mwesiga Baregu, Dk. Matrona Kabyemerwa na Rashid Kejo," anasema.

Anasema mafunzo hayo yalianza Julai mwaka 2018 na kumalizika wiki iliyopita, ambapo wahitimu 20 walikabidhiwa vyeti vyao.

"Unaweza kushangaa kwanini mafunzo yamechukua mwaka mmoja, lakini ndivyo tulipanga na tunaamini kwamba wanafunzi wote wameiva kwa ajili ya kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika siasa," anasema.

Akielezea jinsi walivyowachagua wanawake hao, anasema Ekama iliandika barua kwenye vyama hivyo ngazi ya wilaya ikiomba kila chama kutoa wanachama watano kushiriki katika mafunzo hayo.

"Ombi letu lilikubaliwa, kila chama kikatoa idadi hiyo ya wanachama wakiwamo viongozi wa ngazi ya kata ambao tumewapa mafunzo ambayo yatawawezesha kushiriki katika chaguzi bila wasiwasi wowote," anasema.

### MKURUGENZI

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Kokuteta Mutembei, anawataka wanawake kutobweteka na badala yake watumie fursa zilizopo kuwania nafasi za uongozi katika siasa kwenye ngazi mbalimbali.

Anasema, hatua hiyo itasaidia kuongeza idadi kubwa ya wanawake wa kuchaguliwa kuanzia ngazi ya mtaa hadi jimbo, badala ya kutegemea viti maalum au kuteuliwa.

Mutembei anasema, wanawake hawana budi kuachana na dhana ya kuendelea kuongozwa kwa kila nafasi za uongozi ndani ya vyama vya siasa, badala yake wajiongeze kuwania wenyewe uongozi.

"Sisi wanawake ni wadau wakubwa kwenye demokrasia ya vyama vingi, tunashiriki katika siasa kwa nafasi mbalimbali kama wagombea na wapigakura, ni wahamasishaji katika kampeni, wasimamizi kwenye uchaguzi na waandishi wa wapigakura, lakini ushiriki wetu wa moja kwa moja kwenye maamuzi ya kisiasa bado uko chini ya asilimia 50," anasema Mutembei.

> "Msiishie hapo tu bali hata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 mjitokeze kuwania udiwani na ubunge ili ikiwezekana, idadi ya madiwani na wabunge wa kuchaguliwa iwe sawa kati ya wanawake na wanaume," anasema.

Anabainisha, hatua hiyo inatokana na mtazamo wa kijamii na wanawake wenyewe kuhusu siasa, na hivyo anawataka waliohitimu mafunzo wawe chachu katika maeneo yao kwa kuwania uongozi katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"Msiishie hapo tu bali hata katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 mjitokeze kuwania udiwani na ubunge ili ikiwezekana, idadi ya madiwani na wabunge wa kuchaguliwa iwe sawa kati ya wanawake na wanaume," anasema.

Anafafanua kwamba wanawake wana uwezo wa kusimama wenyewe kupata nafasi za uongozi katika siasa kama walivyo wanaume, hivyo kwa mafunzo waliyopata ana uhakika hilo litafanyika.

### WAHITIMU

Wakizungumza kwa niaba ya wenzao, baadhi ya wahitimu wa mafunzo hayo, kila mmoja anaeleza mtazamo wake.

Kada wa CCM, Mwanafatina Said, anasema yamewaunganisha na kuacha tofauti zao za kisiasa.

"Tunachojua ni kwamba Tanzania ni moja, ila ina vyama vingi, hivyo jambo la msingi ni kuheshimiana...kwa muda wote wa mwaka mmoja tuliokuwa tunakutana katika mafunzo, tulikuwa kitu kimoja," anasema.

Mwanafatina anasema ushirikiano huo wa bila kujali itikadi za vyama wataundeleza ili kudumisha demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini, kwa kutambua kwamba Tanzania ni moja ila ina vyama vingi.

Naye Anna Mboya wa NCCR-Mageuzi, anasema mafunzo hayo ni muhimu yakaenezwa nchi nzima ili kupanua wigo wa wanawake wengi zaidi kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika siasa.

Naye Vaileth Sanga kutoka Chadema, anasema mwanzoni mwa mafunzo hayo alikuwa akiwaona wanawake wenzake wa CCM kama maadui, lakini sasa anatambua umuhimu wa kushirikiana bila kujali itikadi za kisiasa.

"Sisi sote ni Watanzania, tunapaswa kuweka Utanzania mbele kuliko itikadi za vyama...mafunzo haya yamenifundisha mengi sana kwenye siasa na tumemaliza tukiwa wamoja na tuendeleze umoja huu," anasema Sanga.

Saumu Rashid wa UDP anasema baadhi ya wanawake huwa ni waoga wa kugombea uongozi, lakini sasa yeye atakuwa miongoni mwa wale watakaopeleka elimu kwao ili wabadilike.

"Nilichopata nitakieneza kwa wengine ambao wamekuwa wakidhani kwamba uongozi umewekwa kwa ajili ya wanaume tu ili wabadilike na kujitokeza kuwania kuanzia Serikali za Mitaa," anasema Saumu.

Mwanachama wa ACT-Wazalendo, Catherine Semhando, anasema mafunzo hayo si tu kwamba yamewajengea uwezo wa kuwania uongozi, bali pia yamekuwa ni chachu ya kuwaunganisha pamoja kama Watazania.

# Sera za Trump sasa zavuruga uhusiano ya Korea, Japan

Na Nimi Mweta

RAIS Donald Trump wa Marekani, akiwa anajivunia ushindi wa kina katika mvutano wa kibiashara kati ya Marekani na China ambako Marekani imeongeza ushuru wa forodha mara mbili kwa bidhaa kutoka China, sasa anavuna asichojua alipanda.

Ni baada ya Japan kutumia sera hizo hizo ila si kwa mkasa mzima wa mauzo ya China nchini Marekani ila kwa kampuni ya Huawei, kuwa kuuziwa vipengele vya teknolojia kunahatarisha usalama wa Marekani.

Japan hivi karibuni ilibaini jinsi vipengele vya teknolojia vilivyouzwa Korea Kusini vinaishia Korea Kaskazini.

Matokeo yake ni Japan kuchukua hatua za dhati za kuiondoa Korea Kusini kati ya washirika wake wakuu kibiashara wanaopata kipaumbele na kuondolewa kila aina ya vizuizi, na sasa nchi hiyo ambayo inaunda 'utatu' dhidi ya China na Korea Kaskazini ukanda wa Mashariki ya Mbali, pamoja na Korea Kusini na Marekani, sasa iko kivyake.

Marekani imeachwa njiapanda, haijui iunge mkono hatua za Japan au iendelee kutaka suluhu katika suala hilo, ila si rahisi kufanya hivyo kwani imekataa kata kata suluhu suala la Huawei. Kwa hali yoyote masuala hayo ni pacha.

Wachambuzi wa masuala ya usalama wa taifa na biashara kwa upande mwingine wanaafiki nchini Marekani kuwa nchi hiyo haina mbinu za kumaliza mgogoro huo.

Hiyo ni licha ya kuwa hata nchini Japan suala hilo limezua taharuki kwani mauzo ya vipengele vya teknolojia kwa Korea ni eneo muhimu la biashara ya bidhaa za aina hiyo.

Korea Kusini ina maendeleo makubwa katika fani ya teknolojia za mawasiliano lakini kwa hali yoyote ile Japan ilitangulia, hivyo inaongoza kwa utafti katika maeneo kadhaa muhimu. Kufuta au kukata biashara hiyo kwa kina haitakuwa 'poa.'

Kwa upande mwingine, wananchi wameanza kuhamasishwa na maandamano kufanyika miji tofauti Korea Kusini, siyo tu kuhusiana na tofauti hizo za biashara bali kutonesha vidonda vya Wakorea kuhusu maovu waliyotendewa na majeshi ya Japan, chini ya utawala wa kifashisti enzi za Vita Vikuu vya Pili duniani.

Ni suala ambalo hata leo Wakorea (kama walivyo Wachina) kuna wakati wanaanza kutoa machozi wakikumbushiwa yaliyotokea, na tangazo la kuiondoa Korea Kusini kama mshirika muhimu wa biashara inaonyesha dharau.

Hawaoni suala la kibiashara kuwa na msingi ila dharau, kwa maana Japan haikuinua suala hilo lijadiliwe; ilichukua tu hatua.

Wananchi wa Korea Kusini katika maandamano maeneo mengi wanawataka wenzao kuachana na bidhaa kutoka Japan, hali ambayo inaweza kuwa tatizo kwa baadhi ya kampuni kubwa za Japan.

Uchumi wa Japan kwa kiwango kikubwa umetegemea mauzo nje ya nchi, na ukanda wa Mashariki ya Mbali ni moja ya masoko muhimu, au labda muhimu zaidi.




Rais wa Korea Kusini, Moon Jae-in (kulia) na Waziri Mkuu wa japank, Shinzo Abe, kwenye Mkutano wa G-20 jijini Osaka, Japan, Juni 28, 2019. **PICHA: MTANDAO**

Licha ya kuwa Korea Kusini haina wingi wa watu kama mataifa yanayoizunguka, uwezo wake wa kununua ni wa hali ya juu.

Juhudi za awali za kupatanisha nchi hizo mbili ziligonga mwamba kutokana na muonekano kuwa hatari ya kurushwa makombora kutoka Korea Kaskazini bado mbichi, kwani mazungumzo kati ya Marekani na utawala wa Kikomunisti wa Korea Kaskazini yanasuasua.

Matokeo yake ni kuwa hali ya uhasama inaweza kuongezeka wakati wowote na Japan inahofia vipengele vya teknolojia kutoka huko visije kusaidia Korea Kaskazini kuimarisha mifumo ya makombora, ukwepaji rada, n.k.

Korea Kusini haijashtuka teknolojia ilifikaje Kaskazini; wana siri za Kikorea.

Badala ya kufanya uchunguzi na kutoa uhakikisho wa dhati kwa Japan na Marekani kuwa kamwe teknolojia haitavuja kupelekwa kwa utawala hasimu wa Pyongyang, Serikali ya Rais Moon Jae-in jijini Seoul imetafakari kuliendea Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara (WTO).

Ni hatua ambayo kama ilivyo kwa Marekani inaleta wasiwasi kama kampuni za nchi hiyo zitamudu kuvuruga uhusiano na Korea Kusini, hasa kwa sababu kuna maeneo yanayofanana katika suala la Huawei.

Uchumi wa Korea Kusini kwa Japan ni kama China kwa Marekani.

> Korea Kusini ina maendeleo makubwa katika fani ya teknolojia za mawasiliano lakini kwa hali yoyote ile Japan ilitangulia, hivyo inaongoza kwa utafti katika maeneo kadhaa muhimu. Kufuta au kukata biashara hiyo kwa kina haitakuwa 'poa.'

Kwa mfano takwimu za biashara zinaonyesha kuwa mwaka 2017, Japan iliuza vipengele teknolojia vya thamani ya dola za Marekani bilioni 10.4 kwa Korea Kusini, kiasi cha asilimia 20 ya mauzo yote nchi za nje kwa bidhaa hizo.

Ni wazi kuwa Japan inaweza ikafidia kwa kuongeza mauzo yake kwa nchi zinazokua kiteknolojia katika ukanda huo na Asia ya Kusini kwa jumla, na hata barani Ulaya, wakati Korea Kusini itabidi itafute njia nyingine.

Haitakuwa rahisi kwani Marekani itakuwa na hofu vile vile ya vipengele teknolojia kutua Pyongyang, na lazima isitesite.

Licha ya kuwa hadi sasa wachunguzi wa habari wanaangalia zaidi mzozo huo utakavyotatuliwa, baadhi ya wafuatiliaji wa masuala ya uchumi wanaona ni mtihani kwa Korea Kusini kama ilivyo kwa China katika suala la Huawei.

China haijafungua soko lake la teknohama halafu inapania soko la dunia na kampuni kubwa yenye nguvu kubwa ya dola nyuma yake, wakati katika masuala ya usalama ina uhasama wa wazi na Korea Kusini na Japan kuhusu visiwa na mipaka ya bahari.

Pia ina uwezekano wa vita na Marekani endapo itaamua kuingilia na kuitwaa Taiwan.

Korea Kusini kwa upande mwingine ina hisia kali ya uzalendo wa Kikorea hivyo pamoja na uhasama uliopo kati ya pande hizo mbili za Korea iliyogawanyika ambazo kisheria bado ziko vitani kwani mapigano yalisimamishwa tu mwaka 1952, bila mkataba wa amani.

Maofisa wengi nchini humo wana shauku ya kupata unafuu katika biashara endapo Korea Kaskazini itafikia makubaliano na Marekani kuondoa hali ya uhasama kati ya pande hizo mbili.

Kuhamisha vipengele teknolojia ni kama kununua hisa katika shughuli za teknohama zinazokua Kaskazini.

Kwa wakati uliopo inaelekea nchi zote mbili zitayumba kwa kiasi fulani kutafuta uelekeo kiuchumi na kisiasa, wakati Korea Kusini ikiwa zaidi imegubikwa na ukinzani kuhusu hatua hiyo, kwa maandamano na kuelezea chuki kwa Japan.

Serikali ya nchi hiyo haina uhakika ni wapi pa kushika, kwani Marekani itakuwa upande wa Japan katika suala hilo, hivyo inabidi ianze kutafuta vianzio vingine vya kupata teknolojia hiyo, katika hali ambayo inahatarisha ushirikiano kwa jumla katika ukanda huo.

Marekani, Korea Kusini na Japan zinafanya mazoezi ya kijeshi mara kwa mara; sasa mizozo ya biashara na usalama inahatarisha kuwapo kwa mfungamano.





# DC aagiza uunganishwaji maji ya bomba ya kunywa hotelini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro, ameshauri mamlaka za maji nchini kuunganisha huduma ya maji ya bomba kwenye hoteli ili wageni wanaolala humo wanywe maji hayo badala ya kuwapatia yanayozalishwa viwandani.

Alitoa ushauri huo juzi jijini hapa wakati wa majumuisho ya maonyesho ya wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kuwa inatakiwa uwepo utaratibu wa kuwalazimisha wenye hoteli kuunganishiwa huduma hiyo.

Mtatiro alisema hilo linawezekana kwa sababu limeshafanyika katika baadhi ya mataifa ikiwamo Afrika Kusini na baadhi ya mataifa ya Ulaya na kwamba utaratibu huo utasaidia kuongeza ubora wa maji yanayosambazwa na mamlaka hizo.

Alisema baada ya huduma hiyo kuunganishwa uwekwe utaratibu wa wahudumu wa hoteli kuwaelimisha wageni wanaoingia kupata huduma kwenye hoteli hizo kuwa maji ya bomba yanayopatikana vyumbani ni ya kunywa.

"Ikitokea mtalii akanywa maji ya dukani akadhurika, atakayelaumiwa ni Serikali ya Tanzania, hivyo tuweke utaratibu wa kuweka utaratibu kuwa wenye hoteli wanaochimba maji ya visima yatumike kwa ajili ya kazi za nje, lakini kwa ajili ya kunywa watu wanywe ya bomba," alisema Mtatiro.

Alisema utaratibu huo unaweza ukaanza kwenye hoteli kubwa zenye hadhi ya nyota tano kisha baadaye unaendelea kwenye hoteli za hadhi zingine.

Vilevile aliwapongeza viongozi walioshiriki kuandaa maonyesho hayo kuwa yanavutia na kuna teknolojia mbalimbali ambazo wananchi wanatakiwa wafundishwe na wakazitumie kwenye uzalishaji.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alikosoa baadhi ya teknolojia zinazoonyeshwa na halmashauri pamoja na taasisi mbalimbali kuwa hazina uhalisia na kinachofanywa na wananchi nje ya maonyesho hayo.

Alisema baadhi ya taasisi ikiwamo Benki Kuu ya Tanzania (BoT) zinatumia lugha ngumu ambayo wananchi wa kawaida hawawezi kuielewa vizuri na kwamba hata yeye mwenyewe hazielewi baadhi ya lugha hizo.

Aliwataka kuwafafanulia vizuri wananchi baadhi ya maneno hayo ikiwamo neno 'Bondi' ili kuleta uhalisia wa kile wanachokizungumza na wanachokifahamu wananchi wa kawaida.

"Kwa lugha nyepesi naweza kusema bado kuna maigizo kidogo kwenye maonyesho haya, kuna ng'ombe zimeletwa hapa hazina kabisa uhalisia na mifugo ya wananchi wetu, mmezileta hapa na sisi tukiziangalia tunaona kabisa kuwa ni mbingu na ardhi," alisema Chalamila.

Alisema kwenye maonyesho hayo aliona kuna ng'ombe mwenye uzito wa tani moja, lakini kwenye uhalisia wa ufugaji wa wananchi ni vigumu kukuta ng'ombe wa aina hiyo kutokana na elimu yake kutokuwa halisia.

Aliwataka wataalamu kuhakikisha wanafikisha elimu kwa wananchi ili kile kinachoonyeshwa kiwe na uhalisia kwa kuwa watu wanaojitokeza kwenye maonyesho ni wachache kuliko wanaobaki vijijini.



Mmoja wa maofisa wa Mamlaka ya Hali ya Hewa mkoani Mbeya, akitoa maelezo ya taarifa mbalimbali za hali ya hewa zilizofanyiwa kazi na mamlaka hiyo kwa Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila (kushoto), kwenye maonyesho ya Nanenane, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, mkoani humo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kigogo anaswa akidaiwa kuharibu miundombinu ya maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

OPERESHENI iliyoanzishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Mbeya (Mbeya-WSSA) ya kuwasaka wadaiwa sugu na wahujumu wa miundombinu ya maji, imeanza kuzaa matunda baada ya kumnasa kigogo mmoja akishirikiana na vishoka kuharibu miundombinu.

Kigogo huyo ambaye anaishi katika eneo la Forest Mpya jijini hapa, alinaswa juzi na maofisa wa Mbeya-WSSA, wakishirikiana na Jeshi la Polisi na 'vishoka' (mafundi wa mitaani), aliokuwa anashirikiana nao walitimua mbio na kutokomea kusikojulikana.

Kigogo huyo ambaye jina lake halikuwekwa wazi pamoja na mafundi wake, walikutwa wameng'oa dira ya maji pamoja na miundombinu mingine na kuacha maji yakipotea na kusababisha baadhi ya majirani kukosa huduma hiyo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Patali Shida, alisema hali hiyo inasababisha hasara kubwa kwa mamlaka kutokana na kiwango cha maji yanayopotea kutolipwa na kuwakosesha huduma wateja wengine.

Patali ambaye pia ni Meneja wa Rasilimali Watu wa Mbeya-WSSA, alisema baada ya kuwakuta mafundi hao wakiendelea na shughuli, waliamua kupiga simu polisi na kumkamata mke wa kigogo huyo na kuondoka naye kwa ajili ya mahojiano.

"Huyu ni mteja wetu, hivyo tutakaa naye ili tuone namna ya kumalizana naye, lakini shida yetu kubwa kwa sasa ni hawa mafundi ambao wamekimbia baada ya kutuona, tutahakikisha tunawakamata na tunawachukulia hatua kali," alisema Patali.

Alisema wataendelea na operesheni ya kuwasaka watu wengine wenye tabia ya kucheza na miundombinu ya maji pamoja na wadaiwa sugu ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma nzuri na kwa wakati.

Akitoa ufafanuzi wa tukio hilo, mke wa kigogo huyo alibaye alikataa kutaja jina lake kwa waandishi wa habari, alisema hahusiki na uharibifu huo na badala yake akaeleza kuwa dira iliharibiwa na wanafunzi wanaopita kunywa maji nyumbani kwake wakitoka shuleni.

Alisema baada ya kuona dira hiyo imeharibika mume wake ambaye kwa sasa yupo mkoani Iringa kikazi, aliamua kuiondoa na kuiweka ndani ili isije ikaibiwa na kwamba mafundi waliokutwa aliwaita ili wamtengenezee. Alisema lengo lake ilikuwa sio kuharibu miundombinu kwa makusudi na badala yake alitaka afunge ili maji yasipotee wakati akifanya juhudi za kuwatafuta mafundi wa mamlaka.

"Mita iliondolewa na mume wangu baada ya kuona watoto wameiharibu na inaning'inia, aliitoa kwa sababu aliona itaibiwa na leo ndio amenipa namba za mafundi ili wanitengenezee maji yasiendelee kupotea na mimi sikujua kama ni kosa kuwatumia mafundi hao," alieleza.

Mwanasheria wa Mbeya-WSSA, Sophia Sombe, alisema tukio lililofanywa na mwenye nyumba huyo kwa kushirikiana na mafundi wa mitaani ni kosa la uhujumu uchumi na kwamba endapo watapatikana na hatia watatakiwa kupewa adhabu kali.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka hiyo, Neema Stanton, alisema wataendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na maji ili kuepuka kutenda makosa ya aina hiyo.

# Wenye ulemavu walalamika kukosa uwakilishi

**Na Mwandishi Wetu,** KYELA

KUKOSEKANA kwa wawakilishi wa kutosha wa watu wenye ulemavu katika vyombo vya maamuzi kumeelezwa kuwa chanzo cha serikali kushindwa kutekeleza kikamilifu baadhi ya matamko na sera za watu wenye ulemavu nchini.

Mratibu wa mradi wa Sauti ya watu wenye ulemavu katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Siza Mwahula, wakati wa mafunzo maalumu yaliyoandaliwa na chama cha watu wenye ulemavu wilayani humo yenye lengo la kutambua sera na sheria za wenye ulemavu kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unao tarijiwa kufanyika mwezi Novemba mwaka huu.

Mwahula alisema licha ya serikali kuonyesha jitihada za makusudi za kujali haki ya watu wenye ulemavu, juhudi hizo hazijazaa matunda kutokana na kukosekana kwa wawakilishi kwenye vyombo vya uamuzi kuanzia ngazi za vijiji ambako ndio michakato huanzia.

Alifafanua kuwa katika Halmashauri ya Kyela kuna watu wenye ulemavu 2,122 na kati yao ni 32 pekee waliopo kwenye kamati za huduma za jamii, mazingira, afya na Ukimwi za vijiji.

"Hivyo chama cha watu wenye ulemavu Kyela tunaamini kupitia jukwaa la sauti ya pamoja katika kila kijiji au mtaa, kata itakuwa rahisi kujadili yanayotuhusu na kuwa na ushawishi mkubwa wa utekelezaji wa matamko ya viongozi pamoja na sera," alisema Mwahula.

Mwenyekiti wa chama cha watu wenye ulemavu wilaya ya Kyela, Gwamaka Andembwisye, alisema mradi huo unalenga kutoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu 500 katika kata tano za Wilaya ya Kyela.

Alizitaja kata zinazohusika kuwa ni Ikimba, Kyela mjini, Busale, Matema na Itunge na kwamba lengo ni kuhakikisha wanakuwa na ushiriki mpana kwenye vyombo vya maamuzi kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji/mitaa na kata ili iwe rahisi kuwasilisha ajenda zao.

"Kupitia mradi huu ambao tumefadhiliwa na The foundation for civil society katika kipindi chote cha mradi tunaamini utaenda kuleta mabadiliko makubwa kwenye jamii na kuwa mfano kwa wilaya zingine nchini na baada ya mafunzo tunatarajia kuwa na mkutano wa kimkakati wa kupanga mpango kazi kuhusu changamoto zinazotukabili wakati wa uchaguzi," alisema Andebwisye.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema sababu kubwa ya kukosa uwakilishi kwenye vyombo vya uamuzi ni wananchi kushindwa kuwaamini kutokana na hali zao.

Mmoja wa washiriki hao, Amon Mwambembule kutoka katika Kata ya Matema, alisema aliwahi kujitosa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji cha Kisyosyo na kushindwa kwa kupata kura 20 pekee.



# Jafo akoshwa ukusanyaji mapato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameipongeza Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kuendelea kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani.

Jafo alitoa pongezi hizo wakati alipozungumza na madiwani katika mkutano wa mwaka wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji hilo uliofanyika juzi.

Waziri huyo alibainisha kuwa katika mwaka huu wa fedha, halmashauri hiyo imekusanya Sh. bilioni 71.

Alisema kutokana na jiji hilo kuendelea kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, madiwani wanatakiwa kuendeleza mshikamano uliopo baina yao na wakuu wa idara katika kusimamia mapato hayo.

"Kukusanya kwenu mapato haya kiasi cha Sh. bilioni 71 kunatokana na mshikamano uliopo baina ya mstahiki meya, mkurugenzi, madiwani lakini pamoja na wakuu wa idara ambao wamekuwa ndiyo watendaji katika kuleta tija hii ya ukusanyaji wa mapato," Jafo alisifu.

Alisema mapato yaliyokusanywa na halmashauri hiyo ni makubwa na yanatosha kuhudumia halmashauri zingine mbili.

"Kwa hiki mlichokusanya, niwaambie waheshimiwa madiwani kuwa kuna baadhi ya halmashauri mapato yao ya ndani ni kidogo sana.

"Kwa haya ya kwenu mnaweza kuzihudumia hata halmashauri nyingine mbili ambazo matumizi yao ni kiasi cha Sh. bilioni 30 kwa mwaka," alisema.

Jafo aliwataka madiwani hao kuacha tabia ya kutengana au kunyanyapaana bali washikamane na kuwa kitu kimoja katika kuleta maendeleo ndani ya jiji hilo.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema wametenga Sh. bilioni nane kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zilizoko katika sekta ya elimu ya msingi na sekondari.

"Kiasi hiki cha fedha kitasaidia kuondoa tatizo lililopo la uhaba wa madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo katika shule mbalimbali za msingi na sekondari," alisema.

Kunambi alisema halmashari hiyo pia ina mpango wa kujenga shule nyingine nne na kituo kimoja cha afya kitakachogharimu Sh. milioni 600.

Katika mkutano huo, madiwani walimchagua Diwani wa Kata ya Matumbulu, Emannuel Chibago (CCM), kuwa naibu meya kwa kura 52 dhidi ya mpinzani wake kutoka Chadema, Said Kitegile, ambaye ni Diwani wa Kata ya Madukani.




Naibu Meya mpya wa Jiji la Dodoma, Emanuel Chibago wa CCM (kushoto), akipongezwa na mpinzani wake Saidi Kitegile kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi uliofanyika jijini humo juzi, ambapo Chibago alishinda kwa kura 52 dhidi ya 5 za Kitegile. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Magereza waita wakulima shamba darasa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza limewaita wananchi kujitokeza katika kujifunza kilimo na ufugaji kutoka kwa wataalamu waliobobea katika sekta hiyo kupitia shamba darasa la jeshi hilo.

Shamba hilo liko katika Viwanja vya Maonyesho ya Nanenane Nzuguni jijini Dodoma.

Kamishna Msaidizi wa Magereza, Kenneth Mwandige, alisema jeshi hilo liko kwa ajili ya urekebishaji tabia na linatumia wataalamu kuwafundisha wafungwa kilimo, ufugaji na fani za ujenzi ili wakimaliza kifungo, waendeleze fani hizo wakiwa uraiani. "Naomba wananchi husani wakazi wa Dodoma wajitokeze kupata elimu ya kilimo na ufugaji kutoka kwa wataalamu wa jeshi hilo, watapata siri kubwa ya mafanikio kwenye kilimo na ufugaji," Mwandige.

Alisema kilimo na ufugaji ni utajiri mkubwa kama utaendeshwa kupitia elimu ya wataalamu wa sekta hiyo kwa kuzalisha mazao yenye tija.

Alisema wananchi watembelee shamba darasa hilo ili kupata mafunzo ya kuzalisha mbegu bora kwenye kilimo na ufugaji ambazo watakwenda kutumia katika mashamba yao na kuona manufaa yake wakati wa mavuno.

Rehema Mhelela, ofisa wa jeshi hilo, alisema Jeshi la Magereza limekuwa mstari wa mbele katika utoaji mafunzo ili wafungwa wawe na mtazamo chanya kiuchumi.

# Waomba kujengwa kiwanda cha 'soli' viatu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAJASIRIAMALI jijini Dodoma wameiomba serikali kuanzisha kiwanda cha kuzalisha vifaa vya soli ya viatu vya ngozi ili kuwarahisishia utengenezaji wa bidhaa hizo katika maeneo mbalimbali nchini.

Wajasiriamali wanaoshiriki katika maonyesho ya 26 ya Nanenane kwenye Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma walitoa rai hiyo jana walipozungumza na Nipashe.

Akizungunza kwa niaba ya wenzake, Makseline Wandimango, alisema serikali inapaswa kuanzisha au kushawishi wawekezaji kuanzisha kiwanda cha soli walau kimoja kila kanda, akiamini uamuzi huo utawasaidia wajasiriamali kuongeza uzalishaji wa viatu vya ngozi nchini.

Wandimango alisema upatikanaji wa soli za viatu umekuwa ni changamoto kubwa kwa wajasiriamali wa bidhaa za ngozi kwa sababu zinapatikana nje ya nchi.

Alisema kwa sasa wao wanaziagiza kutoka China na Kenya lakini changamoto kubwa ni gharama za uagizaji.

"Soli za viatu ni changamoto kubwa sana kwa wajasiriamali wa bidhaa za ngozi, inachangia ucheleweshaji wa uzalishaji wa viatu vya aina hiyo," alisema.

Alisema viatu vya ngozi vina soko kubwa nchini kutokana na jamii kuvihitaji hasa kwa wanafunzi na watu wengine wanaopenda kuvaa viatu vya aina hiyo.

Ofisa Uendelezaji Biashara wa Shirika la Viwanda Vidogo (Sido) mkoani Dodoma, Crispin Kapinga, alisema Sido iko katika maonyesho hayo kwa ajili ya kuielimisha jinsi ya kuongeza thamani katika bidhaa mbalimbali vikiwamo viatu vya ngozi.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Mifugo, uhitaji wa viatu vya ngozi nchini ni jozi milioni 40, lakini zinazozalishwa ni jozi 600,000 kwa wajasiriamali wadogo na kwa wakubwa 700,000.

"Watanzania wanahitaji kuvaa viatu vizuri, lakini kiatu hicho siyo lazima kitoke Italia, hata Tanzania tunaweza kama viwanda vya soli za viatu vitaanzishwa nchini," Kapinga alisema.





# Wanafunzi wa kike wapongezwa ufaulu mzuri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed, amewapongeza wanafunzi wa kike katika mkoa huo kuwa vinara katika ufaulu wa mitihani yao ya taifa ikilinganishwa na wavulana.

Alisema wasichana wanabidii ya kusoma na kufuatilia masomo yao ikilinganishwa na wanafunzi wa kiume ambao wengi wao ni watoro wa shule.

Akizungumza na Kamati ya Elimu ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, ambayo ilifika ofisini kwake Vuga kuwasilisha ripoti ya matokeo ya majaribio kwa wanafunzi wa kidato cha nne ambayo ufaulu wa wanafunzi wa kike upo juu zaidi kuliko wavulana.

Ayoub alisema hata katika matokeo ya kidato cha sita yaliyotolewa na Baraza la Mitihani Tanzania hivi karibuni ufaulu wa wanafunzi wa kike ni mzuri zaidi.

"Wanafunzi wa kiume kama hamtojitahidi kusoma miaka ijayo nafasi zote za uongozi zitashikiliwa na wanawake maana taifa litakuwa na wataalamu wa kike pekee," alisema Ayoub.

+Ayoub alisema sasa anatangaza vita kwa wanafunzi watoro na katika shule zilizomo katika mkoa wake utoro umekithiri zaidi kwa wanafunzi wa kiume.

"Sasa tunataka kupambana na wanafunzi watoro pamoja na wazazi na walezi wasiowajibika kwa watoto wao kuhudhuria shule ili kuondoa tatizo la utoro," alisema.

Alisema katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha nne, hataki kuona mkoa wake kuna shule zilizoshika mkia na kufanya vibaya katika mitihani hiyo.

Aliwaagiza walimu wakuu wote wa shule za serikali na binafsi ambao shule zao zimeshika nafasi za mwisho katika mitihani ya majaribio ya kidato cha nne iliyofanyika mwezi uliopita, kuandika barua ya kueleza sababu za kufanya vibaya shule zao ili ziweze kufutiwa ufumbuzi kabla ya mitihani ya mwisho ya taifa.

Alisema lengo la mkoa ni kuona shule zote zinafanya vizuri katika mitihani yao na kuitaka kamati hiyo ya elimu kuandaa mikakati maalumu ya kuinua ufaulu katika shule zilizokuwa hazijafanya vizuri katika mitihani ya majaribio ili kuongeza ufaulu katika mitihani ya mwisho ya taifa. Akiwasilisha taarifa ya matokeo ya majaribio ya mitihani ya kidato cha nne, Mwenyekiti wa mitihani hiyo, Mussa Hassan Mussa, alisema licha ya changamoto mbalimbali kujitokeza katika mitihani hiyo, ufaulu kwa mwaka huu umeongeza kwa asilimia 65.42 na kwa mwaka jana kulikuwa asilimia 63.20.

Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Mabrok Jabu Makame, aliwataka wanafunzi waliofanya vizuri kwenye mitihani hiyo ya majaribio kuwa na jitihada zaidi na waliofeli kutumia muda huu kufanya bidii ya kusoma ili kuongeza ufaulu katika mitihani ya taifa.

# Vijana wafurahia kuendelezwa kwenye kilimo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIJANA kutoka maeneo mbalimbali ya Zanzibar wamempongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuwaendeleza katika sekta ya kilimo ili kuwaongezea kipato na kuimarisha uchumi wa nchi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Langoni Wilaya ya Magharibi "A" Unguja katika Maonyesho ya Nanenane, vijana hao walieleza jinsi kilimo kilivyowasaidia kuimarisha uchumi.

Katika maelezo yao vijana hao walikiri kuwa sekta ya kilimo ina umuhimu mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi na iwapo serikali itaazimia kuipa kipaumbele kwa kuwasaidia vijana katika kutekeleza azma hiyo, mafanikio zaidi yatapatikana.

Walisema kuwa kuwapo kwa maonyesho hayo kutawasaidia kwa kiasi kikubwa vijana kuhakikisha ndoto zao zinafikiwa kutokana na elimu kubwa watakayoipata katika maonyesho hayo na elimu itakayotolewa katika vyuo vikuu kikiwamo Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Pascal Mkude, mkazi wa Kiboje ni miongoni mwa vijana hao alisema kuwa azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Shein ya kuwaendeleza kwa kuwapatia mafunzo ya elimu ya juu na kuongeza wataalamu katika sekta ya kilimo ni ya kupongezwa.

Alisema sekta ya kilimo aghalabu inaendana na elimu ya kutosha kwa vijana hasa ya chuo kikuu katika kuendeleza sekta hiyo itakuwa chachu kufikia malengo yao waliyoyaweka.

"Sekta ya kilimo imejaliwa kuwa na fursa nyingi za ajira, hivyo azma ya serikali ya kuimarisha sekta hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kukamilisha ndoto zetu," alisema.

Pia alisifu hatua ya serikali ya kuwaza kufanya maonyesho hayo ambayo yanafaida kubwa hasa kwa vijana ambao wanajishughulisha na kilimo na wale ambao wana lengo la kujiingiza katika sekta hiyo.

Naye Amina Machano, mkazi wa Donge Pwani, alieleza kuwa maonyesho hayo yatawasaidia kinamama hasa wale walioanzisha vikundi vya kilimo kwa kuwa watapata fursa kubwa ya elimu pamoja na kujionea wenyewe utaalamu katika sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji.

Kwa upande wake Juma Haji, mkazi wa Umbuji alieleza kuwa sekta ya kilimo ndio pekee inayoweza kumkomboa mnyonge, hivyo azma ya Dk. Shein kuipa kipaumbele itawasaidia wananchi wa hali zote za maisha wakiwamo maskini.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene (katikati), akizungumza na watendaji kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, alipotembelea mradi wa upandaji mikokoko katika Shehia ya Kilimani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Magharibi, juzi. **PICHA: OMR**

# Balozi Iddi aeleza umuhimu wa Muungano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema upo wajibu na jukumu kubwa la kuwaelimishwa viongozi kutambua umuhimu wa dhana halisi ya uwezo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ili kuelewa kwa kina dhana ya uwapo wake.

Alisema baadhi ya viongozi wanaoingia katika madaraka wakiwa bado hawajaelewa historia ya muda mrefu iliyowaunganisha kidamu wananchi wa pande mbili za Muungano.

Alisema hayo ofisini kwake Vuga wakati akizungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayesimamia Muungano na Mazingira, George Simbachawene, aliyefika kujitambulisha baada ya kuteuliwa hivi karibuni kushika wadhifa huo.

Alisema kazi kubwa inayokabili Watanzania kwa wakati huu ni kuendelea kuuimarisha Muungano huo ulioleta faida kubwa kiuchumi na ustawi wa jamii, faida ambayo inaweza kuwa funzo zuri la kuigwa na mataifa mengine ulimwenguni.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais inayosimamia Muungano, kuona umoja na mshikamano uliojengeka kupitia Muungano huo unaimarika na kustawi kwa maslahi ya wananchi wote. Balozi Iddi alimshauri waziri huyo kwamba anapohisi yapo mambo yanayoashiria kukwama katika kupeleka mbele masuala ya Muungano asione uzito kuyatolea taarifa kwa viongozi wake wakati wowote.

Naye Simbachawene alisema Muungano wa Tanganyika na Zanzibar una shabaha maalum iliyofanya waasisi wa taifa kufikia uamuzi wa kuunganisha mataifa mawili yaliyo huru.

"Wakati umefika sasa kwa kizazi kipya kilichozaliwa ndani ya karne ya 21 kinapaswa kuelewa dhamira hasa ya waasisi hao ambao wengi kati yao wamebahatika kusoma historia ya Muungano ndani ya vitabu," alisema Simbachawene.

Vile vile, alisema wapo baadhi ya watu wakiwamo viongozi wamepitia kujua mfumo wa utawala katika madaraka waliyokabidhiwa wakati wanapokuwa kwenye utumishi wa umma.

# Viongozi 102 wa ushirika watumbuliwa

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

WAKATI serikali ikiagiza viongozi wote wa vyama vya ushirika walioshiriki katika ubadhirifu wachukuliwe hatua, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imewaondoa madarakani viongozi 102 wa vyama vya ushirika katika Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu baada ya kubainika kufanya ubadhirifu katika msimu wa kilimo cha pamba. Akizungumza katika maonyesho ya kilimo yanayoendelea mkoani Simiyu, Naibu Mrajisi Uhamasishaji, Charles Malunde, alisema viongozi hao walibainika baada ya ukaguzi uliofanywa na serikali katika vyama hivyo, na kwamba baada ya kuondolewa watafikishwa mahakamani.

Alisema kuwa hatua hiyo inatokana na Tume ya Ushirika kuanza kuvitazama upya vyama vya ushirika pamoja na kuhamasisha vyama vya ushirika nchini kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na kuleta tija kwa wanaushirika na jamii kwa ujumla. Naibu Mrajisi huyo alisema mpaka sasa kuna jumla ya vyama vya ushirika 11,331 vyenye idadi ya wanachama 4,611,804, huku wanachama tarajiwa 765,804, hivyo wameamua kuhamasisha ili kuongeza uzalishaji kupitia sekta ya kilimo. Naye Kaimu Mrajisi Msaidizi wa Mkoa wa Simiyu, Ibrahim Kadudu, alisema Tume ya Ushirika imeendelea kuwajengea uwezo viongozi wa vyama vya ushirika katika Mkoa wa Simiyu, ili kusimamia kilimo hicho cha pamba kiweze kuleta manufaa kwa wakulima kutokana na mkoa huo kulima zao hilo kwa wingi.

Alisema baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika wamekuwa wakishindwa kwenda na mabadiliko ya sasa ya serikali ya sasa na kuendeleza ubadhirifu, lakini sasa wameanza kudhibitiwa ikiwamo wa Wilaya ya Maswa ambao wameondolewa katika uongozi na watafikishwa mahakamani.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliagiza Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuendelea kusimamia vyama vya ushirika kwa kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara kwa kuwashirikisha wakaguzi wa vyama vya ushirika (COASCO) ili kuwadhibiti viongozi hao wanaofanya ubadhirifu.

Waziri huyo aligiza tume hiyo kuhamasisha wananchi kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika katika sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo pamoja na kutoa elimu kwa viongozi watendaji na wanachama wa vyama kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya ushirika.



Rais John Magufuli akipata maelezo kutoka kwa Meneja Operesheni wa Kampuni ya Mafuta ya Puma Energy Tanzania, Lamecky Hiliyai, alipotembelea banda la kampuni hiyo, baada ya kuzindua Maonyesho ya nne ya Wiki ya Viwanda ya SADC, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Meneja Sheria na Uhusiano wa kampuni hiyo, Godluck Shirima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Mwanri aamuru kamatakamata

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amewaagiza viongozi kuwachukulia hatua kali watu wote wanaoharibu mazingira kwa kuchoma moto maeneo yaliozuiliwa na serikali, na kwamba wawakamate mara moja.

Mwanri alitoa agizo hilo jana katika ufunguzi wa Maonyesho ya Wakulima Nanenane Kanda ya Magharibi yaliofanyika kwenye viwanja vya Ipuli.

Mwanri alisema viongozi wote mkoani hapa wakague maeneo yote ambayo yameharibiwa na kuhakikisha wanakamatwa na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola.

Aidha, aliagiza kuwa baada ya kufanya zoezi hilo, wahamasishe wananchi kutunza mazingira ili kuongeza thamani ya mkoa wa Tabora na wilaya zake.

Mwanri alisema viongozi hao kuhakikishe wanakagua mabanda yote ya wajasiriamali na kuwadhibiti wanaonunua mazao sokoni na kuyapeleka kwenye mabanda ya maonyesho.

"Wajasiriamali feki wanaopeleka mazao kwenye viwanja vya maonyesho ya Nanenane wakamatwe," alisema Mwanri.

Aliwataka wananchi kutunza chakula cha ziada ili waweze kuwa na maisha bora, kuwasomesha watoto wao vizuri ili wawe na afya bora.

Msimamizi wa masoko wa Chama cha Ushirika wa Tumbaku Kanda ya Magharibi (Wetcu), Alawi Sharifu, alilalamikia changamoto zinazowakabili katika sekta ya kilimo na mifugo kuwa ni uhaba wa maji ya kunywesha mifugo.

Alisema changamoto zingine ni ukosefu wa mbegu bora za mifugo, kutotengwa maeneo maalumu kwa ajili ya malisho na kupelekea kuongezeka kwa migogoro kati ya wakulima na wafugaji, na wakati mwingine na hata serikali.

Alisema katika sekta ya kilimo ni bei ya pembejeo kama mbolea, dawa mashambani, pembejeo zisiokuwa na ubora na mabadiliko ya hali ya hewa.

# Wakulima watakiwa kujiunga na ushirika

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

KAIMU Mrajisi wa Vyama vya Ushirika mkoani Rukwa, Anosisye John, amewashauri wakulima mkoani humo kujiunga na vyama vya ushirika kwa kuwa serikali imepania kuvijengea uwezo vyama hivyo baada ya kuamua kununua tani 8,000 za mahindi kupitia Chama Kikuu cha Ushirika cha Ufipa Cooperative Union.

Kauli hiyo aliitoa juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari, baada ya serikali ya mkoa huo kutangaza kuwa imepanga kununua tani 8,000 za mahindi kupitia vyama vya ushirika na kununua tani 5,000 za mahindi kwa mtu mmoja mmoja.

Alisema kuwa uamuzi huo unatoa fursa kwa wakulima waliojiunga na vyama hivyo kwani watanufaika kwa kuuza mahindi yao kwa urahisi tofauti na wale wasiokuwa katika ushirika kwa kuwa watapata tabu kutokana na mahindi yatakayonunuliwa kwao yatakuwa machache.

John alisema hiyo ni njia nzuri ambayo serikali imeamua kwa sababu itakuwa inavijengea nguvu ya kiuchumi vyama hivyo kwa kuwa msimu uliopita wakulima kupitia vyama hivyo waliuza mahindi yenye thamani ya Sh. bilioni 2.8.

Alisema sambamba na hilo, serikali haitakutana na changamoto kubwa katika ukusanyaji wa kodi kwa kuwa ni rahisi kupatikana kwa fedha hizo kwa kuwa watalipa kodi kupitia vyama vyao.

Mrajis huyo alisema Ufipa Co-operative Union inaundwa na vyama vingine vidogo vipatavyo 58 ambavyo vinawanachama wengi ambao pia wanatengeneza soko kubwa, ndiyo maana serikali imeamua kununua mahindi kupitia vyama hivyo.

Mkuu wa Mkoa huo, Joachim Wangabo, aliwaasa wakulima kuhakikisha wanatunza vizuri fedha watakazopata baada ya kuuza mazao yao ikiwamo kufungua akaunti benki na kuzihifadhi ili ziwasaidie

## HABARI KIMATAIFA

# Nusu ya raia wa Burundi wanaumwa malaria

**BUJUMBURA, Burundi**

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema homa ya malaria imeua zaidi ya watu 1,800 nchini Burundi mwaka huu, idadi inayokaribiana na waliokufa kwa ugonjwa wa ebola nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Katika ripoti yake ya hivi karibuni, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu (OCHA) imesema matukio milioni 5.7 ya ugonjwa wa malaria yalirekodiwa nchini Burundi mwaka 2019, idadi hiyo ni sawa na nusu ya watu wote wanaoishi nchini Burundi.

Nchi hiyo ndogo katika ukanda wa Maziwa Makuu barani Afrika ina jumla ya watu milioni 11 na bado mpaka sasa haijatangaza dharura ya kitaifa, licha ya shirika la OCHA Mei, mwaka huu kusema kwamba kuzuka kwa mripuko wa ugonjwa wa malaria ni janga.

Kwa mujibu wa OCHA katika taarifa yake ya hivi karibuni kuhusu dharura ya kibinaadamu, ilieleza kuwa mpango wa kitaifa wa kuudhibiti ugonjwa wa malaria ambao kwa sasa umeanzishwa, umeonyesha kukosa rasilimali watu, vifaa na fedha kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa Shirika hilo limewataka wadau wote, pamoja na mamlaka ya kitaifa na washirika kuchangia rasilimali zinazohitajika kupambana na malaria kabla ya matukio zaidi kuongezeka.

***DW***



## Email zilizovuja zamweka mashakani Ramaphosa

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa (pichani) amesisitiza kuwa hana kosa lolote baada ya kuvuja kwa barua pepe kuhusu mchango aliopokea wakati wa kampeni ndani ya chama cha ANC mwaka 2017.

Mwishoni mwa Julai, Rais Cyril Ramaphosa alisema ataenda mahakamani kupinga ripoti ya ofisi ya msimamizi wa mali za umma ambayo ilimtaja kudanganya bunge kuhusu kupokea fedha za michango kusaidia kampeni yake mwaka 2017.

Kwenye ripoti hiyo Rais Ramaphosa anadaiwa kupokea kiasi cha randi laki tano kusaidia kampeni zake kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

Tayari mkurugenzi wa ofisi ya usimamizi wa mali za umma, Busisiwe Mkhwebane ametoa taarifa akiunga mkono hatua iliyochukuliwa na Rais Cyril Ramaphosa.

Awali Rais Ramaphosa alisema baada ya kuisoma kwa kina alibaini kuwa ripoti hiyo ina makosa na tuhuma za kupikwa na kutaka mara moja ifanyiwe mapitio na mahakama za nchi hiyo.



Wanajeshi wa India wakifanya doria kwenye mitaa ya Jimbo la Kashmir. **PICHA: REUTERS**

# Bobi Wine ashtakiwa kwa kumkasirisha Rais Museveni

**KAMPALA, Uganda**

MBUNGE wa Uganda na mwanamuziki, Bobi Wine, ameshtakiwa kwa lengo la kumkasirisha, na kumkejeli Rais wa nchi hiyo, Yoweri Museveni.

Mbunge huyo na wenzake wametuhumiwa kwa kuurushia mawe msafara wa Rais Museveni wakati wa mkutano wa kampeni za uchaguzi katika mji wa kaskazini wa Arua mwaka 2018.

Shtaka hilo jipya limeongezwa katika shtaka lingine la uhaini dhidi ya mbunge huyo. Iwapo atapatikana na hatia Wine atakabiliwa na kifungo cha maisha jela.

Hata hivyo, Wine ambaye jina lake ni Robert Kyagulani bado anakabiliwa na mashtaka katika mahakama nyingine kwa kuongoza maandamano dhidi ya sheria inayoweka kodi katika mitandao ya kijamii pamoja na biashara zinazofanywa kupitia malipo ya simu mwaka 2018.

Msanii huyo ambaye amekuwa mwanasiasa wa upinzani anayepinga utawala wa miongo mitatu ya Rais Museveni hivi majuzi alitangaza kwamba atawania urais katika uchaguzi wa 2021.

Tayari Wine amezindua kikosi kitakachoendesha kampeni yake ya kuwania urais mwaka 2021.

Umaarufu wake miongoni mwa vijana nchini Uganda unaonekana kama changamoto kwa Rais Museveni.

Rais Museveni, mwenye umri wa miaka 74, anatarajiwa kuwania muhula wa sita madarakani.

Msanii huyo anakabiliwa na mashtaka ya uhaini baada ya kukamatwa mwaka jana kufuatia kuushambulia kwa mawe msafara wa rais baada ya mkutano wa kisiasa.

Aliliambia gazeti la Financial Times kwamba zaidi ya wabunge 50 wakiwamo 13 kutoka kwa chama tawala cha Rais Museveni cha National Resistant Movement (NRM) waliunga mkono ugombeaji wake na hivyo kumpatia ujasiri wa kugombea kiti hicho.

Mchambuzi wa kisiasa nchini Uganda, Nicholas Sengoba alisema uchaguzi mdogo wa Aruaulioshindwa na mgombea aliyeungwa mkono na Wine ulikuwa ni wa kufa au kupona kwa Rais Museveni.

"Chama chake kitaweza iwapo kitakuwa na wafuasi wengi, Bobi Wine sasa amemshinda Rais Museveni na kiongozi wa upinzani Kizza Besigye mara nne' katika uchaguzi mdogo" alisema Sengoba na kuongeza:

"Bobi amepata ufuasi kwa nembo yake ya nguvu za watu, na ananuia kushinikiza na kupanga liwe vuguvugu".

Mchambuzi mwingine wa siasa, Robert Kirunda alisema mvuto wa Wines unatokana na kuwapo pengo la uongozi nchini Uganda.

"Kuna vijana wengi Uganda ambao hawana haja ya kujua vita vya kihistoria vilivyoingiza NRM uongozini, au ukaidi wa upinzani mkuu. Wengi wanataka ajira na wanahisi uchumi hauwasaidii," alisema Kirunda.

Kirunda alisema Wine anapigia upatu sana na anaweza kushinikiza watu pakubwa, lakini bado hajapata nguvu kama alizonazo Besigye katika upinzani.

***BBC***

# Askofu aomba korti Kuu kusikiliza ombi lake

Na Hellen Mwango

ASKOFU Mulilege Kameka wa Kanisa la House of Prayers Shieldof Faith Christian Fellowship, ameiomba Mahakama Kuu kanda ya Dar es Salaam, kutupilia mbali pingamizi la awali dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) la kutaka maombi ya askofu huyo yasisikilizwe.

Akiwasilisha pingamizi la AG, mawakili wa serikali Jacqline Nyanyori na Tuli Helela walidai kwa nyakati tofauti mlalamikaji amewasilisha maombi yake chini ya kifungu ambacho hakiipi mahakama hiyo mamlaka ya kuyasikiliza.

Pingamizi hilo lilisikilizwa jana mbele ya Jaji Dk. Atuganile Ngwala.

Kwamujibu wa hati ya maombi hayo, mlalamikaji ameegemea kifungu cha 392 (A), na 114 A (b), wakidai kwamba kifungu cha 114 kinatengeneza kosa la jinai.

Hata hivyo, mlalamikaji alipaswa kufuata matakwa ya kifungu cha tisa cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), ikiwamo kulalamika rasmi polisi au mahakamani ili itengenezwe hati ya mashtaka na mashahidi wangeitwa kuthibitisha kosa hilo.

"Mtukufu jaji tunaomba maombi haya yafutwe kwa kuwa hayana mashiko ya kisheria," alidai Nyantori.

Askofu huyo kupitia kwa wakili wake John Malya, amewasilisha mahakamani hapo maombi ya kutaka Kamishna Mkuu wa Magereza kwenda kujieleza kwanini asifungwe kwa kukiuka amri halali ya mahakama ya kumwachia huru askofu huyo.

Askofu huyo aliyekuwa akituhumiwa kwamba si raia wa Tanzània, yupo mahabusu katika Gereza la Segerea.

Awali, mahakama iliyoketi Machi 8, mwaka huu, iliamuru kuwa askofu huyo ni raia halali wa Tanzania ambaye ni mzaliwa wa kijiji cha Maenje wilayani Mbozi mkoani Songwe.

Mahakama hiyo iliagiza askofu huyo atolewe mahabusu ndani ya siku mbili na mwenye pingamizi afuate taratibu za kisheria. Hata hivyo Machi 19, mwaka huu, saa 4 asubuhi, baadhi ya wafuasi wa askofu huyo walifika Segerea na hati ya kutolewa kwake, lakini mkuu wa gereza alikataa kwa madai kuwa alipokea amri kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya kutomwachia askofu huyo.

Kwamba, wafuasi hao walirudi kwa Msajili wa Mahakama hiyo kumweleza kuhusu suala hilo na ndipo wakafungua maombi hayo.

# Waziri asitisha operesheni kuchoma nyumba, mazizi

Na Mwandishi Maalum, BABATI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesitisha operesheni ya kuwaondoa na kuwachomea nyumba, mazizi ya mifugo na kambi za uvuvi wananchi wa Kijiji cha Vilimavitatu wilayani Babati mkoani Manyara.

Vilevile, waziri huyo pia ameunda timu ya wataalamu kutoka wizara nane kufuatilia utekelezaji wa operesheni hiyo na kuwasilisha ripoti hiyo serikalini kwa uamuzi zaidi.

Operesheni hiyo ilianza Julai mwaka huu imesababisha wananchi wengi kukosa mahali pa kuishi kutokana na nyumba zao kuchomwa moto na sasa wanaishi chini ya miti. Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Vilimavitatu na kuhudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, baadhi ya wananchi waliangua vilio mbele ya Waziri Mpina wakionesha masikitiko yao kuhusiana na unyama waliofanyiwa na serikali ya wilaya hiyo na kumuomba kuwasaidia.

Walisema mbali na madhara hayo, wanakabiliwa na uhaba wa chakula kutokana na kuchomwa kwa akiba ya chakula waliyokuwa nayo majumbani mwao.

Katika mkutano huo, Waziri Mpina alihoji iweje operesheni hiyo ifanyike huku kukiwa na katazo la Rais John Magufuli la Januari 15, mwaka huu la kusitisha operesheni zote za kuwaondoa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yanayodaiwa kuwa ni hifadhi hadi hapo itakapoamuliwa vinginevyo.

Waziri Mpina pia ahoji sababu za operesheni hiyo kufanyika kwenye eneo hilo huku kukiwa na Hukumu ya Mahakama iliyoliondoa eneo la Kijiji cha Vilimavitatu kwenye Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyapori Burunge (Juhibu).

Waziri Mpina pia alihoji sababu za kuondoa mifugo bila kushirikisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi kama sheria, kanuni na miongozo inavyoelekeza.

Kwa msingi huo, Waziri Mpina alisema operesheni imefanyika kinyume cha Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Namba 17 ya mwaka 2003, Sheria ya Ustawi wa Wanyama Namba 19 ya mwaka 2008, Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Chakula cha Mifugo namba 13 ya mwaka 2010 na Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003.

Alisema wote waliohusika kufanya operesheni hiyo walipaswa kukamatwa na kushtakiwa kutokana na makosa ya kuvunja sheria hizo za mifugo kwa kuwa wanalo jukumu la kuzisimamia ili zisivunjwe.

Waziri Mpina alieleza kasoro nyingine za operesheni hiyo kuwa pamoja na kutokufanya tathmini ya kina ya idadi ya wananchi, kaya, mifugo na mali zingine kabla ya operesheni kufanyika, kukosekana kwa nyaraka muhimu za kuendesha operesheni na uhusiano dhaifu baina ya wafugaji, Juhibu na Mwekezaji Kampuni ya Chemchem Lorge ya Ufaransa.

Mkuu wa Wilaya ya Babati (Kitundu) alisema operesheni hiyo ilifanyika baada ya kudaiwa kuwapo viashiria vya uvunjifu wa amani katika maeneo hayo na kukiri kupokea maelekezo kutoka mkoani.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, (kushoto) akiteta jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Stanbic Tanzania, Ken Cockerill, wakati wa hafla ya uzinduzi wa kampeni ya "I Go Tanzania' ambayo inatoa punguzo la bei na ofa mbalimbali kwa wamiliki wa kadi za benki ya ICBC watakaotembelea Tanzania. Kampeni hii inalenga kukuza sekta ya utalii na kuongeza idadi ya watalii kutoka China kuja Tanzania. **MPIGAPICHA WETU**

# Mtanzania miongoni wanawake 100 wenye ushawishi Afrika

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP), Joyce Msuya, ametajwa kuwa miongoni mwa wanawake 100 wenye ushawishi mkubwa Afrika.

Orodha iliyotolewa na Shirika la Habari la Avance Media, lilimtaja Joyce kama mwanamke mwenye ushawishi mkubwa kwa wanawake wa kizazi kijacho barani Afrika.

Akizungumza kuhusu orodha hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Avance Media, Prince Akpah, alisema orodha hiyo inajumuisha wanawake 100 kutoka nchi 35 barani Afrika ambao wameonyesha mchango



mkubwa katika kuwabadilisha wanawake kimtazamo.

Kadhalika alieleza kuwa miongoni mwao wamejitolea kuwapa uwezo vijana wa kike sehemu mbalimbali barani Afrika kupitia programu za mtoto wa kike ambazo zimeleta mrejesho chanya.

Katika orodha hiyo wapo viongozi mbalimbali kama vile marais, mawaziri wakuu, makatibu wakuu, wake wa marais, magavana, mawaziri, maofisa watendaji wakuu na makamishna.

Miongoni mwao yupo Rais wa Ethiopia, Sahle-Work Zewde, Makamu wa Rais Liberia, Jewel Taylor, Waziri Mkuu wa Namibia, Dk. Saara Kuugongelwa-Amadhila, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Amina J. Mohammed, Rais wa zamani wa Libeia, Ellen Sirleaf Johnson.

Orodha hiyo pia imewataja wanaharakati wanawake vijana akiwamo Aya Chebbi, Farida Bemba Nabourema na Ilwad Elman.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**ANAHITAJIKA MHASIBU SIFA:** MWANAMKE ELIMU: DIPLOMA MAWASILIANO: 0715 885533 / 0752 610700.

## MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA KISEMVULE:** malipo awamu mbili muda wa mwezi mmoja, urefu futi 50 kwa upana futi 40, bei Sh.1,700,000/= tu simu 0623528465/0752737534.

**WACHIMBAJI VISIMA-** Master Drilling:Tunachimba Visima virefu / vifupi mikoa ya Dodoma/Singida/ Arusha/Manyara tunatumia mashine kubwa za kisasa simu:0788767141.

**Wachimbaji Visima** visima Tanzania tunachimba Visima virefu na vifupi kwa gharama nafuu na ofa ya pampu ya bure, simu:0623528465/0713256904.

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

## KUPOTEA KWA KADI

**Zahoro Said Iddi** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajilia wanamba **T132 DMH** aina ya MITSUBISH CANTER, yenye chasis namba **FE538B502168,** Engine namba **4D33Z572HL.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi .

Polisi Taarifa: **DAR/RB/187623/2019**

215364502

## KUPOTEA KWA KADI

**Medard Daudi Mwijage** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T613 AFE** aina ya **NISAN J85,** Yenye chasis namba EO15919.

Yeyote atakaeiona atoe taatifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **ILA/TR/RB/105401/2019**

215364302

## KUPOTEA KWA CHETI



**John E. Mganga** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0369-090** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 1990 katika shule ya Sekondari Ruvu .

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi**

**Polisi Taarifa: DAR/CHA/RB/187119/2019.**

215363102

## KUPOTEA KWA CHETI




**Jumeo Abuu Mapande** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0445/0041** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2008 katika shule ya Sekondari Mwembetogwa**.**

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi**

**Polisi Taarifa: DAR/CHA/RB/176293/2019**

215363302

## KUPOTEA KWA CHETI



**Tumaini Geofrey Mgaya** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.3467/0076** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Mbeyela

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi**

**Polisi Taarifa: NJ/3668/2019**

215362802

## SALES PROMOTION

A Printing company invites youth invites aged 20 -30 to serve as freelancer in Marketing.

**Education:**
Diploma in Marketing.

**Apply to:**
Havila Distributors Ltd

Email:**haviladic16@gmail.com**

**Deadline: 30/08/2019**

215364402

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**TABILIUS ANDREW MLWANDE** Anatangaza kuunguliwa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC685 BUF KING LION** Injini namba **KL.162 FMJ17J O 3037** Taarifa yoyote itolewe kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **IR/TR/RB/5965/2018**

215364702

## KUPOTEA KWA CHETI



**Makweba M. Makweba** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0989.0057** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2016 katika shule Sekondari Kibara .

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi**

**Polisi Taarifa: KBR/RB/464/2018**

215362702

## KUPOTEA KWA KADI

**Annamaria Fredrick Mshote** anatangaza kupotea kwa kadi yenye usajili wa namba **T 691 DGF ya** gari aina ya TOYOTA PREMIO, yenye chasis namba **ZZT2400132637** ingine namba **IZZ2810516**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/190231/2019**

215363002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**

**SHAURI NA. 44 LA 2019**

**ANTHONY MAGARI......................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SYLVIA CHARLES.............MJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

KWA:SYLVIA CHARLES

Mnafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 23/08/2019 katika Chumba cha Baraza, barabara ya Posta. Jengo liko mkabala na Mahakama Kuu ya Biashara, Tanzania.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 23/07/2019.

215364002

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MAN UNITED
## WAJITOSA KUMSAJILI ERIKSEN

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inafanyia kazi mpango wa kumsajili kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili Alhamisi wiki hii.

Wawakilishi wa Eriksen wana matumaini makubaliano ya usajili wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 yatakamilika kwa wakati.

United kwa sasa wanafanyia kazi haraka kuhusu wachezaji wanaowasajili, lakini watakuwa na muda hadi Septemba 2 kuuza wachezaji, akiwemo Paul Pogba kwa klabu za nje.

Hiyo ni kwa sababu dirisha la usajili kwa nchi za Ujerumani, Italia, Hispania na Ufaransa yanafungwa wiki tatu baada ya kufungwa lile la England.

Tottenham nao wanatarajia kukamilisha usajili wa kiungo wa Sporting Lisbon, Bruno Fernandes kwa muda muafaka kabla ya Ahamisi.

Spurs imekuwa ikihusishwa na mpango wa kumsajili nyota wa Real Betis, Giovani Lo Celso.

Eriksen awali alikuwa na matumaini ya kutua Real Madrid, lakini miamba hao wa Hispania wakahamishia nguvu zao kwa Pogba na nyota wa Ajax, Donny van de Beek. Kama Eriksen atabakia Tottenham hadi baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili Alhamisi, timu kama Juventus na Atletico Madrid watahamishia nguvu zao kumuwania mchezaji huyo.

Mkataba wa sasa wa Eriksen unamalizika mwaka 2020, hivyo Tottenham ina hatari ya kumpoteza mchezaji huyo akiwa huru kipindi kijacho cha majira ya joto.

# CANCELO ATUA ENGLAND KUJIUNGA MAN CITY

**MANCHESTER, England**

JOAO Cancelo amefikia hoteli ya The Lowry kwa ajili ya kukamilisha usajili wake wa kujiunga na Manchester City kutoka Juventus.

City inapanga kumsajili beki huyo wa kulia kwa pauni milioni 27.4 pamoja na kuwapa Danilo, ambaye ataelekea kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Cancelo pia ana uwezo wa kucheza nafasi ya beki wa kushoto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 anaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola.

Cancelo ambaye ni raia wa Ureno alijiunga na Juventus kutoka klabu ya Valencia mwaka jana.

Aliichezea mechi 34 Juventus msimu uliopita, akifunga mabao matano na kutoa pasi ya mwisho moja, na kuisaidia klabu hiyo kutwaa taji la Serie A pamoja na Supercoppa Italiana.

Kwa upande wake Danilo ameichezea mechi 60 klabu ya Man City tangu alipojiunga nayo mwaka 2017.

City imefanya usajili wa wachezaji wawili tu kipindi hiki cha majira ya joto, ambao ni Rodri aliyejiunga kutoka Atletico Madrid, huku beki Angelino akirudi kutoka PSV Eindhoven ya Uholanzi.



# BAYERN MUNICH SASA YAMGEUKIA BALE

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich imeripotiwa kwamba, sasa imehamishia nguvu zake kutaka kumsajili nyota wa Real Madrid, Gareth Bale wakati wakiangalia mbadala wa Leroy Sane.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales, hayupo kwenye mipango ya Zinedine Zidane pale Bernabeu na klabu hiyo sasa inataka kumuuza ili kupata fedha za kuingia sokoni.

Bayern sasa inataka kuongeza winga mpya baada ya kustaafu kwa Arjen Robben na Franck Ribery aliyemaliza mkataba wake.

Bayern imekuwa ikimuwania nyota wa Man City, Sane, lakini sasa gazeti la Hispania la AS limedai kwamba, Bavaria hao wanataka kumsajili Bale ndani ya saa 11 zijazo.

Real inataka kupata fedha za kumsajili Paul Pogba kutoka Manchester United na wanaamini kwamba mauzo ya Bale na James Rodriguez yanaweza kuwaingizia kiasi cha pauni milioni 100.

Bale uhamisho wake wa kwenda nchini China katika Klabu ya Jiangsu Suning ulikwama baada ya Real kuusitisha dakika za mwisho kwa sababu klabu hiyo ilitaka kumchukua bure bila ada.

Bale bado ana miaka mitatu kwenye mkataba wake wa sasa na Real Madrid.

Mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham alifunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho sita katika mechi 42 za mashindano msimu uliopita.



# KOSCIELNY

## NJIA NYEUPE KUTUA BORDEAUX



**BORDEAUX, Ufaransa**

NAHODHA wa Arsenal, Laurent Koscielny yupo hatika hatua za mwisho kujiunga na miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Bordeaux, kwa mujibu wa ESPN FC.

Beki huyo wa kati raia wa Ufaransa aliwasili nchini Ufaransa Jumatatu baada ya kufanya mazungumnzo yenye muelekeo mzuri kati ya klabu hizo mbili jijini London wiki iliyopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 alikuwa na imani kubwa kwamba Arsenal wangeweza kukamilisha makubaliano ya yeye kuruhusiwa kwenda Bordeaux baada ya kumuachia atue Ufaransa.

Makubaliano kati ya klabu hizo mbili yalikamilika Jumatatu wiki hii ili mchezaji huyo aweze kuondoka kwa miamba hao wa London.

Koscielny alitarajiwa jana Jumanne kufanyiwa vipimo vya afya yake kabla ya kusaini mkataba wa miaka mitatu, huku ada ya uhamisho wake ikitajwa kuwa ni euro milioni 5.

Mfaransa huyo alikataa kujiunga na Arsenal katika safari ya mandalizi ya msimu mpya nchini Marekani.

Kocha wa Arsenal, Unai Emery alitaka kumbakisha kwenye klabu hiyo, lakini Koscielny mwenyewe aliweka wazi kwamba hataki tena kuwachezea washika bunduki hao msimu ujao.

Baada ya kufanya mazoezi na timu ya vijana chini ya umri wa miaka 23 kwa mwezi mmoja, hatimaye alishinda mpango wake wa kutaka kurudi Ligue 1 ikiwa ni miaka nane baada ya kuondoka huko.

Koscielny alijiunga na Arsenal akitokea Lorient kipindi cha majira ya joto mwaka 2010 kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 10 na amecheza zaidi ya mechi 300 kwa klabu hiyo na kushinda mara tatu taji la FA.

## LIVERPOOL YAMSAJILI ADRIAN KUMSAIDIA ALISSON

**LONDON, England**

**LIVERPOOL imemsajili kwa uhamisho huru golikipa Adrian kwa ajili ya kumsaidia Alisson baada ya kuondoka kwa Simon Mignolet aliyejiunga na Club Brugge kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 8.**

**Kipa huyo mweye umri wa miaka 32 alikamilisa uhamisho wake wa kutua Anfield baada ya kufuzu vipimo vya afya yake na kukubaliana maslahi binafsi Jumatatu.**

**Amejiunga kwa mkataba wa miaka miwili na huku kukiwa na kipengele cha kuweza kuongeza mwaka mmoja zaidi.**

**"Nafikiri yeye ni suluhisho muhimu kwa wakati huu, kwani ana uzoefu wa kutosha," alisema kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp baada ya kukamilika kwa usajili huo wa Adrian.**

**"Hii ni muhimu kwetu. Yeye ni kipa ambaye anaijua vizuri Ligi Kuu ya England, ambaye ameichezea na anjua presha yake.**

**Akiwa ameachwa na West Ham kipindi hiki cha majira ya joto, Adrian alikuwa kwenye mpango wa kufanya mazungumzo na Real Valladolid, lakini alisitisha baada ya Liverpool kumpa ofa hiyo.**

**Adrian ameichezea West Ham jumla ya mechi 150 katika mashindano yote, huku jumla akicheza mechi 287 kwa ujumla ya yake tangu aanze kucheza soka.**



## WAYNE KUWA KOCHA MCHEZAJI DERBY

**LONDON, England**

WAYNE Rooney ametua nchini England kukamilisha mazungumzo ya kuhamia katika Klabu ya Derby.

Nahodha huyo wa zamani wa timu ya taifa ya England aliwasili katika uwanja wa ndege wa Heathrow Jumanne asubuhi na kuelekea kwenye dimba la Midlands kukamilisha mpango wake wa kuwa kocha mchezaji wa klabu hiyo ya ligi ya Championship.

Rooney amebakiwa na miaka miwili katika mkataba wake wa sasa na DC United baada ya kutumia mwaka mmoja kwenye Ligi Kuu ya Mrekani, MLS.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 aliwahi kuzungumza hadharani mpango wake wa kutaka kuwa kocha mara baada ya kustaafu kucheza, na sasa mpango wake huo wa kutua Derby ni nafasi kwake ya kuanza kipindi maisha mapya ya ukocha.

Rooney alikuwa anavutiwa mno na mbinu za kocha, Louis van Gaal wakati alipokuwa pale Manchester United, na ameshawishiwa na kocha wa sasa wa Derby, Philip Cocu.


Anaona mpango huo kama nafasi ya kuanza kutafuta uzoefu wa kazi ya ukocha, huku pia akirudi nyumbani England kuwa karibu na familia yake.

Kama mazungumzo yalikwenda vizuri, alitarajiwa jana Jumanne kutangazwa kuwa kocha mchezaji wa Derby.

Dirisha la usajili kwa ligi ya championships linafungwa sawa la lile la Ligi Kuu ya England Alhamisi wiki hii.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK AMTAHADHARISHA MAGUIRE DAU KUBWA UTD

Ni vigumu kuzima presha zote, lakini mara zote zingatia tu kucheza mchezo wako bora na...

**LIVERPOOL, England**

Virgil van Dijk amemuonya Harry Maguire kwamba kutua kwake Manchester United kuna maana ya presha baada ya kuwa beki ghali zaidi duniani.

Maguire ameondoka Leicester City na kujiunga na miamba ya Ligi Kuu England Manchester United kwa dau la pauni milioni 80 ambalo ni rekodi ya dunia kwa upande wa mchezaji wa nafasi ya beki, hiyo ikiwa ni baada ya tetesi hizo kudumu kwa mwezi mmoja sasa.

Nyota huyo wa kimataifa wa England, ambaye ametia saini mkataba wa miaka sita huku kukiwa na mbadala wa kuongeza kwa msimu mmoja zaidi hapo Old Trafford, dau hilo la kujiunga na United linaaminika sasa kupiku pauni milioni 75 za Liverpool ilizolipa kwa Southampton wakati ikimsajili Van Dijk Januari mwaka jana.

Van Dijk, ambaye ameiongoza Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19, anajua kuwapo kwa presha zinazotokana na kusajiliwa kwa dau kubwa na ametoa ushauri kwa Maguire.

"Bahati nzuri kwake," alisema. "Siwezi kusema chochote kuhusu hilo kwa sababu kila mara kutakuwa na wakati ambapo itabadilika.

"Hilo ndilo soko. Yeye hana ushawishi wowote kwa hilo, lakini ninamtakia kila la heri. Dau linakuja na presha, lakini haibadili sana kwa sababu mara zote unakuwa na presha katika klabu kubwa kama Man United. Lakini ninamtakia heri."

"Zingatia tu kufanya kile unachopenda kufanya na kucheza mchezo wako bora," Van Dijk alisema wakati alipoulizwa ni kwa namna gani alivyoweza kwenda na presha ya kununuliwa kwa dau kubwa. "Chukua ubora wako nje ya uwanja, furahia mchezo wako na usifikiri kuhusu mambo mengine.

"Si rahisi kuzima kabisa presha zote. Binafsi, napenda kuweka mambo katika mtazamo. Vitu vingi sana ni muhimu zaidi kuliko kucheza soka na kile tunachofanya, tumebarikiwa.

"Tunaweza kufanya kile tunachopenda kufanya na pia kuichezea Liverpool - ni klabu kubwa kama hii. Unahitaji kufurahia hilo, lakini shinikizo litakuwapo kila wakati."

Kutua kwa Maguire Old Trafford, kunamfanya kuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa na Kocha Ole Gunnar Solskjaer majira haya ya joto kufuatia kuwanasa winga Daniel James na beki wa kulia Aaron Wan-Bissaka wakitokea Swansea City na Crystal Palace.

"Ni mwenye furaha kujiunga na klabu hii kubwa," Maguire alisema katika taarifa yake iliyotolewa na United.

"Nimefurahia sana wakati wangu nikiwa Leicester na ningependa kushukuru kila mtu kwenye klabu, na mashabiki, kwa msaada wao mzuri katika misimu miwili iliyopita. Hata hivyo, wakati Manchester United inakuja kugonga mlango wako, ni fursa nzuri sana.

"Kutoka kwa mazungumzo yangu na kocha, ninafurahi juu ya maono na mipango aliyonayo kwa timu hiyo. Ni wazi kuona kwamba Ole anaunda timu ya kushinda mataji.

"Sasa ninatarajia kukutana na wachezaji wenzangu wa timu mpya na kuanza msimu."

## KWA UFUPI

**ZAHA AFIKIA PAUNI MIL.100**

Everton imefanya jumla la dau la kuipata saini ya winga wa Crystal Palace, Wilfried Zaha, 26, kwa pamoja kuwa pauni milioni 100, ikimjumuisha mshambuliaji wa Uturuki, Cenk Tosun na kiungo wa Jamhuri ya Ireland, James McCarthy, kila mmoja akiwa na umri wa miaka 28. ***(Sun)***

**JUVE YAMPANIA POGBA**

Juventus inajiandaa kuwatoa ofa wachezaji watatu katika kubadilishana na Manchester United ili kumpata kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26. ***(Mirror)***

**KOSCIELNY ATUA BORDEAUX**

ARSENAL imekubali kumuuza Laurent Koscielny, 33, kwa Bordeaux na tayari amesaini mkataba wa miaka mitatu. ***(Get French Football News, via Sun)***

**UNITED YAMGEUKIA ERIKSEN**

Manchester United inakaribia kuipata saini ya kiungo wa Tottenham na Denmark, Christian Eriksen, 24, baada ya kiungo wa Sporting Lisbon na Ureno, Bruno Fernandes - ambaye alikuwa akiwindwa na miamba hiyo ya Old Trafford - kuweka wazi kuwa anavutiwa kujiunga na Spurs. ***(AS)***

**ROONEY ATUA KUTETA NA DERBY**

Burnley imekuwa ikihusishwa na kwenda kumsajili mshambuliaji wa DC United na nahodha wa zamani wa kimataifa wa England, Wayne Rooney, 33, lakini straika huyo pia ametua kwa mazungumzo ya kuwa kocha mchezaji wa Derby County. ***(Burnley Express)***

**LEICESTER KUMPOTEZEA AKE**

Leicester City haitamsajili beki Nathan Ake katika dirisha hili la usajili, na Bournemouth ikimthaminisha Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 24 na zaidi ya pauni milioni 75. ***(Sky Sports)***

**RODRI KUMBADILI FERNANDINHO**

KIUNGO wa Manchester City, Mbrazil Fernandinho, 34, amethibitisha atakuwa akitumika kama beki wa kati katika baadhi ya mechi msimu huu, kufuatia kutua kwa kiungo Mhispania Rodri, 23, kutoka Atletico Madrid. ***(Manchester Evening News)***

**DRINKWATER AIVUTIA NORWICH**

Norwich City inavutiwa na huduma ya kiungo wa Chelsea na England, Danny Drinkwater, 29, ambaye hahitajiki Stamford Bridge. ***(Mail)***

**UPAMECANO KUGEUKIWA ARSENAL**

Arsenal inaweza kumgeukia beki wa kati wa RB Leipzig, Mfaransa Dayot Upamecano, 20, kama mbadala endapo itamkosa beki wa Juventus, Daniele Rugani - lakini itakimbizwa na dau la thamani ya pauni milioni 50 inayotaka klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Mirror)***

**VERTONGHEN AKUNWA SPURS**

BEKI wa Tottenham, Mbelgiji Jan Vertonghen, 32, amesisitiza ni mwenye furaha hapo kaskazini mwa London wakati huu akiingia mwaka wa mwisho kwenye mkataba wake. ***(Goal.com)***

**BURNLEY YAKATALIWA KWA FRY**

Middlesbrough imekataa ofa ya pauni milioni nane kutoka kwa Burnley kwa beki wao anayeichezea England U-21, Dael Fry, 21. ***(Sky Sports)***



HABARI MICHEZO

# KMC YAWAFUMUA WALIOISHIKA YANGA

Na Mwandishi Wetu

PAMOJA na kuonyesha umwamba mbele ya Yanga kwa kuilazimisha sare ya bao 1-1 Jumapili wakati wa kilele cha Wiki ya Mwanachi iliyofanyika Uwanja wa Taifa, mabingwa wa SportPesa Cup, Kariobangi Sharks ya Kenya, wamekubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya KMC jana.

Jumapili Yanga ililazimika kusubiri hadi dakika ya 57 kuweza kusawazisha kwa mkwaju wa penalti bao la Patrick Otieno aliyelizamisha kimyani dakika ya 48 ya mchezo huo wa kirafiki.

Penalti hiyo ya Yanga ilizamishwa nyavuni na kiungo wao mpya, Patrick Sibomana aliyesajiliwa msimu huu.

Lakini katika mechi ya jana iliyopigwa Uwanja wa Uhuru asubuhi, Kariobangi ilikutana na moto mkali wa KMC inayojiandaa na mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya AS Kigali ya Rwanda mwishoni mwa wiki.

Katika mechi hiyo ya jana, mabao ya KMC yalizamishwa kimyani na Serge Nogues pamoja na Vitalis Mayanga.

Akizungumzia mechi hiyo, Afisa Habari wa KMC, Anwar Bide, alisema mechi hiyo ni mwanzo mzuri kwao kuelekea mchezo wa kimataifa dhidi ya AS Kigali utakaochezwa Jumamosi nchini Rwandwa.

"Ilikuwa mechi ngumu na yenye ushindani mkubwa, lakini hatimaye tumeibuka na ushindi wa mabao 2-1, huu ni mwanzo mzuri kwetu kwa ajili ya michezo yetu ya kimataifa na tunatumai kufanya vizuri," alisema.

Katika hatua nyingine, Anwar alisema timu hiyo inatarajia kuondoka kesho alfajiri kuelekea Rwanda tayari kwa ajili ya mechi hiyo.




Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Geofrey Tengeneza, (wa pili kushoto) akionyesha fulana maalumu ya mbio za Rock City Marathon msimu wa 2019 kwa wageni waalikwa wakati wa uzinduzi wa mbio hizo uliofanyika jana jijini Dar es Salaam. Wanaoshuhudia ni pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mbio hizo, Clement Mshana (wa pili kulia) Mratibu wa mbio hizo kutoka Kampuni ya Capital Plus International (CPI), Kasara Naftali (wa kwanza kulia) Pamoja na muwakilishi kutoka Chama cha Riadha Tanzania (RT), Ombeni Zavara. MPIGAPICHA WETU

# Bodi ya Utalii kuibeba Rock City Marathon 2019

Na Mwandishi Wetu

BODI ya Utalii Tanzania (TTB), imeahidi kushirikiana na waandaaji wa mbio za Rock City Marathon ili kuhakikisha mbio hizo zinatumika vema kuutangaza utalii wa ndani hapa nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa unzinduzi wa msimu wa kumi (10) wa mbio hizo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Devota Mdachi, Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa TTB, Geofrey Tengeneza alisema adhma hiyo inasukumwa na malengo ya mbio hizo ambayo ni kutumia mchezo wa riadha katika kutangaza utalii hususan katika Kanda ya Ziwa.

Hafla hiyo iliyofanyika kwenye viunga vya Ofisi za TTB jijini Dar es Salaam, ilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa mchezo huo wakiwamo viongozi wa serikali pamoja na wadhamini mbalimbali wa mbio hizo.

"Kwa kuzingatia uzito wa malengo ya mbio hizi nitamke bayana kuwa TTB tupo tayari kushirikiana na waandaaji wa mbio hizi kuhakikisha kwamba mwaka huu mbio hizi zinafana na zinavutia washiriki wengi zaidi hususan wa kimataifa," alisema Tengeneza.

Tengeneza pia alithibitisha ushiriki wake pamoja na viongozi waandamizi wa bodi hiyo kwenye mbio hizo zinazoratarajiwa kufanyika Oktoba 20, mwaka huu kwenye viunga vya jengo la kibishara la Rock City Mall, jijini Mwanza ambapo washiriki wa mbio hizo watapita katika barabara mbalimbali za jiji hilo kabla hazijamalizikia katika viunga hivyo.

Mbali na ushiriki huo, Tengeneza pia alitoa pongezo kwa mashirika mbalimbali yenye dhamana ya utalii hapa nchini ikiwamo Hifadhi za Taifa(Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)kwa kuwa sehemu ya wadau wakubwa wa mbio hizo.

"Ukanda wa Ziwa una vivutio vingi ambavyo sisi kama chombo chenye dhamana ya utalii, lazima tuendelee kuvitangaza kwa nguvu na kwa njia tofauti ikiwamo michezo," alisema Tengeneza huku akivitaja baadhi ya vivutio hivyo kuwa ni pamoja na Kisiwa cha Saanane, Makumbusho ya kabila la Wasukuma pamoja na tamaduni za makabila ya wakazi wa Kanda ya Ziwa.

Mbio za Rock City Marathon zilizoanzishwa miaka 10 iliyopita zinazozidi kujiongezea umaarufu kila mwaka, tayari zimefanikiwa kuwavutia baadhi ya wadhamini ikiwa ni pamoja na Kampuni za TIPER, Pepsi, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Tanapa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Wadhamini wengine ni pamoja na Kampuni ya Uwakili ya Lis Law Chambers & Consultants, TFS, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), CF Hospital, Mwanza Water, Isamilo Lodge, Pigeon Hotel, Real PR Solutions Limited na Afrimax Strategic Partnerships Limited.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mbio hizo kutoka Kampuni ya Capital Plus International waandaaji wa mbio hizo, Clement Mshana alitoa wito kwa washiriki wa ndani hususan wa mikoa ya Kanda ya Ziwa pamoja na wadhamini kujitokeza kwa wingi kushiriki katika mbio hizo ambazo kwa mwaka jana zilifanikiwa kuhusisha washiriki zaidi ya 3000.

Alisema mbio za mwaka huu zinatarajiwa kuhusisha washiriki wengi zaidi kutoka kila kona ya dunia ikiwamo Afrika, Ulaya, China, Mashariki ya Kati hususan Israel na Marekani huku akitoa wito kwa washiriki wa ndani kujisajili kwa wingi ili kuthibitisha ushiriki wao kwenye mbio hizo.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Mshauri wa masuala ya Ufundi wa mbio hizo, John Bayo alisema maandalizi ya mbio hizo kwa sasa yamekamilika kwa asilimia 60 huku akitumia uzinduzi huo kuonyesha fulana na medali zitakazotumika katika msimu wa mbio hizo kwa mwaka huu.

# Azam kwa Waethiopia kwa tahadhari kubwa

Na Shufaa Lyimo

AZAM FC imeondoka jana majira ya saa 10 usiku, kuelekea nchini Ethiopia tayari kwa mechi yao ya raundi ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Fasil Katema (Ethiopia 1) ya Ethiopia utakaopigwa Jumapili wiki hii huku ikieleza watashuka dimbani kwa tahadhari kubwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa AZAM FC, Jafari Idd Maganga, alisema msafara wa timu hiyo umeondoka na Shirika la Ndege la Ethiopia ambapo utashukia jijini Addis Ababa kabla ya kuanza safari kuelekea Gondar kaskazini mwa Ethiopia itakapopigwa mechi hiyo.

"Wachezaji wote wana morali ya ushindi katika mchezo wetu wa kwanza, tumecheza michezo mingi ya kirafiki ambayo imewajenga kwa kiasi kikubwa,"alisema Jafari.

Aliongeza kusema kuwa, Mtendaji wao Mkuu, Abdul Karim Amin alitangulia mapema kuweka mambo sawa ikiwa ni pamoja na uwanja wa mazoezi pamoja na hoteli watakayoshukia lakini pia kusoma hali ya hewa ya huko.

**Alisema kwa mujibu wa mtendaji huyo, ame wafahamisha kwamba kuna baridi kali, hivyo wachezaji imebidi ku jiandaa kukabiliana na hali hiyo, ikiwa ni pamoja na kubeba vifaa mbalimbali vya kutumia katika mchezo huo am bavyo vitawasaidia ku kabiliana na hali hiyo ya baridi.**

Alisema kwa upande wa wachezaji walioKuwa kwenye majukumu ya timu ya Taifa (Taifa Stars) wote wamejiunga na wenzao katika msafara huo.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mrundi Etienne Ndayiragije alisema wachezaji wake wapo vizuri kuelekea katika mchezo huo na ana matumaini makubwa ya ushindi.

Alisema wanakwenda kucheza kwa tahadhari kubwa ukizingatia hiyo ni mechi ya kwanza kwao kimataifa ugenini kwa msimu huu.

"Tunakwenda kucheza kwa tahadhari kwa sababu tutakuwa ugenini, lengo ni kutimiza ndoto zetu," alisema Ndayiragije.

# Michezo

Jumatano Agosti 7, 2019
Nipashe



Van Dijk amtahadharisha Maguire dau kubwa Utd HABARI UK 30



Baadhi ya mashabiki wa Simba waliohudhuria tamasha la kilele cha SportPesa Simba Wiki Uwanja wa Taifa jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# SIMBA SC YATETEMESHA NCHI

Waziri Mkuu afunguka kauli ya Magufuli, awataka mashabiki kumuunga mkono Mo, Jumanne yageuka kuwa wikiendi ...

**Na Mwandishi Wetu**

WEKA mbali matokeo ya mechi ya jana kati ya Simba na wageni zao, Power Dynamos ya Zambia kwenye mechi ya kilele cha SportPesa Simba Wiki, ambayo kila mmoja hadi kufikia muda huu anafahamu matokeo ya mechi hiyo iliyokuwa kali na ya kuvutia, kwani shughuli pevu na burudani tosha ni namna tamasha hilo lilivyofana kila idara.

Tofauti na ilivyotarajiwa kuwa ni siku ya kazi watu wangekuwa wachache, Jumanne ilionekana kama mwishoni mwa wiki, huku Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda akisema hiyo ndiyo shughuli yenyewe.

Simba ina kila sababu ya kujiita mhasisi wa tamasha hilo hapa nchini ambalo kwa mara ya kwanza watani zao, Yanga walimefanya mwaka huu kwa kulihitimisha Jumapili iliyopita kwa kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya na kutoka sare ya bao 1-1.

Kama ambavyo, Simba imekuwa ikitamba kwa kaulimbiu yao ya "Iga Ufe" kabla ya tamasha hilo, ndivyo ambavyo ilionyesha mambo tofauti kabisa na kila kitu kikionekana kuwa katika mpangilio mzuri wa kuvutia kwenye ratiba yao, tofauti na ile ya Yanga juzi ambayo muda mwingine kulionekana kukiwa hakuna tukio linaloendelea.

Lakini huwezi kuilaumu Yanga kwa mapungufu hayo, kwani yalichangiwa na ugeni wao wa tukio kubwa kama hilo, tofauti na Simba ambayo huu ni mwaka wao wa 10 kuendesha tamasha hilo la Simba Day.

Mgeni Rasmi katika tamasha hilo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, alieleza kuwa Rais John Magufuli anataka makombe likiwamo la Afrika na akaitaka Simba kwenda kufanya hivyo.

Aidha, Majaliwa alisema serikali ipo pamoja na wawekezaji katika klabu za Tanzania na akawataka mashabiki wa Simba waliopo uwanjani hapo kuendelea kumuunga mkono mwekezaji wao, Mohamed 'Mo' Dewji ili aweze kuiletea klabu hiyo maendeleo.

Alisema serikali itaendelea kuunga mkono wawekezaji kwa kuwa inataka kuona klabu za Tanzania zikipata maendeleo kama za Ulaya.

**UWANJA WAANZA KUJAA SAA 4**

Uwanja wa Taifa ulianza kufurika mashabiki kuanzia saa 4 asubuhi, huku kufikia majira ya saa sita tiketi za Sh. 5,000 zikielezwa kumalizika na ilipofika saa nane kwa watoto wa mjini husema "uwanja umetapika".

**TIKETI ZOTE ZAISHA SAA 11:30**

Tiketi zote zilizoandaliwa kwa ajili ya kilele cha SportPesa Simba Wiki, katika Uwanja wa Taifa unaochukua watazamani 60,000, ilipofika saa 11:30 jioni ziliripotiwa kumalizika kuelekea mechi yao iliyoanza saa 12:00 jioni.

**BURUDANI MWANZO MWISHO**

Achana na wasanii wa maigizo walioburudisha vilivyo kwa nyakati mbalimbali, Bendi ya Twanga Pepete ilitoa burudani mubashara uwanjani hapo na hakuna aliyejutia kiingilia chake.

**SIMBA QUEENS, SIMBA B ZASHINDA**

Katika kilele hicho cha SportPesa Simba Wiki, ambacho mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, Simba Queens ilifungua ushindi kwa kuwachapa wanadada wenzao wa JK Park kwa bao 1-0 huku wakionyesha kandanda safi.

Simba Queens ambayo hiyo ni mechi yao ya kwanza hapa nchini tangu ilipotokea katika ziara ya kimafunzo na maandalizi ya msimu mpya nchini Ujerumani, ilipata bao hilo kupitia kwa Mwanahamisi Omary 'Gaucho' katika dakika 27.

Kwa upande wa Simba B iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Fountain Gate Academy ya Dodoma.

**UTAMBULISHA WAFUNIKA**

utamu ulianza kunoga wakati Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alipoanza kutambulisha benchi la ufundi la Simba, likiongozwa na Kocha Mbelgiji Patrick Aussems, na wachezaji wa kikosi hicho kwa msimu wa 2019/20.

Mashabiki wa Simba walijawa na furaha huku wakisimama kushangilia wakati huo wakichagizwa na wimbo maalum wa timu hiyo ulioimbwa na Tunda Man akishirikiana na Mrisho Mpoto.

**BOCCO ALA BIRTHDAY UWANJANI**

Mshambuliaji John Bocco aliimbiwa wimbo wa kusherehekea siku yake ya kuzaliwa huku mashabiki wote wakisimama na kushangilia kwa furaha.

**CHAMA APEWA HESHIMA MAALUM**

Kiungo Mzambia Clatous Chama alitambulishwa kipekee huku mashabiki wote wakitakiwa kusimama kumpa heshima ya kipekee kutokana na juhudi zake za kuifungia mabao muhimu yaliyoivusha Simba hatua ya makundi na robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika.

**MO AFUNGA HESABU**

Utambulisho wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji, uliwainua mashabiki wote uwanjani kumshangilia huku akichagiza kwa kusema This is Sisisimbaaa... na kushangiliwa na mashabiki wa timu hiyo.

Mo alizunguka uwanja mzima akiwapungia mashabiki kabla ya kurejea uwanjani na kusalimiana na wachezaji wa benchi la ufundi.

Kwa ujumla ilikuwa zaidi ya burudani kabla ya mechi hiyo kuanza kwani kila kitu kilikuwa cha kuvutia.

**MAKONDA AZUNGUMZIA UWANJA KUJAA**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda alipoulizwa uwanja umejaa kwa maana watu hawana shughuli za kufanya? Alijibu: "Shughuli za kufanya wanazo na shughuli yenyewe ndiyo hii."

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042